

**KANUNI ZA LUGHA ZINAVYOATHIRI SOMO LA KISWAHILI  
KATIKA SHULE ZA UPILI: MFANO WA KAUNTI YA BUSIA**

**ELIZABETH AUMA OSODO**

**C50/CE/28181/2013**

**TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTIMIZA BAADHI YA MAHITAJI YA  
SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA KENYATTA**

**APRILI, 2025**

## UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijatolewa kwa mahitaji ya shahada katika chuo kingine.

SAHIHI:  TAREHE: 16/4/2025

**ELIZABETH AUMA OSODO**

**CSO/CE/28181/2013**

Tasnifu hii imetolewa kwa idhini yangu kama msimamizi aliyeteuliwa na Chuo Kikuu cha Kenyatta.

SAHIHI:  TAREHE: 16.4.2025

**PROF. PAMELA MUHADIA Y. NGUGI**

**IDARA YA KISWAHILI**

**CHUO KIKUU CHA KENYATTA**

## **TABARUKU**

Kazi hii naitabaruku kwa wanangu Kigan Keita na Kaila Machel kwa uvumilivu wao wakati nilipoanza safari hii ya masomo. Kila wakati walinitia moyo. Mungu awalinde daima dawamu.

## SHUKRANI

Shukrani zangu kwa Mwenyezi Mungu kwa kunijalia akili razini na afya njema wakati nilipokuwa nikifanya utafiti huu hadi nikaukamilisha. Vilevile ningependa kumshukuru msimamizi wangu Prof. Pamela Ngugi kwa uvumilivu, ushauri na uelekezi wake mwema ulioniwezesha kuiboresha kazi hii na kuikamilisha. Aidha, namshukuru Dkt. Mirriam Osore aliyenielekeza na kunishauri nilipoanza uandishi wa tasnifu hii. Sitasahau kuwashukuru wahadhiri wengine katika idara ya Kiswahili kwa kuweka msingi dhabiti mwanzo wa kozi.

Fauka ya hayo, ningependa kuwashukuru wanangu kwa kuvumilia upweke wa kukosa malezi ya mama kila mara niliposafiri kwa ajili ya kufanikisha masomo yangu. Namshukuru mamangu mzazi Felesta Amollo kwa kuniombea kila mara hasa nilipokumbana na changamoto mbalimbali katika kazi hii. Namshukuru pia ndugu yangu Dkt. Boniface Osodo kwa kunielimisha, kunihimiza na kuhakikisha kwa vyovyote vile ndoto yangu ya elimu imetimia. Shukrani kwa walimu na wanafunzi wa shule mbalimbali nilizofanyia utafiti, bila wao huenda malengo ya utafiti huu hayangetimia. Wote walionitilia pondo katika mchakato mzima wa kuufanya utafiti huu na ambao sikuwataja, shukrani jazila.

## UFAFANUZI WA ISTILAHU

**Kanuni-** Ni sheria zilizopitishwa na taasisi, shirika au bunge.

**Kanuni za lugha shuleni** – ni sheria zilizowekwa shuleni ili kuwaongoza wanafunzi katika matumizi yao ya lugha wanapowasiliana shuleni.

**Mielekeo** – Ni ile hali ya kupenda au kuchukia kitu au jambo.

**Mielekeo chanya** – Ni ile hali ya kupenda kitu au jambo.

**Mielekeo hasi** – Ni ile hali ya kuchukia au kudharau kitu au jambo.

**Mielekeo ya lugha** – Ni ile namna ya kuipenda au kuichukia lugha.

**Motisha** – Ari na hamu ya kufanya kitu au jambo.

**Shule za Kitaifa (*National schools*)** – Ni shule za kiwango cha juu zenye ufanisi zinazoteua wanafunzi kutoka sehemu tofauti za nchi kwa madhumuni ya kuleta umoja wa taifa na mshikamano wa jamii. Huwa za bweni.

**Shule za Kaunti za kiwango cha juu (*Extra County schools*)** – Ni shule za upili zinazopokea wanafunzi kutoka kaunti mbalimbali lakini kwa kiasi kikubwa zinahudumia wanafunzi wa kaunti zao pamoja na baadhi kutoka nje. Zinachukua nafasi ya pili baada ya shule za Kitaifa kwa hadhi na rasilimali.

**Shule za Kaunti (*County schools*)** - Ni shule ambazo wanafunzi wengi huteuliwa katika Kaunti husika. Huwa za kutwa na bweni.

## **ORODHA YA VIFUPISHO**

**K.C.P.E-** Kenya Certificate of Primary Education

**K.C.S.E -** Kenya Certificate of Secondary Education

**K.N.E.C-** Kenya National Examination Council

**NACOSTI** – National Commission for Science Technology and Innovation

**TUKI** – Taasisisi ya Uchunguzi wa Kiswahili

**KNDC-** Kenya National Debates Council

## YALIYOMO

|   |             |
|---|-------------|
| <b>UNGAMO</b> .....   | <b>ii</b>   |
| <b>TABARUKU</b> .....   | <b>iii</b>  |
| <b>SHUKRANI</b> .....   | <b>iv</b>   |
| <b>UFAFANUZI WA ISTILAHU</b> .....  | <b>v</b>    |
| <b>ORODHA YA VIFUPISHO</b> .....  | <b>vi</b>   |
| <b>YALIYOMO</b> .....   | <b>vii</b>  |
| <b>ORODHA YA MAJEDWALI</b> .....  | <b>xi</b>   |
| <b>ORODHA YA GRAFU NA CHATI</b> .....   | <b>xiii</b> |
| <b>ORODHA YA VIELELEZO</b> .....  | <b>xiv</b>  |
| <b>ORODHA YA VIAMBATISHO</b> .....  | <b>xv</b>   |
| <b>IKISIRI</b> .....  | <b>xvi</b>  |
| <b>ABSTRACT</b> .....   | <b>xvii</b> |
| <b>SURA YA KWANZA</b> .....   | <b>1</b>    |
| <b>UTANGULIZI</b> .....   | <b>1</b>    |
| 1.0 Usuli wa Mada .....   | 1           |
| 1.1 Suala la utafiti .....  | 6           |
| 1.2 Malengo ya Utafiti .....  | 7           |
| 1.3 Maswali ya Utafiti .....  | 8           |
| 1.4 Sababu za Kuchagua mada ya Utafiti .....  | 8           |
| 1.5 Upeo na Mipaka ya Utafiti.....  | 9           |
| 1.6 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada .....   | 10          |
| 1.6.1 Tafiti Bayana Kuhusu Mielekeo ya Watu Tofauti Kuhusu Lugha ya<br>Kiswahili..... | 11          |
| 1.6.2 Tafiti kuhusu Vipengele Vinavyoathiri Lugha ya Kiswahili .....                  | 17          |
| 1.7 Misingi ya Nadharia.....  | 23          |
| 1.7.1 Nadharia ya Vitendo Vilivyofikiriwa .....                                       | 23          |
| 1.7.2 Nadharia ya Kijumuia na Kibinadamu.....   | 26          |
| 1.8. Mbinu za Utafiti.....  | 28          |
| 1.8.1. Muundo wa Utafiti .....  | 28          |
| 1.8.2 Mahali pa Utafiti .....   | 29          |
| 1.8.3 Uteuzi wa Sampuli .....   | 30          |

|  |           |
|--|-----------|
| 1.8.4 Ukusanyaji wa Data .....   | 32        |
| 1.8.4.1 Mahojiano .....  | 32        |
| 1.8.4.2 Uchunzaji.....   | 33        |
| 1.8.4.3 Hojaji .....   | 33        |
| 1.8.4.4 Majadiliano Elekezi ya Vikundi .....   | 34        |
| 1.8.4.5 Matokeo ya Mtihani wa Kitaifa.....   | 35        |
| 1.8.5 Uchanganuzi wa data .....  | 36        |
| 1.8.6 Uwasilishaji wa Matokeo.....   | 37        |
| 1.8.7 Maadili ya utafiti .....   | 37        |
| 1.9 Hitimisho .....  | 38        |
| <b>SURA YA PILI .....</b>  | <b>39</b> |
| <b>KANUNI ZA LUGHA KATIKA SHULE ZA UPILI .....</b>                                   | <b>39</b> |
| 2.0 Utangulizi.....  | 39        |
| 2.1 Kanuni za lugha katika shule .....   | 39        |
| 2.1.1 Lugha ya mawasiliano katika mazingira ya shuleni .....                         | 41        |
| 2.1.2 Siku za Kiswahili .....  | 44        |
| 2.1.3 Mabango na maandishi katika mazingira ya shule .....                           | 49        |
| 2.1.4 Matumizi ya lugha ya Kiswahili katika mijadala.....                            | 51        |
| 2.1.5 Shughuli za idara ya Kiswahili .....   | 55        |
| 2.1.5.1 Vipindi vya ziada.....   | 56        |
| 2.1.5.2 Makongamano ya ndani na nje ya shule.....                                    | 59        |
| 2.1.5.3 Kusoma vitabu na magazeti ya Kiswahili .....                                 | 65        |
| 2.1.5.4 Vyama vya Kiswahili .....  | 68        |
| 2.2 Hitimisho .....  | 71        |
| <b>SURA YA TATU .....</b>  | <b>73</b> |
| <b>MIELEKEO YA WANAFUNZI NA WALIMU KUHUSU KANUNI ZA LUGHA SHULENI .....</b>          | <b>73</b> |
| 3.0 Utangulizi.....  | 73        |
| 3.1 Uchanganuzi wa mielekeo ya wanafunzi kuhusu kanuni za lugha shuleni ..           | 74        |
| 3.1.1 Lugha ya mawasiliano katika mazingira ya shule .....                           | 74        |
| 3.1.2 Siku za Kiswahili .....  | 85        |
| 3.1.2.1 Adhabu za ukiukaji wa kanuni za lugha za shule kuhusu siku ya Kiswahili..... | 87        |

|  |            |
|--|------------|
| 3.3.3 Mabango na maandishi katika mazingira ya shule. ....                                   | 90         |
| 3.1.4 Matumizi ya lugha ya Kiswahili katika mijadala.....                                    | 92         |
| 3.1.5 Shughuli za idara.....   | 94         |
| 3.1.5.1 Vyama vya Kiswahili .....  | 95         |
| 3.1.5.2 Vipindi vya ziada.....   | 96         |
| 3.1.5.3 Makongamano ya ndani na nje ya shule.....  | 98         |
| 3.1.5.4 Usomaji wa vitabu vya hadithi na magazeti ya Lugha ya<br>Kiswahili .....             | 102        |
| 3.2 Uchanganuzi wa mielekeo ya walimu kuhusu kanuni za lugha shuleni.....                    | 105        |
| 3.2.1. Lugha ya mawasiliano katika mazingira ya Shule.....                                   | 105        |
| 3.2.2 Siku za Kiswahili .....  | 110        |
| 3.2.3 Mabango na maandishi katika mazingira ya shule .....                                   | 112        |
| 3.2.4 Matumizi ya lugha ya Kiswahili katika mijadala shuleni .....                           | 113        |
| 3.2.5 Shughuli za idara ya Kiswahili .....   | 115        |
| 3.2.5.1 Vipindi vya ziada.....   | 115        |
| 3.2.5.2 Makongamano ya ndani na nje ya shule.....  | 117        |
| 3.2.5.3 Usomaji wa magazeti na vitabu vya hadithi kwa lugha ya<br>Kiswahili .....            | 120        |
| 3.2.5.4. Vyama vya Kiswahili .....   | 121        |
| 3.2.5.5 Uteuzi wa kanuni za lugha za shule .....   | 122        |
| 3.3 Hitimisho .....  | 124        |
| <b>SURA YA NNE .....</b>   | <b>126</b> |
| <b>ATHARI YA KANUNI ZA LUGHA SHULENI KWA SOMO LA<br/>            KISWAHILI .....</b>         | <b>126</b> |
| 4.0. Utangulizi.....   | 126        |
| 4.1 Matokeo ya mtihani wa wanafunzi katika somo la Kiswahili .....                           | 126        |
| 4.2 Athari ya kanuni za lugha za shule katika somo la Kiswahili .....                        | 128        |
| 4.2.1 Athari ya lugha ya mawasiliano katika mazingira ya shule kwa somo<br>la Kiswahili..... | 129        |
| 4.2.2 Athari ya siku za Kiswahili katika somo la Kiswahili .....                             | 135        |
| 4.2.2.1 Matumizi ya lugha ya Kiswahili mara tatu kwa wiki ....                               | 135        |
| 4.2.2.2 Matumizi ya lugha ya Kiswahili mara moja kwa<br>muhula.....                          | 138        |

|  |            |
|--|------------|
| 4.2.2.3 Matumizi ya lugha ya Kiswahili kila siku shuleni .....                             | 139        |
| 4.2.2.4 Athari ya maoni ya walimu kuhusu Siku ya Kiswahili .                               | 140        |
| 4.2.2.5 Athari ya adhabu katika somo la Kiswahili.....                                     | 142        |
| 4.2.3 Athari ya mabango na maandishi katika mazingira ya shule kwa somo la Kiswahili ..... | 145        |
| 4.2.4 Athari ya matumizi ya lugha ya Kiswahili katika mijadala kwa somo la Kiswahili.....  | 147        |
| 4.2.5 Athari ya shughuli za idara ya Kiswahili kwa somo la Kiswahili.....                  | 149        |
| 4.2.5.1 Athari ya vipindi vya ziada kwa somo la Kiswahili.....                             | 150        |
| 4.2.5.2 Athari ya makongamano ya ndani na nje kwa somo la Kiswahili .....                  | 155        |
| 4.2.5.2.1. Athari ya Makongamano ya ndani ya shule kwa somo la Kiswahili .....             | 156        |
| 4.2.5.2.2. Athari ya Makongamano ya nje ya shule kwa somo la Kiswahili. ....               | 158        |
| 4.2.5.3 Athari ya vyama vya Kiswahili kwa somo la Kiswahili                                | 161        |
| 4.2.5.4 Athari ya usomaji wa vitabu na magazeti kwa somo la Kiswahili .....                | 163        |
| 4.4 Hitimisho .....  | 165        |
| <b>SURA YA TANO.....</b>   | <b>166</b> |
| <b>HITIMISHO, MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UTAFITI.....</b>                                   | <b>166</b> |
| 5.0. Utangulizi.....   | 166        |
| 5.1 Muhtasari wa utafiti .....   | 166        |
| 5.2 Matokeo ya utafiti .....   | 169        |
| 5.3 Changamoto za utafiti .....  | 172        |
| 5.4 Mchango wa utafiti .....   | 172        |
| 5.5 Mapendekezo .....  | 173        |
| <b>MAREJELEO.....</b>  | <b>175</b> |
| <b>VIAMBATISHO.....</b>  | <b>186</b> |

## ORODHA YA MAJEDWALI

|  |     |
|--|-----|
| Jedwali 1.1 Uanishaji wa shule za Sekondari.....   | 29  |
| Jedwali 1.2 Matokeo ya Mtihani wa Kitaifa katika shule saba za Kaunti ya Busia.....        | 36  |
| Jedwali 3.1 Mimi huzungumza kwa lugha ya Kiswahili na wenzangu nikiwa shuleni .....        | 75  |
| Jedwali 3.2 Napenda Kiswahili kizungumzwe kila siku shuleni .....                          | 77  |
| Jedwali 3.3 Kuwasiliana kwa lugha ya Kiswahili kuna manufaa katika somo la Kiswahili ..... | 78  |
| Jedwali 3.4 Mimi hutumia lugha ya Kiswahili nikiwa nyumbani au kwenye bweni .....          | 80  |
| Jedwali 3.5 Napenda somo la Kiswahili.....   | 82  |
| Jedwali 3.6 Nikitumia lugha ya Kiswahili mimi huhisi raha sana .....                       | 83  |
| Jedwali 3.7 Napenda siku za Kiswahili shuleni mwetu .....                                  | 86  |
| Jedwali 3.8 Unakubaliana na adhabu za ukiukaji wa kanuni za lugha shuleni .....            | 88  |
| Jedwali 3.9 Mabango na maandishi yanayohusu matumizi ya lugha shuleni ni ya mahufaa .....  | 91  |
| Jedwali 3.10 Mijadala inayoendeshwa kwa lugha ya Kiswahili ni muhimu. 93                   |     |
| Jedwali 3.11 Vyama vya Kiswahili vina manufaa shuleni.....                                 | 95  |
| Jedwali 3.12 Vipindi vya ziada vya somo la Kiswahili ni muhimu .....                       | 97  |
| Jedwali 3.13 Mimi hushiriki katika makongamano ya Kiswahili ya ndani mwa shule .....       | 99  |
| Jedwali 3.14 Mimi huhudhuria makongamano ya Kiswahili ya nje ya shule .....                | 101 |
| Jedwali 3.15 Mimi husoma vitabu vya hadithi na magazeti ya lugha ya Kiswahili shuleni..... | 103 |
| Jedwali 3.16 Mimi huwasiliana na walimu wenzangu kwa lugha ya Kiswahili shuleni .....      | 106 |
| Jedwali 3.17 Mimi hufundisha kwa lugha sanifu ya Kiswahili.....                            | 107 |
| Jedwali 3.18 Lugha ya Kiswahili inafaa kuwa lugha ya mawasiliano ya kila siku shuleni..... | 108 |

|   |     |
|---|-----|
| Jedwali 3.19 Siku za Kiswahili shuleni zina manufaa .....   | 110 |
| Jedwali 3.20 Mabango na maandishi yaliyo katika mazingira ya shule yana manufaa .....                   | 112 |
| Jedwali 3.21 Mimi huhudhuria siku za mijadala kwa lugha ya Kiswahili ..                                 | 114 |
| Jedwali 3.22 Vipindi vya ziada shuleni mwetu vina manufaa .....   | 116 |
| Jedwali 3.23 Mimi huhudhuria makongamano ya nje ya shule .....  | 117 |
| Jedwali 3.24 Mimi hushiriki katika makongamano ya ndani ya shule.....                                   | 119 |
| Jedwali 3.25 Kuna manufaa katika usomaji wa magazeti na vitabu vya hadithi kwa lugha ya Kiswahili ..... | 120 |
| Jedwali 3.26 Kuwepo kwa vyama vya Kiswahili shuleni vina manufaa ....                                   | 121 |
| Jedwali 3.27 Nilihusishwa katika uteuzi wa kanuni za lugha shuleni.....                                 | 123 |
| Jedwali 4.1 Matokeo ya mtihani wa Kitaifa katika somo la Kiswahili kati ya mwaka 2020-2023 .....        | 127 |

## ORODHA YA GRAFU NA CHATI

|   |    |
|---|----|
| Jedwali 1.2 Matokeo ya Mtihani wa Kitaifa katika shule saba za Kaunti ya Busia.....                       | 36 |
| Grafu 2.1 Majibu ya wanafunzi kuhusu lugha ya mawasiliano shuleni.....                                    | 42 |
| Chati 2.1 Majibu ya wakuu wa idara ya Kiswahili kuhusu lugha ya mawasiliano shuleni .....                 | 43 |
| Grafu 2.2 Majibu ya wanafunzi kuhusu Siku ya Kiswahili.....   | 45 |
| Chati 2.2 Majibu ya wakuu wa idara kuhusu siku ya Kiswahili .....   | 48 |
| Grafu 2.3 Majibu ya wanafunzi kuhusu mabango na maandishi shuleni.....                                    | 50 |
| Grafu 2.4 Majibu ya wanafunzi kuhusu mijadala kwa lugha ya Kiswahili.....                                 | 52 |
| Chati 2.3 Majibu ya wakuu wa idara ya Kiswahili kuhusu mijadala ya lugha ya Kiswahili.....                | 54 |
| Chati 2.4 Majibu ya wanafunzi kuhusu vipindi vya ziada shuleni.....                                       | 57 |
| Chati 2.5 Majibu ya wakuu wa idara ya Kiswahili kuhusu vipindi vya ziada shuleni .....                    | 58 |
| Chati 2.6 Majibu ya wanafunzi kuhusu makongamano ya ndani ya shule .....                                  | 60 |
| Chati 2.7 Majibu ya wakuu wa idara ya Kiswahili kuhusu maandalizi ya makongamano ya ndani mwa shule ..... | 62 |
| Chati 2.8 Majibu ya wanafunzi kuhusu makongamano ya nje ya shule .....                                    | 63 |
| Chati 2.9 Majibu ya wakuu wa idara ya Kiswahili kuhusu makongamano ya nje ya shule.....                   | 64 |
| Chati 2.10 Majibu ya wanafunzi kuhusu usomaji wa vitabu na magazeti shuleni .                             | 66 |
| Chati 2.11 Majibu ya wakuu wa idara ya Kiswahili kuhusu usomaji wa vitabu na magazeti shuleni .....       | 67 |
| Chati 2.12 Majibu ya wanafunzi kuhusu uwepo wa vyama vya Kiswahili shuleni .....                          | 69 |

## **ORODHA YA VIELELEZO**

|  |     |
|--|-----|
| Kielelezo 1.1 Shule ya upili ya Chakol .....   | 195 |
| Kielelezo 1.2. Shule ya upili ya wasichana ya Lwanya.....  | 196 |
| Kielelezo 1.3 Shule ya upili ya Chakol .....   | 197 |
| Kielelezo 1.4: Ratiba ya vipindi vya ziada vya Kiswahili katika shule ya Mseto<br>ya Makunda ..... | 198 |
| Kielelezo 1.5 Barua ya mwaliko katika kongamano la kitaifa .....                                   | 199 |

## ORODHA YA VIAMBATISHO

|  |     |
|--|-----|
| Kiambatisho A: Mwongozo wa mahojiano kwa walimu wakuu wa Shule za upili<br>Kaunti ya Busia .....                               | 186 |
| Kiambatisho B : Hojaji kuhusu kanuni za lugha shuleni .....  | 187 |
| Kiambatisho C : Hojaji kuhusu kanuni za lugha shuleni .....  | 188 |
| Kiambatisho D : Hojaji likati ili kupima mielekeo ya wanafunzi kuhusu kanuni<br>za lugha shuleni .....                         | 189 |
| Kiambatisho E: Mwongozo wa mjadala elekezi wa makundi kwa wanafunzi .....  | 191 |
| Kiambatisho F: Hojaji likati ili kupima mielekeo ya wakuu wa Idara ya<br>Kiswahili kuhusu kanuni za lugha shuleni .....        | 192 |
| Kiambatisho G: Mwongozo wa mahojiano kwa wakuu wa Idara ya Kiswahili<br>kuhusu mielekeo yao kwa kanuni za lugha za shule ..... | 194 |
| Kiambatisho H: Kielelezo cha picha ya mabango katika shule za upili Kaunti<br>ya Busia .....                                   | 195 |
| Kiambatisho I: Barua Ya kuomba Idhini Ya Kutafiti .....  | 200 |
| Kiambatisho J: Leseni Ya Utafiti Wa NACOSTI .....  | 201 |

## IKISIRI

Utafiti huu ulishughulikia mielekeo ya wanafunzi na walimu wa shule za upili katika Kaunti ya Busia kuhusu kanuni za lugha shuleni na namna kanuni hizi zinavyoathiri somo la Kiswahili. Utafiti huu ulichunguza na kuhakiki kanuni za lugha katika shule za upili. Aidha ulibaini mielekeo ya wanafunzi na walimu kuhusu kanuni za lugha shuleni na athari yake kwa somo la Kiswahili. Malengo matatu yalioongoza utafiti huu ni: Kueleza kanuni za lugha shuleni, kuchunguza mielekeo ya wanafunzi na walimu kuhusu kanuni za lugha shuleni na kufafanua athari za kanuni za lugha shuleni kwa somo la Kiswahili katika shule zilizo Kaunti ya Busia. Utafiti huu ulitumia nadharia mbili katika uchanganuzi wa data. Kwanza, nadharia ya Saikolojia ya jamii ya Vitendo Vilivyofikiriwa ya Ajzen na Fishbein (1980). Nadharia hii inasema kuwa, binadamu huwa na mtazamo kubalifu kuhusu jambo ambalo litamnufaisha na kuwa na mwelekeo hasi kwa jambo ambalo halina manufaa kwake. Nadharia hii ilitumika kubainisha mielekeo ya walimu na wanafunzi kuhusu kanuni za lugha za shule. Nadharia hii haingeweza kuhakiki kanuni za lugha za shule na athari yake kwa somo la Kiswahili kwa kukosa vigezo vya kuchanganua data hii. Kwa hivyo, nadharia ya pili ambayo ni ya Kijumuia na Kibinadamu ilioasisiwa na Richards na Rodgers (1995) ilitumika. Nadharia hii inasema kuwa, mazingira yenye usalama na utu kwa mwanafunzi humwathiri anapojifunza lugha ya pili. Ili kufanikisha malengo ya utafiti, wanafunzi na walimu kutoka shule za upili saba zenye viwango vya Kitaifa, Zaidi ya Kaunti na Kaunti ziliteuliwa. Walimu na wanafunzi walijaza hojaji likati na wanafunzi kushiriki katika mjadala elekezi wa makundi. Utafiti huu ulihusisha wanafunzi 560 na walimu saba wa somo la Kiswahili ambao pia ni wakuu wa idara ya Kiswahili. Mtafiti pia alifanya mahojiano na walimu wakuu kwa kila shule kuhusu kanuni za lugha zilizoteuliwa. Utafiti uliteua shule tatu za wasichana za bweni, tatu za wavulana za bweni na shule moja ya mseto ya kutwa. Utafiti huu ulifanywa nyanjani na maktabani. Vifaa tofauti vilitumiwa nyanjani, hojaji likati ilitumika ili kubainisha mielekeo ya walimu na wanafunzi kuhusu kanuni za lugha za shule. Mjadala elekezi wa makundi ulitumika kubainisha sababu ya mielekeo chanya au hasi na manufaa ya kanuni za lugha za shule kwa wanafunzi. Mbinu ya uchunzaji ilitumika kwa kutazama mabango yaliyo shuleni na kuchunguza namna mijadala kwa lugha ya Kiswahili ilivyoendesha. Utafiti wa maktabani ulifanywa kwa kusoma kazi za waandishi mbalimbali zinazohusu sera ya lugha kwa jumla, kanuni za lugha shuleni pamoja na mielekeo yao. Uchanganuzi wa data ulifanywa kwa kuainisha mada tofauti tofauti. Njia ya maelezo ilitumika kuwasilisha data kwa kiasi kikubwa. Picha, majedwali na michoro pia ilitumika. Matokeo ya utafiti yalionyesha kuwa, shule tofauti zina kanuni za lugha tofauti na utekelezaji wake pia ni tofauti. Kanuni hizi ni kama lugha ya mawasiliano katika mazingira ya shule, siku za Kiswahili, mabango na maandishi katika mazingira ya shule, matumizi ya lugha ya Kiswahili katika mijadala, shughuli za idara ya Kiswahili kama makongamano, usomaji wa vitabu na magazeti pamoja na vyama vya Kiswahili. Ilibainika kuwa, wanafunzi na walimu wana mielekeo chanya kwa kanuni za lugha za shule ambazo zinaimarisha matokeo ya mtihani katika somo la Kiswahili. Utafiti pia ulibaini kuwa, utekelezaji wa kanuni za lugha za shule unahitaji mchango na ushirikiano wa wizara ya elimu, uongozi wa shule, walimu na wanafunzi wote ili athari yake iwe chanya kwa somo la Kiswahili.

## ABSTRACT

This research sought to establish secondary school student and teacher's attitudes towards school rules on language use and their effect on Kiswahili as a subject. The study analysed different rules on language use, student and teacher's attitude towards rules on language use and its effect on Kiswahili as a subject. This research was guided by three objectives namely; to describe rules on language use found in secondary schools in Busia County, examine teachers and students attitude towards school rules on language use and explain effects of rules on language use on Kiswahili as a subject in Busia County. The study was guided by two theories: The first theory by Ajzen and Fishbein (1980) which states that, human beings tend to have positive attitude towards what is beneficial to them and a negative attitude towards what is less important. The second theory is community language learning by Richards and Rodgers (1995). It explains the impact of a secure environment, to a student learning second language. To achieve the research objectives, students and teachers were selected and identified from National, extra County and County schools. Stratified purpose sampling was used to get respondents. Teachers and students filled questionnaires through use of likert scale and focus group discussion to establish their attitude, importance and reasons for such attitudes towards rules on language at school. The study involved 560 students and seven teachers who are head of Kiswahili department from seven secondary schools. The researcher interviewed each head of the institution to establish rules on language use found in their schools. The research selected three boarding schools for girls and boys and one mixed day secondary school. The study incorporated both field and library work. This study used various types of research instruments; student and teacher attitude likert questionnaires, focus group discussion for getting the reasons for student attitude towards rules on language use and its importance. Research methods such as observation was used by observing placards found in school environment on language use and how debates were conducted by teachers and students in Kiswahili language. The research was conducted in the library by reading books from different authors on language policies, rules on language use and attitude. Data analysis was done through analysis of various sub topics based on research objectives. Data presentation to a large extent took form of discussions. Photographs, tables and diagrams were also used. The research found out that, different schools have different rules on language use and those that have similar rules differ on implementation. The rules on language use are; Mode of communication in the school setting, use of Kiswahili language during debates, Kiswahili days in schools, availability of write ups and placards on language use and departmental activities of Kiswahili such as participation in Kiswahili symposia, Kiswahili and journalism club and reading of story books and newspapers to enforce reading culture. The study also revealed that, students and teachers have positive attitude towards rules on language use especially those that have positive impact on Kiswahili as a subject. The findings too revealed that, implementation of rules on language use at school need the input and co-operation from all stakeholders such as, Ministry of education, school administration, teachers and students for them to have a positive impact on Kiswahili as a subject.

## **SURA YA KWANZA**

### **UTANGULIZI**

#### **1.0 Usuli wa Mada**

Kulingana na utafiti wa Koko (2016), kanuni za lugha shuleni ni shughuli na sheria ambazo huteuliwa na shule fulani ili kuhakikisha kuwa matumizi ya lugha yameimarishwa shuleni. Kanuni hizi huamua ni lugha ipi itatumiwa katika mawasiliano na wakati upi katika mazingira ya shule. Kanuni hizi ni kama, lugha ya mawasiliano shuleni, siku za Kiswahili, siku za mijadala, maandishi na mabango yanayoonyesha matumizi ya lugha shuleni pamoja na shughuli za idara ya Lugha. Kanuni hizi huteuliwa kutokana na sera ya lugha nchini inayotambua Kiswahili na Kiingereza kama masomo ya lazima shuleni (Republic of Kenya, 1981).

Sera ya lugha ni dhana inayorejelea mpango wa utekelezaji wa yale yanayohusu lugha ambazo huwa zimechaguliwa. Lugha hizi hutekeleza majukumu mbalimbali katika taifa au jamii. Sera ya lugha aidha ni maamuzi yanayofanywa na watawala pamoja na wanasheria kuhusu uteuzi wa lugha mbalimbali nchini Kenya (Mukhwana, 2008). Katika shule za upili, watawala ambao ni walimu wakuu huteua kanuni za lugha shuleni ili kuwaongoza wanafunzi katika kuimarisha somo la Kiswahili na Kiingereza. Masomo haya ni ya lazima na hutahiniwa kulingana na sera ya lugha nchini Kenya (Republic of Kenya, 1981).

Lugha ya Kiswahili ilitumiwa katika mawasiliano kati ya watawala Waingereza na watawaliwa waliokuwa Waafrika kabla ya uhuru nchini Kenya. Kiswahili kilionekana kama lugha ya wananchi wa kawaida wasiokuwa na jukumu muhimu katika utawala. Kiingereza nacho kilichukuliwa kama lugha ya kifahari na ya watu wenye hadhi ya juu. Hii ilisababisha Kiingereza nchini Kenya kuchukuliwa kama lugha ya kifahari na daraja ya kupata elimu (Mukhwana, 2008). Sera ya lugha nchini Kenya iliongozwa na mapendekezo ya tume zilizoteuliwa kuchunguza maswala yanayohusu elimu baada ya uhuru. Tume ambazo ziliundwa kuweka mikakati na mapendekezo ya kuimarisha kiwango cha elimu nchini pamoja na masuala ya lugha ni; Tume ya elimu Kenya iliyoongozwa na Prof. Ominde S.H. (Republic of Kenya, 1964). Tume hii ilipendekeza Kiswahili kiwe somo la kufundishia shuleni bila kutahiniwa. Tume nyingine ni ile ya Ripoti ya Kamati ya ukufunzi. Tume hii iliyoongozwa na mwenyekiti wa Baraza la Utumishi wa Umma, Bwana W.N. Wamalwa (Republic of Kenya, 1972). Tume hii ilipendekeza kozi za Kiswahili zianzishwe katika Taasisi ya usimamizi ya kutoa mafunzo kwa watumishi wa serikali. Kamati ya Kitaifa kuhusu malengo ya sera ya elimu iliyoongozwa na Bw. P.J. Gachathi (Republic of Kenya, 1976) ilipendekeza Kiswahili kuwa somo la lazima na la kutahiniwa katika shule za msingi, za upili na vyuo vikuu. Licha ya mtazamo wa tume ya Gachathi, pendekezo la kukifanya Kiswahili kuwa somo la lazima na kutahiniwa katika shule za msingi na upili halikutekelezwa hadi mwaka wa 1985, serikali ilipoanzisha mfumo mpya wa elimu wa 8-4-4. Ripoti ya tume iliyoongozwa na Dkt. C. B. Mackay (Republic of Kenya, 1981) ilipendekeza kuwa pendekezo la Tume ya Gachathi kuhusu somo la Kiswahili kuwa la lazima na la kutahiniwa litekelezwe. Tume iliyoongozwa na Koech (Republic of Kenya, 1999)

ilipendekeza kuwa lugha ya Kiswahili, Kiingereza na Hesabu yawe masomo ya lazima.

Ingawa ni tume nyingi ambazo zimeorodheshwa, ni Tume ya Mackay ya 1981 ambayo ilichangia pakubwa kuendeleza lugha ya Kiswahili. Baadhi ya mapendekezo yake yaliweza kutekelezwa hivyo kuinua hadhi ya Kiswahili kama somo. Mfumo wa elimu wa 8-4-4 ulianzishwa mwaka wa 1982 ambapo Kiswahili kilianza kuwa somo la lazima na la kutahiniwa katika mtihani wa darasa la nane (K.C.P.E- 1985) na kidato cha nne (K.C.S.E- 1989). Baada ya mfumo mzima wa elimu kubadilishwa, mageuzi haya yalipendekezwa kuwe na silabasi mpya katika masomo yote. Kwa mara ya kwanza, somo la Kiswahili lilipata silabasi kamili kwa lugha ya Kiswahili. Hata hivyo, tume hii ilipendekeza kuwa lugha ya Kiingereza ibaki kama lugha ya kufundishia. Kwa mujibu wa katiba ya Kenya Sura ya 2, ibara ya 7 (Republic of Kenya, 2010), lugha ya Kiswahili kama lugha mojawapo ya lugha za Kenya na lugha ya taifa, imeinuliwa kihadhi. Kiswahili ni lugha rasmi sambamba na lugha ya Kiingereza. Mapendekezo haya yanadhihirisha mielekeo chanya ya wadau wa sera ya lugha kwa kukitambua Kiswahili kama lugha muhimu kupitia mfumo wa elimu.

Kutokana na mabadiliko haya, somo la Kiswahili linatarajiwa kuwa na nafasi sawa kama masomo mengine ya lazima kama Kiingereza katika shule za upili. Huenda ikawa hali si hivyo. Kwa mfano, kuanzia hapo awali kabla ya mapendekezo ya tume ya Mackay (1981), kulikuwa na sheria ambazo zilichukuliwa kama kanuni za lugha shuleni. Sheria hizi zilizuia mawasiliano katika lugha ya Kiswahili. Mbaabu 1996 :153, anamnukuu Mutahi (1978) anayesema kuwa ;

“Katika baadhi ya shule za viwango vya juu, wanafunzi walitaka kuwepo kwa walimu wa Kiswahili. Ingawa Kiswahili kilifunzwa kama somo, wanafunzi walipigwa marufuku kuzungumza lugha ya Kiswahili isipokuwa tu wakati wa kipindi cha Kiswahili. Hawangezungumza lugha hii nje ya darasa. Katika shule za viwango hivi, wanafunzi walikuwa huru kuzungumza Kiingereza na Kifaransa”

Kuna baadhi ya shule za upili ambazo mojawapo ya kipengele katika kanuni za lugha shuleni, ni sheria inayokubali mawasiliano katika lugha ya Kiingereza pekee. Vilevile, kutokana na utafiti wa awali, kuna mabango yanayosisitiza matumizi ya lugha ya Kiingereza katika mawasiliano. Hali kama hii inaonyesha kuwa, hata baada ya mfumo mpya wa elimu kupitishwa, lugha za kigeni zinaenziwa kuliko lugha ya Kiswahili. Kulingana na Kiganya (1995), Kiingereza na lugha nyingine za kigeni zinaendelea kuenziwa zaidi kuliko Kiswahili na lugha za Kiafrika. Kiganya (1995), anasema kuwa, ingawa Kiswahili kinafunzwa kote nchini katika shule za msingi kuambatana na mfumo mpya wa elimu wa 8-4-4, Kiingereza ndiyo lugha rasmi ambayo imeendelea kusambazwa kupitia kwa mfumo wa elimu. Hii ni kwa sababu Kiingereza kinatumiwa kufunzia katika viwango vyote, kuanzia shule za msingi hadi chuo kikuu na ndiyo inayotumiwa kuwatahini wanafunzi isipokuwa katika somo la Kiswahili. Pia, kati ya vipindi 43 na 45 kwa wiki kwa shule za upili, Kiingereza kimetengewa vipindi sita na Kiswahili vitano. Hali ya kutokipa Kiswahili nafasi sawa na somo la Kiingereza pia ilijitokeza katika baadhi ya shule za upili katika uteuzi wa kanuni za lugha shuleni. Shule nyingi zimekipa Kiswahili siku chache za mawasiliano ikilinganishwa na Kiingereza.

Kanuni za lugha shuleni huamua lugha ya mawasiliano katika mazingira ya shule hivyo yaweza kuchangia umaarufu wa lugha au kutochangia. Baadhi ya kanuni za lugha shuleni hukiuka sera ya lugha nchini kulingana na mapendekezo ya tume ya Mackay 1981 ambapo lugha ya Kiswahili ni somo la lazima. Kanuni hizi ni zile ambazo hupinga matumizi ya lugha ya Kiswahili katika mawasiliano. Shule kama hizi huongozwa na sheria kama ‘Lugha ya mawasiliano ni Kiingereza na Kiswahili sanifu kizungumzwe tu wakati wa somo la Kiswahili’ (Mutahi, 1978). Katika uchunguzi wa Mukele (2008), baadhi ya shule zimeweka sheria zinazomzuia mwanafunzi kuwasiliana kwa lugha ya Kiswahili au ya mama. Mwanafunzi anayepatikana akitumia lugha ya Kiswahili huadhibiwa vikali na hivyo anaweza kuamua kukichukia Kiswahili kwa kufikiria kuwa ni lugha ambayo haina manufaa yoyote nchini na kwa maisha yake ya hapo baadaye. Utafiti huu kwa hivyo, ulichunguza namna sheria kama hizi zinavyoathiri mielekeo ya wanafunzi kuhusu somo la Kiswahili.

Kulingana na Richards na wengineo (1985), mielekeo ya lugha ni mitazamo ya watu kuhusu lugha fulani. Mielekeo inaweza kuwa chanya au hasi na hudhihirika wanapotumia lugha hiyo kuwasiliana. Onyango (2008) anasema kuwa, mwelekeo wa mwalimu kuhusu lugha ya pili anayoifunza, huathiri mwelekeo wa mwanafunzi kwa kupenda lugha hiyo au kuichukia. Koko (2016) anamnukuu Kembo – Sure (1916) anasema kuwa, walimu huchukuliwa kama watekelezaji wa sera za lugha shuleni. Wao wanamiliki mada za kufundisha wanafunzi. Mielekeo ya mwalimu kuhusu kanuni za lugha za shule hivyo kuwa muhimu katika utafiti huu.

Kando na shule ambazo zimepiga marufuku matumizi ya Kiswahili katika mawasiliano, kuna shule za upili ambazo kanuni za lugha shuleni zinawaruhusu kutumia lugha ya Kiswahili au ya Kiingereza katika mawasiliano yao shuleni. Kuna zile ambazo zimetenga siku fulani ambapo Kiswahili au Kiingereza kinatumika kwa mawasiliano. Hata hivyo, nyingi za shule hutenga siku nyingi za mawasiliano katika lugha ya Kiingereza, Kachipela (2014). Kanuni za lugha shuleni huwekwa ili wanafunzi waweze kufanya vyema katika mitihani ya kitaifa. Shule ambazo zinatekeleza kanuni za lugha za shule hupita somo la Kiswahili (Nyakeoga 2018). Ni kutokana na matokeo ya utafiti kama haya ambapo utafiti huu ulinua kubaini athari ya kanuni za lugha za shule kwa somo la Kiswahili kaunti ya Busia. Kanuni za lugha za shule hujumuisha shughuli kama vile mijadala, vipindi vya ziada, shughuli za idara ya lugha, mabango na maandishi ambayo hulenga kuimarisha matumizi ya lugha shuleni. Tofauti ya kanuni za lugha shuleni kutoka shule moja hadi nyingine ilitokana na sababu moja au nyingine na hivyo basi, athari yake kwa somo la Kiswahili pia kuwa tofauti.

### **1.1 Suala la utafiti**

Kulingana na matokeo ya utafiti wa wataalamu mbalimbali, wakuu wa shule pamoja na walimu wa lugha wamelaumiwa kwa kuteua kanuni za lugha za shule ambazo utekelezaji wake unaathiri somo la Kiswahili. Somo la Kiswahili ni kati ya masomo ya lazima katika shule za upili. Shule za upili hufuata silabasi moja iliyoundwa na Taasisi ya ukuzaji mitaala Nchini Kenya. Matarajio ya mfumo huu ni kuwa, wanafunzi wote wa shule za upili katika nchi nzima ya Kenya watakuwa na mielekeo chanya kuhusu Kiswahili. Katika shule za upili, kuna kanuni za lugha za shule ambazo huteuliwa. Baadhi ya kanuni hizi huathiri mielekeo ya walimu na wanafunzi

kuhusu somo la Kiswahili. Kwa hivyo, mielekeo ya walimu na wanafunzi kuhusu kanuni za lugha za shule ni muhimu katika utafiti huu. Aidha, walimu ni wadau muhimu katika utekelezaji wa kanuni za lugha shuleni na mielekeo yao kuhusu kanuni za lugha shuleni ni muhimu kufanyiwa utafiti.

Utafiti wa awali ulibainisha kuwa, Shule za upili katika kaunti ya Busia zina kanuni za lugha ambazo ni tofauti. Kanuni hizi ni sheria ambazo huonyesha ni lugha ipi itumiwe katika mawasiliano na siku gani. Pia, huonyesha adhabu ambayo mwanafunzi hupata anapoenda kinyume na sheria hizi. Sheria hizi huteuliwa ili kuimarisha lugha ya Kiswahili na Kiingereza. Kutokana na sababu za shule tofauti kuwa na kanuni ya lugha tofauti, utafiti huu ulilenga kubainisha na kueleza aina tofauti za kanuni za lugha shuleni katika kaunti ya Busia. Kutokana na sababu ya Kanuni za lugha shuleni kuteuliwa ili kuimarisha somo la Kiswahili, utafiti huu ulilenga kufafanua athari ya kanuni za lugha shuleni kwa somo la Kiswahili katika Kaunti ya Busia.

## **1.2 Malengo ya Utafiti**

Malengo yafuatayo yaliongoza utafiti huu;

- i.** Kuchunguza kanuni za lugha katika shule za upili Kaunti ya Busia.
- ii.** Kuchunguza mielekeo ya wanafunzi na walimu kuhusu kanuni za lugha katika shule za upili Kaunti ya Busia.
- iii.** Kufafanua athari ya kanuni za lugha shuleni kwa somo la Kiswahili katika Shule za upili Kaunti ya Busia.

### **1.3 Maswali ya Utafiti**

Maswali yafuatayo yaliongoza utafiti;

- i. Ni kanuni zipi za lugha zinazopatikana katika shule za upili Kaunti ya Busia?
- ii. Wanafunzi na walimu wana mielekeo ipi kuhusu kanuni za lugha katika shule za upili Kaunti ya Busia?
- iii. Je, kanuni za lugha za shule zina athari ipi kwa somo la Kiswahili katika shule za upili Kaunti ya Busia?

### **1.4 Sababu za Kuchagua mada ya Utafiti**

Kiswahili ni somo la lazima na la kutahiniwa kufuatia mapendekezo ya Tume ya 1981 almaarufu kama Tume ya Mackay. Katika shule za upili, wakuza mitaala bado wamekipa Kiingereza vipindi sita ilhali Kiswahili vipindi vitano. Hali ya kutokipa Kiswahili nafasi sawa na somo la Kiingereza pia inajitokeza katika uteuzi wa kanuni za lugha shuleni. Hivyo utafiti huu ulitoa mapendekezo kwa wakuza mitaala, wateuzi wa sera ya lugha nchini na wadau wanaoshiriki katika uteuzi wa kanuni za lugha katika shule za upili kubuni mbinu mwafaka ya kuimarisha somo la Kiswahili kupitia matokeo ya utafiti.

Shule za upili kama asasi ya kielimu ni mojawapo ya asasi ambazo hukuza na kuendeleza matumizi ya lugha nchini. Hii ni kwa sababu Kiswahili na Kiingereza ni kati ya masomo ya lazima. Walimu na wanafunzi wa shule za upili ni wadau ambao ni watekelezaji wa kimsingi wa kanuni za lugha shuleni. Kwa sababu hii, ilikuwa muhimu kufanya utafiti kubaini mielekeo ya wanafunzi na walimu wa shule za upili kuhusiana na kanuni za lugha shuleni. Hii ilisaidia kupata matokeo ambayo

yanaweza kutumiwa na walimu wakuu kama mwongozo wa kuunda kanuni za lugha shuleni. Munialo (2010) alipendekeza utafiti zaidi kufanywa kuhusu mielekeo ya Wakenya kutoka jamii mbalimbali kuhusiana na lugha ya Kiswahili ili kupata njia mwafaka ya kuiendeleza lugha ya Kiswahili. Aidha, Nyakeoga (2018) ambaye utafiti wake unakaribiana na huu, alipendekeza utafiti wa aina hii ufanywe katika maeneo mengine mbali na mji wa Wajir. Matokeo ya utafiti huu yaliongeza maandishi yanayohusu mielekeo ya Wakenya hasa wanafunzi na walimu kuhusu lugha ya Kiswahili na athari ya mielekeo yao kwa somo la Kiswahili.

### **1.5 Upeo na Mipaka ya Utafiti**

Utafiti huu ulilenga kuchunguza kanuni za lugha katika shule za upili, Kaunti ya Busia. Kulingana na Wizara ya elimu 2018, Kaunti ya Busia ina shule 153. Mtafiti aliteua shule saba za bweni na kutwa kati ya shule 153. Shule za viwango vya Kitaifa, Zaidi ya Kaunti na ya kaunti ziliteuliwa kutokana na utafiti wa awali mnamo Julai 2016. Wanafunzi katika shule za bweni waliteuliwa kwa kuwa hawana mahusiano ya karibu na wanajamii, hivyo mara nyingi hutii sheria zinazoambatana na kanuni za lugha shuleni ambayo husisitiza mawasiliano katika lugha ya Kiswahili na Kiingereza. Wanafunzi wa shule za kutwa walichaguliwa kwa sababu ya uhusiano wao na wanajamii wanapoenda shuleni asubuhi na wanaporudi nyumbani jioni.

Hata hivyo kuna nadharia tofauti zinazoweza kushughulikia mada hii, nadharia mbili ziliteuliwa ili kuchanganua malengo ya utafiti. Nadharia ya Vitendo vilivyofikiriwa ilibainisha mielekeo ya walimu na wanafunzi kuhusu kanuni za lugha za shule. Nadharia ya pili ya kijumuia na kibinadamu ikabainisha kanuni za lugha na

kuchunguza athari yake kwa somo la Kiswahili. Japo kuna vipengele vingi vinavyoathiri lugha ya Kiswahili shuleni, utafiti huu ulijibana katika kipengele cha kanuni za lugha za shule zinavyoathiri somo la Kiswahili.

Utafiti huu ulilenga wanafunzi na walimu. Wanafunzi walioteuliwa ni wa kidato cha pili na cha tatu kwa sababu wao si wageni katika mazingira ya shule na hawajitayarishi kufanya mtihani wa Kitaifa. Walimu wakuu walihusishwa katika utafiti huu kwa kuwa wao huhusika katika uteuzi wa kanuni za lugha za shule. Wakuu wa idara ya Kiswahili walichaguliwa kwa sababu wao ni wadau wa kimsingi katika mchakato wa utekelezaji wa kanuni za lugha shuleni. Walimu hawa husimamia shughuli za idara ambazo ni kati ya kanuni za lugha za shule. Kwa hivyo, yale waliyoyasema kuhusu kanuni za lugha za shule na mielekeo yao kuhusu kanuni hizi yalikuwa muhimu katika kubainisha mielekeo ya walimu.

### **1.6 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada**

Tafiti kuhusu mielekeo ya watu kuhusu lugha ya Kiswahili na sera ya lugha kwa jumla zimefanywa na watafiti mbalimbali. Vilevile tafiti nyingi zimerejelea vipengele tofauti ambavyo huathiri lugha ya Kiswahili. Utafiti huu ulichunguza namna mielekeo ya walimu na wanafunzi katika shule za upili kuhusu kanuni za lugha shuleni ilivyoathiri somo la Kiswahili. Sehemu hii imegawanywa katika makundi mawili: Tafiti bayana kuhusu mielekeo ya watu katika Kiswahili na tafiti kuhusu vipengele vinavyoathiri lugha ya Kiswahili.

### **1.6.1 Tafiti Bayana Kuhusu Mielekeo ya Watu Tofauti Kuhusu Lugha ya Kiswahili**

Utafiti wa Agheyis na Fishman (1970) ulifafanua mielekeo kuhusu lugha kwa kuzingatia mtazamo wa kiakili na ule wa kitabia. Mbinu za utafiti zilizotumiwa katika utafiti huu ni kama zifuatazo: Mahojiano, hojaji, mlinganuo fiche, na uchunguzi kutokana na kuangalia vitendo vya wanaotumia lugha. Wanaeleza kuwa hojaji ni maarufu sana katika udadisi wa mielekeo. Utafiti wa Agheyis na Fishman ni muhimu kwa sababu utafiti huu ulitumia hojaji kama njia mojawapo ya kubainisha mielekeo ya wanafunzi na walimu kuhusu kanuni za lugha za shule za upili kaunti ya Busia.

Akishughulikia mielekeo ya wasomi kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili nchini Kenya, Ogolla (1990), alizingatia matumizi ya lugha ya Kiswahili katika mazingira rasmi na yasiyo rasmi. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya vitendo vilivyofikiriwa ya Ajzen na Fishbein (1980). Mbinu za utafiti zilizotumika katika utafiti huu ni hojaji na mahojiano fiche. Utafiti huu uligundua kuwa, katika mazingira ya elimu ya msomi, lugha ya Kiingereza ndiyo lugha inayosisitizwa mno. Katika mazingira ya nyumbani lugha za kiasili husisitizwa sana. Uchunguzi wake ulidhihirisha kwamba lugha ya Kiswahili hutumiwa kwa nadra katika maisha ya msomi ikilinganishwa na lugha nyinginezo kama Kiingereza. Anasema kuwa mojawapo ya taasisi muhimu katika uchipukaji wa mielekeo kuhusu lugha ni ile ya elimu. Hivyo basi, watu ambao wamepitia taasisi hii watakuwa na mielekeo fulani kuhusu mambo yanayozingatiwa katika elimu. Matokeo haya yalikuwa muhimu katika utafiti huu kwa sababu watafitiwa ambao ni wanafunzi, walimu wakuu na walimu wa somo la Kiswahili ni wadau katika taasisi ya elimu ya shule ya upili.

Ingawa tafiti hizi zinafanana kwa njia za utafiti pamoja na nadharia, tofauti ni kuwa, utafiti wa Ogolla (1990) ulilenga mielekeo ya wasomi kuhusu lugha ya Kiswahili kabla ya Kiswahili kuwa lugha rasmi lakini huu ulilenga mielekeo ya wanafunzi na walimu wa somo la Kiswahili baada ya Kiswahili kuteuliwa kama lugha rasmi nchini Kenya. Tofauti nyingine ni kuwa, utafiti wa Ogolla ulichunguza mielekeo ya wakenya ilhali huu ulichunguza mielekeo ya walimu na wanafunzi katika Kaunti ya Busia.

Katika utafiti wake, (Okwany, 1993) alifanya utafiti kupeleleza mielekeo ya wanafunzi wa shule za upili kuhusu Kiswahili kama somo la lazima. Utafiti wake ulilenga kutoa taarifa ambazo zitasaidia kutathmini mtaala wa somo la Kiswahili. Okwany alichagua sampuli ya wanafunzi 483 kutoka aina tofauti za kabila na jinsia. Alitumia mbinu za hojaji na mjadala elekezi ya vikundi katika kukusanya data ya utafiti wake. Matokeo ya utafiti yalionyesha kuwa, ijapokuwa wanafunzi hawa walitofautiana kikabila na kijinsia, walikuwa na mwelekeo chanya wa kijumla kuhusu Kiswahili. Utafiti huo pia ulionyesha kuwa mwelekeo huo wa wanafunzi kuhusu Kiswahili ulisababishwa na mambo ambayo yalikuwa ndani na nje ya darasa. Ijapokuwa wanafunzi wote walionyesha mielekeo chanya kuhusu Kiswahili, wale ambao wana asili ya makabila ya Kibantu, walionyesha mielekeo chanya zaidi kushinda wale wenye asili za makundi mengine ya kikabila. Utafiti huo ulithibitisha kuwa Kiswahili kilipofanywa somo la lazima, motisha ya kukisoma iliongezeka na pia hadhi yake ikainuka. Tofauti ya utafiti wa Okwany na huu ni kuwa, miaka zaidi ya ishirini imepita tangu afanye utafiti wake. Mambo mengi yamebadilika katika mtaala wa Kiswahili. Wakati huo, somo la Kiswahili lilihusu lugha, insha, fasihi, riwaya, tamthilia na ushairi. Hivi sasa, mtaala umepanuliwa na kuongezewa vitengo

vingine kama isimujamii, fasihi simulizi na hadithi fupi. Vilevile, wakati wa Okwany (1993) Kiswahili kilikuwa lugha ya taifa pekee ilhali sasa Kiswahili ni lugha ya taifa na rasmi.

Mielekeo ya wasikilizaji kuhusu taarifa ya habari katika mtaa wa Komarock jijini Nairobi imetafitiwa na Namulanda (2002). Nadharia iliyotumiwa ilikuwa ya vitendo vilivyofikiriwa ya Ajzen na Fishbein (1980). Mbinu za utafiti zilizotumika katika utafiti ni hojaji na mahojiano yasiyo rasmi. Alibaini kuwa, ikiwa mpokezi haipendi lugha inayotumiwa hawezi kutilia maanani ujumbe unaotolewa na mpashaji. Kwa sababu hii, sera ya lugha ya vyombo vya habari kwa kiasi fulani hutegemea mielekeo ya wapokezi wa habari kuhusu lugha zinazotumiwa. Matokeo yalionyesha kuwa kundi kubwa la watafitiwa walio na mwelekeo hasi kuhusu taarifa ya habari kwa Kiswahili linapatikana miongoni mwa watafitiwa walio na elimu ya kiwango cha kidato cha nne. Watafitiwa walio na elimu ya kiwango cha chuo kikuu na darasa la nane ndio wanaonyesha mielekeo kubalifu zaidi. Matokeo haya ni muhimu katika utafiti huu kwa kuwa yatachangia katika kuchunguza mielekeo ya wanafunzi wa shule ya upili ambao ni kati ya watafitiwa katika utafiti wa Namulanda. Utafiti wa Namulanda ni tofauti na huu kwa kuwa ulilenga mielekeo ya wasikilizaji wa taarifa ya habari ya Kiswahili. Utafiti huu ulishughulikia mielekeo ya wanafunzi na walimu wa somo la Kiswahili kuhusu kanuni za lugha shuleni na athari yake katika somo la Kiswahili.

Babusa (2010), alifanya utafiti kuhusu uchanganuzi linganuzi wa mielekeo na umilisi wa lugha ya Kiswahili wa wanafunzi katika mikoa ya Pwani na Nairobi nchini Kenya. Nadharia mbili zilielekeza utafiti huu. Nadharia ya kwanza ni ya utabia ambayo iliasisiwa na Skinner na ya pili ni ya motisha ya kujifunza lugha ya

pili ambayo iliasisiwa na Gardner. Mbinu ya tapakishi – makusudi ilitumika kupata wasailiwa. Utafiti huu ulitumia hojaji Likati ya kutathmini mielekeo ya wanafunzi kuhusu Kiswahili, mtihani wa Kiswahili wa kutathmini viwango vya umilisi wa lugha ya Kiswahili vya wanafunzi na mjadala elekezi wa makundi wa kutathmini mielekeo na sababu za mielekeo ilionyeshwa na wanafunzi. Uchunguzi wake ulibaini kuwa, wanafunzi wa mkoa wa Pwani walikuwa na mielekeo chanya zaidi kuhusu Kiswahili kushinda wanafunzi wa mkoa wa Nairobi. Aidha, wasichana walikuwa na mielekeo chanya kuhusu Kiswahili kuliko wavulana. Kati ya wanafunzi waliokuwa na mielekeo chanya kuhusu Kiswahili, wengine walikuwa na viwango vya chini vya umilisi wa lugha ilihali baadhi ya wale waliokuwa na mielekeo hasi kuhusu Kiswahili, walikuwa na viwango vya juu vya umilisi. Babusa (2010), alishughulikia wanafunzi wa shule za upili katika mikoa ya Pwani na Nairobi ilihali utafiti huu ulishughulikia wanafunzi wa shule za upili katika Kaunti ya Busia. Tofauti nyingine ni kuwa Babusa alichunguza mielekeo na umilisi wa lugha ya Kiswahili ilihali huu ulichunguza mielekeo ya walimu na wanafunzi kuhusu kanuni za lugha katika shule za upili.

Mada kuhusu mielekeo ya wanafunzi kwa lugha ya Kiswahili katika wilaya ya Rachuonyo na athari zake katika matokeo ya mtihani imetafitiwa na Munialo (2010). Utafiti ulinua kubaini mielekeo ya wanafunzi katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili na jinsi walimu wanavyobuni mikakati, ratiba na vitabu ili kuleta mabadiliko katika mielekeo ya wanafunzi katika ujifunzaji wa lugha ya pili. Aliteua shule thelathini katika tarafa tano za wilaya. Wanafunzi sita waliteuliwa kutoka kila shule kwa njia ya bahati nasibu. Hojaji ilipewa wanafunzi kujaza, kisha walimu walifanyiwa mahojiano. Uchunguzi wa majaribio ulifanywa katika shule nne jirani

kutoka wilaya ya Kisumu na Nyando. Majibu yaliingizwa katika jedwali la thibitisho. Matokeo ya utafiti huu yalionyesha kuwa, wanafunzi wa eneo la Rachuonyo huwa na mielekeo hasi katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili jambo ambalo liliathiri matokeo yao ya Kiswahili. Matokeo haya pia yalibainisha kuwa mielekeo hasi inaweza kubadilishwa kwa kuwa na vyama vya Kiswahili na mikakati mingine kama majadiliano, makongamano, matembezi ya nje, mashindano na kuanzishwa kwa siku za Kiswahili. Utafiti huu ni muhimu kwa kuwa unarejelea kanuni za lugha shuleni ambazo huchangia ubadilishaji wa mielekeo ya wanafunzi kuhusiana na somo la Kiswahili.

Mirianga (2014), alichunguza mielekeo ya walimu wa shule za msingi kuhusu suala la lugha kama linavyoelezwa katika katiba ya Kenya. Utafiti ulifanywa katika shule za msingi wilaya ya Igembe Kaskazini. Utafiti uliongozwa na nadharia mbili ya kijamii nafsia ya Lambert (1963) na ya kijamii ya Fishman (1969). Utafiti ulifanywa kwa njia ya maswali ya hojaji, mahojiano na utazamaji wa matendo ya wahojiwa kuhusu matumizi ya lugha wakati wa utafiti. Matokeo yalionyesha kuwa, asilimia kubwa ya watafiti walionyesha mielekeo chanya kuhusu matumizi ya Kiswahili kama lugha rasmi katika mazingira rasmi nchini Kenya. Mielekeo chanya hudhihirika katika shule za msingi nchini Kenya. Walimu waliohojiwa pia walikuwa na mielekeo chanya kuhusu dhima ya Kiswahili kama lugha ya taifa na rasmi nchini Kenya. Matokeo ya utafiti pia yalionyesha kuwa lugha ya Kiingereza inapendelewa sana kama lugha rasmi kuliko Kiswahili. Matokeo haya yalikuwa muhimu katika utafiti huu kwa sababu yalichangia katika kubainisha mielekeo ya walimu na wanafunzi kuhusiana na Kiswahili kama somo na lugha rasmi. Tofauti ya utafiti wa Mirianga na huu ni kuwa, alichunguza mielekeo ya walimu katika shule za msingi

wilaya ya Igembe Kaskazini ilhali huu ulichunguza mielekeo ya walimu, wanafunzi katika shule za upili katika kaunti ya Busia.

Mielekeo na changamoto za Maafisa wa kaunti katika utekelezaji wa katiba kuhusu sera ya lugha ilishughulikiwa na Ndung'u (2014). Utafiti huu ulifanywa katika kaunti ya Nakuru. Nadharia alizotumia katika utafiti wake ni nadharia ya vitendo vilivyofikiriwa na ya utekelezaji. Utafiti ulitumia mbinu ya hojaji na mahojiano rasmi na yasiyo rasmi ili kupata mielekeo ya wasomi na wanafunzi. Hojaji iliyotumiwa ilikuwa ya maswali funge na pia maswali wazi. Katika utafiti wake aligundua kuwa, katika sekta ya elimu, wakuu wa shule wameweka sheria ambazo zinabana matumizi ya lugha ya Kiswahili, licha ya kuwa Kiswahili ni somo la lazima na kutahiniwa. Baadhi ya sheria hizo ni zile zinazozuia wanafunzi kuongea lugha ya Kiswahili wakiwa shuleni. Utafiti wa Ndung'u (2014) ni muhimu katika utafiti huu kwa sababu, sheria hizi ni kati ya vipengele vya kanuni za lugha shuleni zinayoshughulikiwa katika utafiti huu. Tofauti ya utafiti wa Ndung'u na utafiti huu ni kuwa, wake umelenga sera ya lugha kwa jumla ilhali huu ulilenga kanuni za lugha shuleni hasa katika shule za upili Kaunti ya Busia.

Okeyo, Kimemia na Ndethiu (2023) wamefanya utafiti kuhusu uchunguzi wa mielekeo ya walimu na wanafunzi kuhusu mbinu na nyenzo za kufundishia Kiswahili katika shule za upili za umma, kaunti ya Kisumu na Kakamega nchini Kenya. Utafiti huu ulilenga walimu na wakuu wa idara ambao walikuwa kumi na wawili katika kila Kaunti. Wanafunzi walioteuliwa walikuwa 960. Data zilikusanywa kupitia hojaji za wanafunzi na walimu, mwongozo wa usaili kwa wakuu wa idara ya Kiswahili pamoja na uchunguzi wa darasani. Data zilichanganuliwa kwa kutumia Toleo la takwimu 13 kuonyesha idadi katika alama

za asilimia na uradidi. Matokeo ya utafiti wake yalibaini kuwa, pana uhusiano kati ya mielekeo, utendakazi na matokeo ya wanafunzi somoni. Mielekeo chanya iliathiri utendakazi na matokeo kwa namna chanya bali mielekeo hasi iliathiri haya yote kwa namna hasi. Utafiti wa Okeyo na wenzake ni muhimu kwa kuwa, kama huu, umeshughulikia mielekeo ya walimu na wanafunzi wanapofunza na kujifunza lugha ya Kiswahili. Aidha matokeo ya utafiti wake yametupa habari kuhusu mbinu ambazo mwalimu anaweza kutumia ili kufanya mielekeo ya wanafunzi kuwa chanya wanapojifunza lugha ya Kiswahili kama njia moja ya kuimarisha matokeo ya mitihani. Tofauti ya tafiti hizi ni kuwa, ule wa Okeyo na wengineo unashughulikia mielekeo ya walimu na wanafunzi kuhusu mbinu na nyenzo za kufundishia Kiswahili ilhali huu unashughulikia mielekeo ya walimu na wanafunzi kuhusu kanuni za lugha za shule. Maeneo ya utafiti pia ni tofauti.

Tafiti nyingi katika sehemu hii zimeshughulikia namna mielekeo ya watu tofauti kama vile wasomi, wanafunzi, wasikilizaji habari, walimu na maafisa wa elimu huathiri lugha ya Kiswahili. Pengo ambalo utafiti huu ulijaza ni kuchunguza namna mielekeo ya walimu na wanafunzi wa shule ya upili kuhusu kanuni za lugha shuleni zinavyoathiri somo la Kiswahili shule za upili kaunti ya Busia.

### **1.6.2 Tafiti kuhusu Vipengele Vinavyoathiri Lugha ya Kiswahili**

Watafiti wengi kama vile Onyango (1997), Odeo (2007), Kachipela (2014), Koko (2016), Nyakeoga (2018) na Nyongesa na wenzake (2022) wamechunguza namna vipengele mbalimbali kama uziada wa kisarufi, utekelezaji wa silabasi mpya, sheng', umilisi, utendaji wa wanafunzi na utekelezaji wa kanuni za lugha za shule huathiri lugha ya Kiswahili.

Onyango (1997), alichunguza uziada wa kisarufi katika Kiswahili cha wanafunzi wanaozungumza Kinyala. Lengo lake kuu katika utafiti huu lilikuwa ni kuchunguza iwapo tofauti za kisarufi zilizopo kati ya Kinyala na Kiswahili ni kikwazo kwa wanafunzi wa lugha ya Kinyala wanapojifunza Kiswahili sanifu. Matokeo ya uchunguzi wake yalionyesha kuwa, makosa mengi ya wanafunzi husababishwa na athari za lugha ya kwanza, hata hivyo kuna makosa mengine ambayo hayahusiani na athari za lugha ya kwanza. Utafiti huu ni muhimu kwa sababu lahaja ya Kinyala iliyoshughulikiwa ni kati ya lahaja ya Kiluhya katika kaunti ya Busia ambapo mtafiti alifanyia utafiti. Tofauti na utafiti huu ni kuwa, utafiti wake ulishughulikia uziada wa kisarufi katika Kiswahili cha wanafunzi wa Kinyala ilhali huu unatafiti kuhusu mielekeo ya wanafunzi wa shule ya upili kuhusu kanuni za lugha shuleni na athari yake katika somo la Kiswahili.

Utafiti wa Odeo (2007) ulichunguza utekelezaji wa silabasi mpya ya somo la Kiswahili katika shule za upili. Njia alizotumia katika ukusanyaji wa data zilikuwa mahojiano, utazamaji na utafiti wa maktabani. Matokeo ya utafiti yalionyesha kuwa hivi sasa ratiba ya shule za sekondari inatenga vipindi rasmi vitano vya Kiswahili kwa kidato cha 1 na 2 na vipindi sita kwa kidato 3 na 4. Pia utafiti ulibainisha kuwa silabasi iliyopo haikuhusisha walimu wa somo la Kiswahili hivyo basi akapendekeza kuwa, silabasi inapofanyiwa mageuzi, wadau wote washirikishwe kikamilifu na majaribio yafanywe kabla haijatumwa shuleni. Tofauti kati ya utafiti wa Odeo na utafiti huu ni kuwa, ulishughulikia utekelezaji wa silabasi mpya ya somo la Kiswahili katika shule za upili kinyume na huu ambao ulitafiti kuhusu mielekeo ya wanafunzi wa shule ya upili kuhusu kanuni za lugha shuleni na athari yake katika somo la Kiswahili.

Mada kuhusu athari ya Sheng' katika matokeo ya mtihani wa Kiswahili katika shule za msingi mtaa wa Kangemi ilitafitiwa na Kachipela (2014). Nadharia iliyotumika katika utafiti ni ya kitambulishi jamii ilioasisiwa na Henri Taifel na John Turner (1979). Mbinu za utafiti zilikuwa kuwahoji na kuwapa wadau hojaji ili kubainisha athari za Sheng kwa matokeo ya Kiswahili katika shule za msingi nchini Kenya. Ilibainika kuwa, sababu ambazo huwafanya wanafunzi kutofanya vizuri katika mtihani hasa wa Kiswahili ni athari ya lugha ya misamiati ya sheng katika uandishi wao wa insha. Wanafunzi huathirika kimsamiati kwa sababu ya kuwasiliana kwa kutumia Sheng'. Pia, ilibainika kuwa, walimu hupendelea sana wanafunzi kuzungumza na kuwasiliana kwa lugha ya Kiingereza kuliko Kiswahili. Hali hii hudhihirika kupitia kanuni za lugha shuleni ambapo lugha ya mawasiliano katika shule hizi huwa lugha ya Kiingereza kwa aghalabu siku nne au tano za wiki. Mwanafunzi anayekwenda kinyume na kanuni za lugha za shule huadhibiwa. Hali hii huwafanya wanafunzi wa shule kuuliza au kujibu maswali katika lugha ya Kiingereza hata kama kipindi husika ni cha somo la Kiswahili hivyo basi kuathirika kimsamiati. Utafiti wa Kachipela (2014) ulichangia kubainisha athari ya kanuni za lugha shuleni katika somo la Kiswahili. Tofauti ya utafiti wa Kachipela (keshatajwa) na huu ni kuwa wake ulichunguza athari ya sheng kwa somo la Kiswahili katika shule za msingi. Utafiti huu ulichunguza athari ya kanuni za lugha shuleni kwa somo la Kiswahili katika shule za upili.

Koko (2016), naye alichunguza umilisi na utendaji wa wanafunzi wa shule za upili katika eneo la Nyanza. Lengo lake lilikuwa kutathmini changamoto na uimarikaji wa Kiswahili katika baadhi ya shule. Nadharia ya Sarufi Zalishi (Chomsky, 1965) na ya Kijumuia na Kibinadamu (Richards na Rodgers, 2001) zilitumiwa katika utafiti wake. Walimu na wasimamizi wa somo la Kiswahili walijaza hojaji. Mbinu ya uteuzi kimaksudi ilitumiwa kuchagua shule nne. Data zilikusanywa kwa kutumia hojaji na mahojiano. Matokeo ya utafiti wake yalionyesha kuwa, kanuni za lugha shuleni huchangia katika kuimarisha somo la Kiswahili ingawa kuna changamoto nyingine zinazoathiri lugha ya Kiswahili. Utafiti wa Koko ulibaini kuwa, kuna sheria inayohusu matumizi ya lugha. Lugha zote za kiasili zimepigwa marufuku katika shule nne zilizoteuliwa ili kuboresha matokeo ya Kiswahili. Shuleni mna mkusanyiko wa wanafunzi kutoka makabila mbalimbali. Hivyo, Kiswahili hutumiwa ili kuondoa ubaguzi. Lugha rasmi zinazokubaliwa kutumiwa na wanafunzi ni Kiingereza, Kiswahili na Kifaransa. Wanafunzi aidha walihimizwa kuzungumza kwa Kiswahili sanifu bila kuchanganya ndimi wala kutumia sheng'. Utafiti wa Koko pia ulionyesha kuwa, katika shule ya wasichana ya Kisumu kanuni ya shule ni kuwa wanafunzi wote watumie Kiingereza kama lugha rasmi lakini Kiswahili huzungumzwa tu wakati wa somo la Kiswahili. Koko (2016), alishughulikia eneo la Nyanza, ilhali utafiti huu ulishughulikia Kaunti ya Busia. Tofauti nyingine ni kuwa Koko alichunguza kanuni za lugha shuleni kama kipengele kinachoathiri lugha ya Kiswahili ilihali huu ulichunguza mielekeo ya walimu na wanafunzi wa shule ya upili kuhusu kanuni za lugha shuleni inavyoathiri somo la Kiswahili.

Suala la wajibu wa kanuni za lugha za shule katika kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili katika kaunti ndogo ya Wajir Mashariki limetafitiwa na Nyakeoga (2018). Lengo lake lilikuwa kubainisha kanuni za lugha za shule katika eneo la Wajir, mchango wa walimu na wanafunzi katika utekelezaji wake pamoja na changamoto katika utekelezaji wa kanuni za lugha shuleni. Nadharia ya Mkusanyo ya upangaji lugha ya Liddicoat (2005) na nadharia ya hadhi ya lugha katika elimu na mpangilio wake ya Van Ells (2005) zilitumika katika utafiti wake. Katika uchunguzi wake, aliteua shule nane, wanafunzi mia mbili na walimu wa somo la Kiswahili thelathini. Data ilikusanywa kupitia uchunzaji, hojaji na mahojiano. Matokeo ya utafiti wake yalionyesha kuwa, shule nyingi katika kaunti ndogo ya Wajir Mashariki zina kanuni za lugha za shule ingawa kuna changamoto katika utekelezaji wake. Walimu ni chombo muhimu katika utekelezaji wa kanuni za lugha. Aidha aligundua kuwa, katika shule ambazo kanuni za lugha za shule zinazingatiwa, matokeo ya mtihani katika somo la Kiswahili ni mazuri. Utafiti wa Nyakeoga ni tofauti na huu kwa sababu, alishughulikia eneo la Wajir ilhali huu unashughulikia eneo la Busia sehemu iliyo na wazungumzaji wengi wa lugha za Kibantu. Nadharia pia zinatofautiana katika tafiti hizi. Katika utafiti wake, pia alipendekeza kuwa, utafiti kama huu unafaa kufanywa katika maeneo tofauti ya nchi ya Kenya.

Mada kuhusu motisha, muundo na utekelezaji wa kanuni za lugha ilishughulikiwa na Nyongesa, Omulando na Wanyonyi (2022) walipochunguza matumizi ya Lugha ya Kiswahili katika mazingira ya shule. Lengo la utafiti huu lilikuwa kukadiria namna motisha, muundo na utekelezaji wa kanuni za lugha za shule huathiri matumizi ya lugha ya Kiswahili katika mazingira ya shule. Utafiti huu ulifanywa

katika shule za upili za umma 30 katika Kaunti ya Bungoma. Idadi ya wanafunzi walioteuliwa walikuwa 360 wa kidato cha tatu, walimu 90 na wakuu wa shule 30. Data ilikusanywa kupitia hojaji na uchanganuzi wa nyaraka. Uchanganuzi wa data ulifanywa kupitia maelezo, matumizi ya asilimia na masimulizi. Matokeo ya utafiti yalibaini kuwa, shule zilizoteuliwa zina kanuni za lugha za shule ingawa zilitofautiana katika utekelezaji wake. Ilibainika kuwa, motisha na adhabu ziliathiri utekelezaji wa kanuni za lugha za shule. Kwa sababu hii, utafiti huu ulipendekeza kuwa, kila mwalimu licha ya somo analofundisha, anafaa kuhusika katika utekelezaji wa kanuni za lugha za shule. Ingawa utafiti wa Nyongesa na wenzake (2022) unafanana na utafiti huu katika kipengele cha kanuni za lugha za shule, tofauti inayobainika ni kuwa, utafiti huu ulishughulikia mielekeo ya walimu na wanafunzi kuhusu kanuni za lugha za shule na athari yake kwa somo la Kiswahili ilihali wa Nyongesa na wenzake ulishughulikia motisha kama kipengele muhimu katika utekelezaji wa kanuni za lugha za shule. Maeneo ya utafiti na nadharia zilizotumika katika utafiti pia ni tofauti. Utafiti wa Nyongesa na wenzake ulikuwa muhimu kwa sababu ulibainisha umuhimu wa motisha katika kuimarisha mielekeo ya wanafunzi kuhusu kanuni za lugha za shule.

Watafiti hawa wamechunguza namna lugha ya pili, utekelezaji wa silabasi, Sheng' pamoja kanuni za lugha shuleni zinavyoathiri somo la Kiswahili. Tafiti hizi zilikuwa muhimu katika utafiti huu kwa kuwa zilichangia kujibu lengo la kwanza na tatu la utafiti huu. Utafiti huu ni tofauti kwa kuwa ulishughulikia kwa upana athari ya kanuni za lugha shuleni tofauti kwa somo la Kiswahili kaunti ya Busia hivyo kujaza pengo lililopo. Sehemu inayofuata ilirejelea misingi ya nadharia.

## **1.7 Misingi ya Nadharia**

Utafiti huu ulitumia nadharia mbili ambazo ni nadharia ya vitendo vilivyofikiriwa na ile ya kijumuia na kibinadamu. Nadharia ya vitendo vilivyofikiriwa ilitumika ili kubainisha mielekeo ya walimu na wanafunzi kuhusu kanuni za lugha za shule na sababu ya mielekeo hiyo. Kwa kuwa, nadharia ya vitendo vilivyofikiriwa haikuwa na vigezo vya kubainisha kanuni za lugha za shule na athari yake kwa somo la Kiswahili, nadharia ya pili ambayo ni ya kijumuia na kibinadamu ikatumika kufidia upungufu huu. Nadharia ya kijumuia na kibinadamu ilichanganua kanuni za lugha shuleni na athari yake kwa somo la Kiswahili.

### **1.7.1 Nadharia ya Vitendo Vilivyofikiriwa**

Watangulizi wa nadharia hii ni Ajzen na Fishbein (1980). Nadharia ya Vitendo vilivyofikiriwa ni nadharia inayoeleza kwamba, binadamu anaweza kutumia maarifa aliyo nayo kwa utaratibu kwa sababu ni kiumbe razini. Wanaeleza kuwa ikiwa binadamu anafanya jambo ambalo litamnufaisha atakuwa na mtazamo kubalifu kuhusu jambo hilo na ikiwa halitakuwa na manufaa kwake, atakuwa na msimamo usiokubalifu. Swali ambalo binadamu hujiuliza kila wakati ni kwa namna gani atakavyofaidika na tendo kubalifu. Lengo kuu la nadharia hii ni kutabiri na kuelewa kikamilifu tabia ya mtu. Hivyo basi katika utafiti huu, nadharia hii ilisaidia mtafiti katika kuelewa tabia na mielekeo ya walimu na wanafunzi wa shule za upili kuhusu kanuni za lugha shuleni. Mielekeo yao iliweza kuwa chanya au hasi hivyo kubainisha ikiwa wanapenda au kuchukia kanuni za lugha za shule.

### **Mhimili ya nadharia ya Vitendo Vilivyofikiriwa**

- i. Hutabiri na kuelewa tabia za watu. Katika kuelewa na kutabiri tabia za watu ni sharti kutathmini kinachosababisha tabia hiyo. Wanaeleza kuwa si vigumu kutabiri tabia ya binadamu lakini wakati mwingine kutokana na matukio yasiyotabiriwa anaweza kubadilisha tabia yake. Utafiti huu unalenga kuchunguza mielekeo ya wanafunzi kuhusu kanuni za lugha shuleni. Mhimili huu ulifaa kwa sababu, kwa kurejelea tabia ya wanafunzi kuhusu kanuni za lugha shuleni, ilitubainishia mielekeo yao kuhusu kanuni hizo. Tabia ya wanafunzi kuhusu kanuni za lugha shuleni inaweza kuwa kubalifu au isiokubalifu. Mtafiti alitathmini kinachosababisha tabia ya mwanafunzi kuhusu kanuni za lugha shuleni kuwa kubalifu au la, hivyo kubainisha mwelekeo wake.
- ii. Nia ya mtu hutathminiwa na vipengele viwili vya kimsingi ; nia yake binafsi na pili ushawishi kutoka kwa jamii. Katika kipengele cha binafsi, binadamu hutathmini ikiwa tabia anayofanya itamnufaisha na hivyo atakuwa na mwelekeo chanya kuhusu tabia hiyo na ikiwa haitamnufaisha basi atakuwa na mwelekeo hasi. Kabla ya kutekeleza kanuni za shule, wanafunzi hujiuliza ikiwa kanuni hizo zitamsaidia katika somo la Kiswahili au la. Jibu la swali hili lilibainisha mwelekeo wa mwanafunzi huyo kuwa chanya au hasi. Vilevile mhimili huu ulisaidia kuchunguza sababu zinazomfanya mwalimu mkuu kuteua kanuni za lugha shuleni kwa kumuuliza baadhi ya maswali kama, je, kuna manufaa ya kanuni za lugha shuleni kwa mwanafunzi anayesoma Kiswahili. Hii ilisaidia kujibu swali la kwanza ambalo lilichunguza kanuni za lugha zinazotumiwa shuleni na sababu ya uteuzi wa kanuni hizi kwa shule za upili. Mhimili huu pia ulibainisha sababu ya walimu na wanafunzi kuwa na mielekeo chanya au hasi kuhusu kanuni za lugha.

Ushawishi kutoka kwa jamii pia hubainisha mwelekeo wa mtu kuwa chanya au hasi. Shule kama jamii hujumuisha wadau kama walimu, wazazi, wanafunzi na hata maafisa wa elimu. Kanuni za lugha shuleni huteuliwa katika jamii ambayo ni shule. Hivyo mielekeo ya wanajamii kama walimu na wanafunzi kuhusu kanuni za lugha shuleni ilitubainishia mwelekeo wa mwanafunzi kuhusu kanuni za lugha shuleni. Onyango (2008) anasema kuwa mwelekeo wa mwalimu kuhusu lugha ya pili anayoifunza huathiri mwelekeo wa mwanafunzi kwa kuipenda au kuichukia lugha hiyo.

Wataalamu hawa pia wanaeleza kuwa, ili kutambua ikiwa mielekeo ya mtu ni chanya au hasi, sharti kupima tabia yake kwa kumhoji au kumpa hojaji ajaze. Katika utafiti huu ili kupima mielekeo ya wanafunzi na walimu wa shule ya upili kuhusu kanuni za lugha shuleni, hojaji likati, majadiliano elekezi ya vikundi ni kati ya njia za utafiti ambazo zilitumika.

Nadharia ya vitendo vilivyofikiriwa ilimsaidia mtafiti kuchunguza mielekeo ya walimu na wanafunzi kuhusu kanuni za lugha shuleni. Pia, ilimsaidia kubainisha sababu za uteuzi wa kanuni za lugha katika shule za upili. Nadharia ya pili ilituliwa kwa lengo la kufidia upungufu wa nadharia ya Vitendo vilivyofikiriwa ambayo inachunguza tu mielekeo ya walimu na wanafunzi kuhusu kanuni za lugha za shule. Nadharia ya pili ya Kijumuia na Kibinadamu ya Richards na Rodgers (1995) inarejelea vipengele vilivyo katika kanuni za lugha za shule. Kanuni za lugha shuleni zinajumuisha sheria za ujifunzaji wa lugha ya pili na namna adhabu anayopewa mwanafunzi anapoenda kinyume na sheria hizi humuathiri anapojifunza lugha ya pili. Aidha shughuli kama mijadala na makongamano vimeshughulikiwa katika

nadharia ya kijumuia na kibinadamu. Hivyo kufidia upungufu wa nadharia ya vitendo vilivyofikiriwa.

### **1.7.2 Nadharia ya Kijumuia na Kibinadamu**

Nadharia hii iliasisiwa na Richards na Rodgers (1995). Nadharia hii ilijengeka kutoka kwa mawazo ya mtaalamu Charles Curran aliyekuwa profesa wa saikolojia katika chuo kikuu cha Loyola, Chicago. Curran (1976) anasema kuwa, mwanafunzi hujifunza vizuri akiwa na uhusiano mzuri na mwalimu. Katika mazingira ya shule, mwalimu ni kama mshauri na mwanafunzi ni kama msaidizi. Ili mwanafunzi aweze kujenga uhusiano mzuri na mwalimu wake, mwalimu ana wajibu wa kuhakikisha kuwa mazingira ya mwanafunzi ni salama na yenye utu. Kutokana na mawazo haya, Richards na Rodgers (keshatajwa) waliibuka na nadharia ya kijumuia na kibinadamu ambapo wanapendekeza namna ya ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya pili. Wanasema kuwa, katika kujifunza lugha ya pili, mwalimu ana jukumu la kuwa mshauri na msaidizi wa mwanafunzi. Nadharia hii inasisitiza ufunzaji ulio na utu na ubinadamu.

### **Mihimili ya Nadharia**

Kwa mujibu wa Richards na Rodgers (1995) katika nadharia ya Kijumuia na Kibinadamu, mihimili ya nadharia ya Kijumuia na Kibinadamu ni ifuatayo :

- i. Usalama wa mwanafunzi ni muhimu sana. Wanafunzi wakiwa na wasiwasi na kutohisi salama hawawezi kujifunza lugha vizuri. Baadhi ya shule za upili zilizofanyiwa utafiti huadhibu wanafunzi wanapoenda kinyume na kanuni za lugha shuleni. Jambo hili laweza kumpa mwanafunzi wasiwasi

hivyo kuathiri ujifunzaji wa lugha ya pili. Hali ya wasiwasi kuhusu lugha pia huondolewa ikiwa walimu watazingatia kanuni za lugha shuleni. Hivyo mtafiti alichunguza kupitia hojaji ikiwa walimu huzingatia kanuni za lugha shuleni hasa anapohitajika kuwasiliana kwa lugha ya Kiswahili.

- ii. Kutomakinika kwa wanafunzi kupunguzwe hasa kwa kuwapa majukumu tofauti tofauti katika ufundishaji. Mtafiti alichunguza namna kanuni za lugha shuleni zinawasaidia wanafunzi kumakinika katika mawasiliano kwa kuonyesha ujuzi waliojifunza katika somo la Kiswahili. Kanuni za lugha shuleni zinahusu namna lugha inavyotumiwa katika mawasiliano na katika shughuli kama mijadala na makongamano. Hivyo mtafiti alitazama namna wanafunzi walivyotumia lugha katika mijadala na mazungumzo nje ya darasa. Hii ilimsaidia mtafiti kubaini athari ya kanuni za lugha shuleni kwa somo la Kiswahili.
- iii. Wanafunzi wanafaa kujifunza lugha kwa njia mbalimbali kama vile kwa kutafsiri, kujirekodi katika kanda za kunasia sauti, vikundi, uchambuzi, usikilizaji na mazungumzo ya jumla. Kanuni za lugha shuleni zilichunguzwa ili kubainisha namna zinavyohusisha lugha ya Kiswahili katika vikundi, usikilizaji na mazungumzo ya jumla shuleni. Njia hizi pia zilimsaidia mtafiti kubainisha athari yake katika somo la Kiswahili.
- iv. Ujifunzaji ni jukumu la jumuiya ya wanafunzi pamoja na walimu. Mhimili huu ulimsaidia mtafiti kuchunguza mchango wa walimu pamoja na wanafunzi katika uteuzi na utekelezaji wa kanuni za lugha shuleni.

Vipengele kama mijadala ni kati ya shughuli zinazojumuishwa katika uteuzi wa kanuni za lugha shuleni. Baadhi ya shule huwaadhibu wanafunzi wanaoenda kinyume na sheria hizi. Jambo ambalo huzua wasiwasi. Kwa njia hii, mihimili ya nadharia ilimsaidia mtafiti katika kuainisha kanuni za lugha za shule kisha akatafiti kuhusu athari ya kanuni hizi za lugha katika somo la Kiswahili.

### **1.8. Mbinu za Utafiti**

Kulingana na Orodho (2003), mbinu za utafiti ni utaratibu maalumu unaotumiwa ili kuibuka na majibu ya maswali ya utafiti. Mambo yaliyoangaziwa katika sehemu hii ni, muundo wa utafiti, mahali pa utafiti, uteuzi wa sampuli, mbinu za ukusanyaji data, mbinu za uchanganuzi wa data, mbinu za uwasilishaji wa matokeo na uzingatiaji wa maadili.

#### **1.8.1. Muundo wa Utafiti**

Kothari (2007) anaeleza muundo wa utafiti kama mwongozo wa kutimiza malengo na kupata majibu ya maswali ya utafiti kwa kufuata utaratibu maalumu. Ili kuafikia malengo ya utafiti, utafiti huu ulitumia muundo wa kimaelezo. Kwa mujibu wa Mugenda na Mugenda (1999), utafiti wa kimaelezo hutoa ripoti ya jinsi mambo yalivyo katika mazingira fulani na hueleza kuhusu tabia, mielekeo, itikadi na hali mbalimbali za watu. Muundo wa kimaelezo ulifaa katika utafiti huu kwa sababu, maelezo kuhusu uteuzi wa kanuni za lugha katika mazingira ya shule tofauti yalihatijika. Maelezo pia yalihatijika ili kuelewa namna mielekeo ya walimu na wanafunzi kuhusu kanuni za lugha za shule inavyoathiri somo la Kiswahili.

## 1.8.2 Mahali pa Utafiti

Utafiti huu ulifanywa maktabani na nyanjani. Mapitio ya kazi na makala yanayohusiana na mada kwa mfano; machapisho, tafiti mbalimbali, tasnifu, vitabu na majarida yalifanyika maktabani. Kazi hizo zilisaidia katika kueleza na kuchanganua nadharia na masuala muhimu katika utafiti huu. Utafiti wa nyanjani ulifanywa katika shule saba kati ya jumla ya shule 153 kutoka kaunti ya Busia. Hii ni asilimia 4.6% ya shule zote katika Kaunti ya Busia. Kaunti ya Busia ina shule za viwango vya shule ya Kitaifa, shule za Kaunti za kiwango cha juu na shule za Kaunti. Sita ni za bweni na moja ya kutwa. Shule hizi zimeanishwa katika jedwali lifuatalo

**Jedwali 1.1 Uanishaji wa shule za Sekondari**

| <b>Kiwango cha shule</b> | <b>Idadi</b> |
|--------------------------|--------------|
| Kitaifa                  | 1            |
| Zaidi ya Kaunti          | 5            |
| Kaunti na kutwa          | 1            |
| <b>Jumla</b>             | <b>7</b>     |

Shule za upili nchini Kenya, zimegawanywa katika viwango vinne: za Kitaifa, Zaidi ya Kaunti, Kaunti na za Kaunti ndogo (School Net Kenya Consultation, 2014). Wizara ya elimu (2015) inaeleza kuwa, Shule za Kitaifa ni vituo vya ufanisi vilivyoteuliwa ili kuleta umoja wa taifa na mshikamano wa Kijamii. Ingawa Shule Zaidi ya Kaunti pia huwa vituo vya ufanisi baada ya kitaifa, wanafunzi katika shule zaidi ya Kaunti huteuliwa kutoka kaunti tofauti ili kuendeleza mshikamano wa Kijamii. Shule hizi huwa za bweni. Wanafunzi katika shule za Kitaifa na Zaidi ya Kaunti ziliteuliwa kwa sababu hutoka sehemu tofauti katika taifa la Kenya, hivyo

lugha ya mawasiliano mara nyingi huwa Kiswahili au Kiingereza. Shule za Kaunti huteua wanafunzi wengi kutoka kaunti hiyo. Shule hizi huwa za bweni na kutwa. Lugha ya mawasiliano katika shule hizi huwa lugha ya kienyeji, Kiswahili au Kiingereza. Vilevile, wanafunzi hawa wanaporudi nyumbani ni vigumu kutekeleza kanuni za lugha za shule. Ogolla (1990) anasema kuwa, katika mazingira ya nyumbani lugha ya Kiasili husisitizwa sana.

### **1.8.3 Uteuzi wa Sampuli**

Kothari (2007) anaeleza kuwa, sampuli ni sehemu ya kitu au watu fulani. Sehemu hii huteuliwa na kutumiwa kwa minajili ya kufanya maamuzi yanayohusu kundi zima. Sampuli ni idadi ndogo ya jumla inayochaguliwa kwa minajili ya kufanyiwa uchunguzi ili kuwasilisha matokeo ya idadi kubwa. Mbinu ya uteuzi nasibu ilitumika kuteua shule saba kati za shule za upili 153 zilizo kaunti ya Busia. Utafiti wa awali ulionyesha kuwa, shule hizi saba zinaongozwa na kanuni za lugha za shule ambazo ni tofauti. Kuna zile ambazo zimepiga marufuku matumizi ya lugha ya Kiswahili katika mazingira ya shule ilihali zingine zimetenga siku ya kuwasiliana katika lugha ya Kiswahili. Aidha shughuli za idara ya somo la Kiswahili zinatofautiana. Utafiti wa awali pia ulibaini matokeo ya mtihani katika somo la Kiswahili ni tofauti. Utafiti wa awali katika Shule ya Wasichana ya Kisoko ulionyesha kuwa lugha ya Kiswahili imepigwa marufuku lakini wana siku ya Kiswahili kila muhula, pia kuna siku za mijadala kwa lugha ya Kiswahili. Lugha ya Kiswahili huzungumzwa wakati wa somo la Kiswahili na Siku ya Kiswahili. Ingawa Shule ya wasichana ya Lwanya na Chakol zina mabango na maandishi yanayosisitiza wanafunzi wazungumze Kiingereza, wanafunzi wanaruhusiwa kuzungumza Kiswahili siku ya Ijumaa. Shule ya upili ya mseto ya Makunda imeteuliwa kwa kuwa ni kutwa na huzungumza

Kiswahili siku ya Ijumaa na wanaporudi nyumbani. Shule ya Wavulana ya Mundika iliteuliwa kwa kuwa lugha ya Kiswahili huzungumzwa wakati wa somo la Kiswahili lakini wana siku za mijadala kwa lugha ya Kiswahili. Pia idara ya Kiswahili huandaa makongamano ya ndani mwa shule. Shule ya Kitaifa ya wavulana ya Butula ina kanuni za lugha tofauti na wana chama cha Kiswahili. Wanafunzi huzungumza Kiswahili kuanzia Ijumaa hadi Jumapili. Katika shule ya upili ya Amukura, mawasiliano huwa kwa lugha ya Kiswahili au Kiingereza kuanzia Jumapili hadi Jumamosi.

Kutokana na lengo la utafiti la kupata mielekeo ya wanafunzi na walimu, wanafunzi 40 kutoka kidato cha pili na 40 kutoka kidato cha tatu. Jumla ya wanafunzi 560 kutoka shule saba ndio waliooteuliwa kujaza hojaji. Wanafunzi 40 walitolewa kwa kila mkondo. Walimu wa somo la Kiswahili saba ambao ni wakuu wa idara pia waliteuliwa ili kubainisha mielekeo yao kuhusu kanuni za lugha shuleni. Majibu yao yalimpa mtafiti habari alizohitaji kuhusu athari ya kanuni za lugha shuleni kwa somo la Kiswahili.

Shule za upili ya Wasichana ya Kisoko, Lwanya na Chakol ni za bweni. Shule za upili za Wavulana ya Butula, Mundika na Amukura aidha ni za bweni. Shule ya mseto ya Makunda ni ya kutwa. Wanafunzi wa shule ya kutwa walichaguliwa kwa sababu inachukuliwa kuwa uhusiano wao na wanajamii wanapoenda shuleni asubuhi na wanaporejea nyumbani jioni huathiri kanuni za lugha shuleni. Ogolla (1990) anasema kuwa, katika mazingira ya nyumbani, lugha ya kiasili husisitizwa sana. Hivyo mtagusano wao wa watu wanaozungumza lugha ya kwanza huwafanya kuathirika kwa sababu wao hutumia lugha yao ya kwanza katika mawasiliano.

#### **1.8.4 Ukusanyaji wa Data**

Kwa mujibu wa Kombo na Tromp (2006), ubora wa kazi yoyote ya utafiti hutegemea ubora wa data iliyokusanywa ili kuchanganuliwa. Mtafiti alikusanya data kutoka maktabani na nyanjani. Mtafiti alisoma machapisho mbalimbali maktabani kuhusu mada ya utafiti. Mtafiti alitumia mbinu ya mahojiano, uchunzaji, hojaji funge na hojaji likati pamoja na majadiliano elekezi kule nyanjani alipokuwa akikusanya data. Mbinu hizi zimejadiliwa katika sehemu ifuatayo:

##### **1.8.4.1 Mahojiano**

Kuhoji ni kukusanya data kwa kuwauliza walengwa maswali na kupata majibu kutoka kwao (Mugenda na Mugenda, 2003). Kuna aina nyingi za mahojiano kama vile mahojiano ya simu ya ana kwa ana. Mtafiti alitumia mahojiano ya moja kwa moja kuwahoji walimu wakuu na wakuu wa idara ya Kiswahili ili kupata habari kuhusu kanuni za lugha zilizo katika shule zao. Mahojiano haya yaliendeshwa ana kwa ana kwa kutumia usaili. (Tazama Kiambatisho cha A kwa walimu wakuu na kiambatisho G kwa wakuu wa idara ya Kiswahili). Mtafiti alitumia kalamu na karatasi kuandika hoja muhimu wakati wa mahojiano. Mtafiti pia litumia mbinu ya mahojiano kwa wakuu wa idara ya Kiswahili ili kubaini umuhimu wa kanuni hizi na sababu ya mielekeo yao kuhusu kanuni za lugha za shule. Kulingana na Seliger na Shohamy (1989), mbinu ya mahojiano humwezesha mtafiti kufafanua vipengele tata vya maswali na kudadisi zaidi hasa pale ambapo majibu hayakukamilika.

#### **1.8.4.2 Uchunzaji**

Onen (2005) anasema kuwa, uchunzaji ni ushuhudiaji wa tukio linapotendeka na kukusanya taarifa zake. Ni kitendo cha kuchunguza watafitiwa wanafanya nini badala ya kuwauliza maswali. Kulingana na Kipchirchir (2019), uchunzaji ni njia muhimu sana katika utafiti kwani ndiyo njia ya pekee isiyo na ubaguzi. Ni kwa msingi huu ambapo uchunzaji ulichaguliwa kukusanya data kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili kwenye mijadala na gwaride. Aidha mtafiti alitumia mbinu hii ya kukusanya data kwa kushuhudia mabango na maandishi yanayopatikana shuleni hasa yanayohimiza matumizi ya lugha shuleni (Tazama kielelezo 1.1, .1.2, 1.3). Mtafiti pia alitumia mbinu hii alipopata nafasi ya kuhudhuria mijadala ya shule wakati wa jioni. Katika mijadala hii, mtafiti alitazama jinsi wanafunzi walivyotumia lugha ya Kiswahili kujadili mada husika. Pia alitaka kujua michango ya walimu wa somo la Kiswahili walipohudhuria mijadala shuleni mwao.

#### **1.8.4.3 Hojaji**

Huwa ni maswali yanayoandaliwa kwa kutumia utaratibu maalum kwa lengo la kukusanya data iliyokusudiwa (Kothari, 2007). Mbinu hii ya utafiti ilitumika kukusanya habari kuhusu kanuni za lugha katika shule za upili Kaunti ya Busia na mielekeo ya walimu na wanafunzi kuhusu kanuni za lugha za shule. Ili kupata habari kuhusu ni kanuni zipi za lugha zinazotumiwa shuleni, hojaji funge ilitumika kwa walimu na wanafunzi walipohitajika kuchagua mojawapo ya majibu yaliyoorodheshwa kwenye hojaji (Tazama kiambatisho B na C). Utafiti kuhusu mielekeo ya walimu na wanafunzi kuhusu kanuni za lugha za shule ilikusanywa kwa kutumia hojaji iliyoandaliwa kufuatia mfumo wa likati. Baada ya kupata vitabu na machapisho mengine mbalimbali kuhusu swala la mielekeo ya lugha, mtafiti

alikusanya kauli 15 kutoka kwa wanafunzi na kauli 14 kutoka kwa walimu wa somo la Kiswahili ambao ni wakuu wa idara. Kauli hizi zilijumuishwa kuunda hojaji likati (Tazama kiambatisho D na F). Majibu yalitolewa kwa kauli hizo yalipewa alama kulingana na mfumo wa Likati (Jahoda na Warren, 1966). Kulingana na mfumo huu, majibu huonyeshwa kwa kutumia vibadala vitano. Vibadala hivi hueleza kiwango cha kukubaliana ama kutokubaliana na kauli fulani ambazo ni;

Nakubali kabisa

Nakubali

Sikubali wala sikatai

Nakataa

Nakataa kabisa

Hojaji hizi ziligawiwa wakuu wa idara saba na wanafunzi 560 kutoka shule saba zilizoteuliwa. Walichagua jibu moja kutoka kwa vibadala 5 walivyopewa vinavyoeleza kiwango cha kukubaliana ama kutokubaliana na kauli fulani. Kauli ya nakubali na nakubali kabisa ilionyesha mielekeo chanya ilhali ya nakataa na nakataa kabisa ilionyesha mielekeo hasi. Mtafiti aliunda hojaji hizo ili kutimiza lengo la pili la utafiti kuhusu mielekeo.

#### **1.8.4.4 Majadiliano Elekezi ya Vikundi**

Utafiti huu pia ulitumia majadiliano elekezi wa vikundi ili kupata taarifa muhimu kutoka kwa wanafunzi. Mtafiti alitaka kujua sababu ya mielekeo ilioonyeshwa kutoka kwa hojaji likati (Tazama kiambatisho E) na maoni yao kuhusu manufaa ya kanuni za lugha za shule. Kulingana na Dawson na wenziwe (1993), majadiliano elekezi ya vikundi ni mbinu ya kudadisi imani za watu, mielekeo na maoni yao

kuhusu jambo. Mbinu hii ina manufaa kwa kuwa inaweza kuibua habari upesi kushinda mahojiano ya mmoja mmoja. Baada ya wanafunzi kujaza hojaji likati, mtafiti aliteua makundi tano ya wanafunzi wanane kwa kila kidato kwa kila shule. Kidato cha pili kilikuwa na vikundi tano na kila kikundi na wanafunzi wanane. Kidato cha tatu vile vile kilikuwa na vikundi tano, na kila kikundi kikawa na wanafunzi wanane. Kila shule ilikuwa na makundi ya mijadala elekezi. Idadi ya wanafunzi wanane katika kila kikundi ilikuwa mwafaka kwa sababu kikundi chenye idadi chache ya wasailiwa huishia kutawaliwa na mtu mmoja au wawili na makundi makubwa huzuia nafasi ya mjadala kwa wasailiwa wengine (Sherraden, 1995 na Dawson na wenziwe, 1993). Kila mjadala ulichukua saa mbili ambayo ni muda uliopendekezwa na mtaalamu (Sherraden, 1995). Mwongozo wa haya majadiliano elekezi ulikuwa na maswali 16, ambapo kila swali lilihitaji jibu la kutaja au kueleza umuhimu wa kanuni hizi ili kupima mwelekeo wa mwanafunzi kuhusu kanuni za lugha za shule kama zilivyo katika kauli za likati. Kila swali lilifuatwa na swali la kuuliza sababu za jibu hilo la wanafunzi. Sababu zilizotolewa zilisaidia utafiti huu kufahamu sababu za wanafunzi kuwa na mielekeo ilioonyeshwa katika majibu ya hojaji likati na manufaa ya kanuni za lugha za shule.

#### **1.8.4.5 Matokeo ya Mtihani wa Kitaifa**

Matokeo ya watafiti kama (Nyakeoga 2018, Nyongesa na wenzake 2022, Ogero 2012) yameonyesha kuwa, utekelezaji wa kanuni za lugha za shule una athari katika matokeo ya mitihani ya kitaifa. Kwa mfano kulingana na Nyongesa na wenzake (2022), wanasema kuwa, matokeo mabaya katika mitihani ya Kitaifa kwa somo la Kiswahili kwa njia moja hutokana na kutoajibika katika utekelezaji wa kanuni za lugha za shule. Ili kufafanua lengo la tatu la utafiti, mtafiti alipata matokeo ya

mtihani wa Kitaifa katika somo la Kiswahili kutoka ofisi za Elimu Kaunti ya Busia kama ifuatavyo;

**Jedwali 1.2 Matokeo ya Mtihani wa Kitaifa katika shule saba za Kaunti ya Busia**

| <b>Shule<br/>Mwaka</b> | <b>2020</b> | <b>2021</b> | <b>2022</b> | <b>2023</b> |
|------------------------|-------------|-------------|-------------|-------------|
| Butula                 | 8.904       | 9.101       | 9.327       | 10.45       |
| Mundika                | 5.395       | 5.725       | 8.32        | 7.37        |
| Amukura                | 5.98        | 5.29        | 5.58        | 7.01        |
| Lwanya                 | 8.776       | 8.949       | 8.500       | 9.625       |
| Chakol                 | 6.245       | 7.871       | 8.775       | 8.819       |
| Kisoko                 | 6.8073      | 8.430       | 7.836       | 8.4223      |
| Makunda                | 4.750       | 3.5029      | 4.700       | 4.232       |

Lengo muhimu la kifaa hiki ni kupata habari kuhusu athari ya kanuni za lugha za shule kwa somo la Kiswahili kwa shule zilizoteuliwa katika Kaunti ya Busia. Mtafiti alitumia matokeo ya mitihani ya mwaka wa 2020, 2021, 2022 na 2023.

**1.8.5 Uchanganuzi wa data**

Data iliyokusanywa ilichanganuliwa kwa kuzingatia maswali na malengo ya utafiti. Uchanganuzi wa data ili kutambua mielekeo ya watafitiwa ulifanywa kwa kurejelea nadharia ya vitendo vilivyofikiriwa ya Ajzen na Fishbein (1980). Mihimili ya nadharia hii ilisaidia kutambua mielekeo ya wanafunzi kuhusu kanuni za lugha shuleni. Matokeo ya hojaji likati na mijadala elekezi ya vikundi ilipangwa na kuainishwa kwa kutumia idadi na asilimia kwa jedwali. Majibu yalielezwa kwa kifupi. Data zingine zilikusanywa na kuchanganuliwa kwa kulinganisha na mihimili ya nadharia ya kijumuia na kibinadamu ya Richards na Rodgers (1995) ambayo inaorodhesha vipengele muhimu katika ujifunzaji wa lugha ya pili. Vipengele hivi ndivyo vilitubainishia kanuni za lugha shuleni. Matokeo ya mitihani katika shule saba teule ilimsaidia mtafiti kufafanua athari ya kanuni za lugha kwa somo la

Kiswahili. Data hizi pia zilipangwa katika mada tofauti kulingana na malengo ya utafiti.

### **1.8.6 Uwasilishaji wa Matokeo**

Data iliyokusanywa iliwasilishwa kwa kutumia maelezo, majedwali, chati na vielelezo. Njia za uwasilishaji data zilitilia maanani malengo ya utafiti ambayo ni; Kueleza kanuni za lugha za shule, kuchunguza mielekeo ya wanafunzi na walimu wa shule za upili kuhusiana na kanuni za lugha shuleni na kufafanua athari ya kanuni za lugha shuleni kwa somo la Kiswahili katika Shule za upili Kaunti ya Busia. Matokeo yaliyowasilishwa yalitokana na mahojiano kati ya mtafiti na walimu wakuu pamoja na wakuu wa idara ya Kiswahili. Maoni mbalimbali kuhusu kanuni za lugha za shule yalinukuliwa na kuandikwa. Matokeo ya uchunzaji na hojaji yaliwasilishwa katika majedwali, vielelezo na chati.

### **1.8.7 Maadili ya utafiti**

Utafiti huu umezingatia taratibu maalumu za maadili. Mtafiti alipata kibali cha kufanya utafiti kutoka NACOSTI na ruhusa ya Chuo Kikuu cha Kenyatta ya kuenda kufanya utafiti nyanjani. Suala la utafiti liliwekwa wazi kwa kila kundi lengwa ili kurahihisha upatikanaji wa data. Aidha mtafiti alionyesha vifungu vya maneno kutoka kwa watafiti na waandishi wengine kwa kufanya unukuzi wa maandishi yao pamoja na mchango wao. Kulingana na Mligo (2012), wizi wa kitaaluma ni kinyume na maadili ya uandishi. Wizi huu huhusisha wizi wa maneno, mawazo au vifungu vya maneno kutoka kwa watafiti au watu wengine bila kuonyesha chanzo chake.

## **1.9 Hitimisho**

Sura hii imechunguza vipengele vya kimsingi katika utafiti huu kama vile; usuli wa mada, suala la utafiti, malengo na maswali ya utafiti, sababu za kuchagua mada ya utafiti, upeo na mipaka ya utafiti, yaliyoandikwa kuhusu mada, misingi ya nadharia na mbinu za utafiti. Aidha, sura hii ina malengo ambayo yalipaswa kutimizwa kufikia mwishoni mwa utafiti huu. Sura inayofuata ilichunguza kanuni za lugha katika shule za upili Kaunti ya Busia.

## **SURA YA PILI**

### **KANUNI ZA LUGHA KATIKA SHULE ZA UPILI**

#### **2.0 Utangulizi**

Katika sura hii, lengo la kwanza ambalo ni kueleza kanuni za lugha za shule limechanganuliwa. Kanuni za lugha za shule ni muhimu katika utafiti huu kwa kuwa zimesaidia kuweka msingi wa sura zilizofuata baadaye. Sura hii imefafanua kanuni za lugha za shule kama vile; Lugha ya mawasiliano katika mazingira ya shule, siku za Kiswahili, mabango na maandishi katika mazingira ya shule, matumizi ya lugha ya Kiswahili katika mijadala na shughuli za idara. Sehemu hii imeongozwa na nadharia ya Kijumuia na Kibinadamu ya Richards na Rodgers (1995). Ili kufanikisha lengo la utafiti huu kuhusu kanuni za lugha katika shule za upili, mtafiti alipeana hojaji kwa wakuu wa idara ya Kiswahili na wanafunzi kutoka shule teule saba za Kaunti ya Busia, alifanya mahojiano na walimu wakuu saba ili kupata sababu ya uteuzi wa kanuni za lugha za shule.

#### **2.1 Kanuni za lugha katika shule**

Nyakeoga (2018) anasema kuwa, kanuni za lugha shuleni ni mikakati ya utendakazi iliyokubaliwa au kuchaguliwa na kundi la watu. Ni misimamo ambayo shule huamini na hivyo huathiri mienendo yao. Misimamo hii hukubaliwa na kuteuliwa na shule na huhusiana na matumizi ya lugha katika mazingira ya shule.

Kwa mujibu wa Koko (2016), sheria za lugha shuleni ni shughuli au kanuni ambazo huteuliwa ili kuwaongoza wanafunzi katika mawasiliano. Sheria hizi huhakikisha kuwa matumizi ya lugha shuleni yameimarishwa kupitia shughuli kama vile, uteuzi wa siku za Kiswahili au Kiingereza, matumizi ya mabango na maandishi katika mazingira ya shuleni, mijadala au midahalo ya wanafunzi na shughuli za idara ya lugha. Shughuli za idara hii zinajumuisha makongamano, kusoma vitabu na magazeti na vyama vya Kiswahili. Kimemia (2001) anasema kuwa, mtindo wa kufundisha Kiswahili kwa kutumia ubao na chaki tu umepitwa na wakati. Ufundishaji wa somo la Kiswahili unapasa kujenga stadi zote za lugha kama vile kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika. Wanafunzi wakipata umilisi wa lugha katika stadi zote, watajiamini na pia kuwa na ufundi wa lugha. Kwa hivyo, Sheria hizi huteuliwa kwa lengo la kumsaidia mwanafunzi katika kumudu stadi zote za lugha ya Kiswahili.

Katika mahojiano na walimu wakuu, hojaji walizojaza walimu wa somo la Kiswahili pamoja na wanafunzi katika kutaka kubaini kanuni za lugha shuleni, matokeo ya utafiti yalionyesha kanuni mbalimbali zikiwemo: Lugha ya mawasiliano katika mazingira ya shule, siku za Kiswahili, mabango na maandishi katika mazingira ya shule, matumizi ya lugha ya Kiswahili katika mijadala na shughuli za idara. Kanuni ya lugha ya mawasiliano katika mazingira ya shuleni ilichanganuliwa kwanza.


### **2.1.1 Lugha ya mawasiliano katika mazingira ya shuleni**

Aruba (2017) anasema kuwa, lugha hutumia njia ya maandishi na mazungumzo kupitisha ujumbe kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine. Wanafunzi hujua lugha kupitia kutagusana wao wenyewe. Wanafunzi hawa wanapotagusana, hubadilishana mawazo na kuchagua maneno yanayofaa kutumiwa katika miktadha. Kwa hivyo, lugha ya mawasiliano ni lugha iliyoteuliwa katika mazingira fulani ili itumike na wanafunzi kupitisha ujumbe kwa njia ya maandishi na mazungumzo wakiwa shuleni. Kanuni za lugha shuleni hueleza kinagaubaga lugha ambayo mwanafunzi anafaa kuwasiliana nayo akiwa shuleni (Nyakeoga 2018).

Matokeo ya utafiti yalibaini kuwa, lugha ya mawasiliano inayokubaliwa katika mazingira ya shule za upili kutoka Kaunti ya Busia ni Kiswahili na Kiingereza. Lugha zote za kiasili zimepigwa marufuku katika shule zote saba za utafiti katika Kaunti ya Busia kwa sababu ya kutaka kuboresha matokeo ya somo la Kiswahili. Kando na Kiswahili kuwa somo la lazima katika shule za upili, katika katiba ya Kenya (2010), lugha ya Kiswahili ni lugha rasmi na pia kuwa lugha ya taifa. Shuleni kuna mkusanyiko wa wanafunzi kutoka makabila mbalimbali, hivyo lugha ya Kiswahili hutumiwa kuondoa ubaguzi kwani ndio lugha unganishi (Ryanga, 2002).

Kupitia mbinu ya uchunzaji, mtafiti aligundua kuwa sheria za shule, kumbukumbu za mikutano ya idara ya Kiswahili na mabango yaliyo kwenye mazingira ya shule, yanaonyesha kuwa kuna matumizi ya Kiswahili na Kiingereza. Kwa hivyo, mtafiti alitaka kujua ikiwa lugha ya Kiswahili huzungumzwa kila siku shuleni au la. Majibu ya wakuu wa idara ya Kiswahili saba na wanafunzi 560 yamebainishwa katika grafu 2.1. na chati 2.1. Kauli iliojazwa kwenye hojaji ni *Mimi huwasiliana kwa lugha ya Kiswahili shuleni.*

**Grafu 2.1 Majibu ya wanafunzi kuhusu lugha ya mawasiliano shuleni**




Katika grafu 2.1, asilimia 44.82 ya wanafunzi kutoka shule saba teule walikubali kuwa wao huzungumza lugha ya Kiswahili kila siku. Jumla ya wanafunzi asilimia 2.5 hawakukubali wala kukataa kwa kuwa hawakuwa na uhakika. Asilimia 44.82 ya wanafunzi wanaowasiliana kwa lugha ya Kiswahili wakiwa shuleni, walisema kuwa, lugha ya Kiswahili ni lugha ya taifa na hurahisisha mawasiliano yao. Utafiti uligundua kuwa, baadhi ya wanafunzi huzungumza lugha ya Kiswahili hata ikiwa si siku ya kuwasiliana kwa lugha ya Kiswahili. Asilimia 2.5 ya wanafunzi ambao hawana uhakika, walisema kuwa wakati mwingine hujipata wakizungumza lugha ya sheng au ya kwanza hasa penye hakuna walimu au viranja.

Katika shule ya upili ya Makunda ambayo ni ya kutwa, mtafiti alibaini kuwa, wanafunzi katika shule hii wanapenda kuwasiliana kwa lugha ya kienyezji au sheng' wakiwa shuleni. Matokeo haya yanawiana na ya Kevogo na wengine (2015), wanasema kuwa, katika shule nyingi za upili, kanuni za lugha shuleni, zinaruhusu mawasiliano kwa lugha ya Kiswahili au Kiingereza. Kuna baadhi ya wanafunzi

hukiuka kanuni hizi na kutumia lugha ya Kwanza. Wanasema kuwa, kuna baadhi ya wanafunzi kutoka shule za Upili za kutwa ambao wanapendelea kuwasiliana kwa lugha za kiasili au sheng' wakiwa shuleni. Jumla ya wanafunzi asilimia 52.68 waliokataa kuwa hawawasiliani kwa lugha ya Kiswahili, walisema kuwa, kanuni za lugha shuleni haziharuhusu kuwasiliana kwa lugha ya Kiswahili kila siku.

Kutokana na data hii, mtafiti alibaini kuwa, kati ya kanuni za lugha za shule, kuna siku ambazo hutengewa mawasiliano kwa lugha ya Kiswahili. Wakuu wa idara ya Kiswahili kutoka shule saba walijaza hojaji. Kauli waliojaza ni, *wanafunzi huwasiliana kwa lugha ya Kiswahili*. Majibu yao yaliwasilishwa kwa chati 2.1 kama ifuatavyo.

### **Chati 2.1 Majibu ya wakuu wa idara ya Kiswahili kuhusu lugha ya mawasiliano shuleni**




Kwa kurejelea chati 2.1, Asilimia 29 ya wakuu wa idara ya lugha ya Kiswahili walisema kuwa huwasikia wanafunzi wakizungumza lugha ya Kiswahili kila siku. Lugha hii hupendwa na wanafunzi kwa kuwa hurahisisha mawasiliano yao. Asilimia 57 ya wakuu wa idara ya Kiswahili walisema kuwa wanafunzi hawazungumzi lugha ya Kiswahili kila siku kwa sababu kuna siku ambayo imetengewa mawasiliano kwa lugha ya Kiswahili. Kwa hivyo wanafunzi wakipatikana wakiwasiliana kwa lugha ya Kiswahili huadhibiwa. Asilimia 14 ya wakuu wa idara ya Kiswahili hawakuwa na uhakika. Walisema kuwa, baadhi ya wanafunzi huzungumza sheng' au lugha za kienyeji. Kupitia mahojiano na walimu wakuu, mtafiti aliwauliza swali lifuatalo, *Taja lugha zinazotumiwa katika mawasiliano shuleni.* Mtafiti alibaini kuwa, lugha ya mawasiliano ni Kiswahili na Kiingereza ingawa mtafiti alibaini kuwa, kuna baadhi ya walimu ambao si wa somo la Kiswahili au Kiingereza huzungumza sheng'. Wakati mwingine, walimu hawa huwasiliana na wanafunzi kwa kuchanganya lugha ya Kiswahili na Kiingereza. Wengi wa walimu hawa ni wa umri wa 25-40.

### **2.1.2 Siku za Kiswahili**

Siku ya Kiswahili ni siku ambayo lugha ya Kiswahili imetengewa kuzungumzwa na wanafunzi katika mazingira ya shule. Kutokana na uchunguzi, kuna siku ambazo hutengwa na viongozi wa shule au idara ya lugha kwa mawasiliano kwa lugha ya Kiswahili. Siku hii huteuliwa ili kuimarisha mawasiliano kwa lugha ya Kiswahili. Krashen (1985) anasema kuwa, ni muhimu kwa wanafunzi wanaojifunza lugha ya pili, kuwasiliana kwa lugha lengwa. Ili kuibua habari hii, kauli ziafuatazo zilijazwa kwenye hojaji na wanafunzi na walimu wa somo la Kiswahili. Walimu hawa pia wakuu wa idara ya Kiswahili. Swali ambalo wanafunzi waliulizwa ni, *kuna siku ambayo imetengewa kuwasiliana kwa lugha ya Kiswahili shuleni.*

**Grafu 2.2 Majibu ya wanafunzi kuhusu Siku ya Kiswahili**



Kwa mujibu wa grafu 2.2, Kati ya wanafunzi 560 kutoka shule saba teule, Asilimia 58.24 walikubali kuwa kuna siku ambayo imetengewa mawasiliano katika lugha ya Kiswahili. Wanafunzi 28.55% katika shule za utafiti walisema kuwa, mawasiliano katika lugha ya Kiswahili hayaruhusiwi hasa katika mazingira ya shule. Asilimia 13.21 ya wanafunzi ambao hawakuwa na msimamo walisema kuwa, hakuna siku ambayo imetengewa kuzungumza kwa lugha ya Kiswahili. Wanafunzi wana uhuru katika uamuzi wa lugha ya mawasiliano, Kiswahili au Kiingereza. Kanuni hizi za shule zimebaki tu kuwa katika maandishi.

Utafiti huu aidha ulibaini kuwa, katika shule ya Kitaifa ya Butula, Shule ya wasichana ya Chakol na Shule ya Mseto ya Makunda, kuna siku maalum ya wanafunzi kuzungumza katika lugha ya Kiswahili. Katika shule ya upili ya wavulana ya Mundika na Shule ya upili ya wasichana ya Kisoko, lugha ya Kiswahili imepigwa marufuku ingawa kuna shughuli za idara ambazo huwapa wanafunzi fursa

ya kuzungumza lugha ya Kiswahili. Aidha katika shule hizi, lugha ya Kiswahili hutumiwa wakati wa somo la Kiswahili.

Katika shule ya upili ya wasichana ya Kisoko, kupitia mbinu ya mahojiano, mwalimu mkuu alipoulizwa, *Eleza sababu za Kiswahili kupigwa marufuku*. Mwalimu mkuu alisema kuwa, mawasiliano kwa lugha ya Kiswahili imepigwa marufuku kwa sababu, badala ya wanafunzi kuzungumza lugha sanifu ya Kiswahili, wao huzungumza Sheng'. Hali hii huathiri uandishi wa insha za Kiswahili. Kulingana na utafiti wa Kachipela (2014), wanafunzi hujumuisha leksimu za Sheng' na zile za Kiswahili sanifu wakati wanapoandika insha zao. Watahini huona kama uchafuzi wa lugha ya Kiswahili sanifu. Hii huchangia mwanafunzi huyu kupata alama zisizoridhisha katika somo zima la Kiswahili.

Mwalimu mkuu wa shule ya upili ya wavulana ya Mundika alisema kuwa, walimu wa somo la Kiswahili hutaka wanafunzi watengewe siku ya Kiswahili lakini hawawajibiki katika utekelezaji wa kanuni hii. Walimu hawa hawahakikishi kuwa wanafunzi wanazungumza Kiswahili sanifu. Hivyo, aliona bora wanafunzi wazungumze lugha ya Kiingereza kwa kuwa masomo mengi isipokuwa somo la Kiswahili hutahiniwa kwa lugha ya Kiingereza. Aidha ni rahisi kwa walimu wote katika shule yake kuhakikisha kuwa wanafunzi wanawasiliana kwa lugha ya Kiingereza kuliko lugha ya Kiswahili.

Kwa mujibu wa nadharia ya Kijumuia na Kibinadamu, Richards na Rodgers (1995), wanasema kuwa, wanafunzi wanafaa kujifunza lugha kwa njia mbalimbali kama tafsiri, kujirekodi katika kanda za kunasia sauti, vikundi, uchambuuzi, usikilizaji na mazungumzo kwa jumla kwa hivyo, siku za Kiswahili huwa njia moja ambayo


humpa mwanafunzi fursa ya kuzungumza na kusikilizwa kwa lugha ya Kiswahili akiwa katika mazingira ya shule. Utafiti pia ulibaini kuwa, siku za Kiswahili huwapa walimu wakuu na walimu wa zamu, fursa ya kupitisha ujumbe kwenye gwaride kwa lugha ya Kiswahili. Siku hii, wanafunzi wa chama cha wanahabari huwasiliaa kwa lugha ya Kiswahili sanifu hivyo kuimarisha somo la Kiswahili. Munialo (2010) anasema kuwa, baadhi ya mikakati ambayo hufanya mwanafunzi kupenda somo la Kiswahili ni kama kumpa fursa ya kuzungumza lugha ya Kiswahili mbele ya wanafunzi wengine.

Mtafiti pia alitaka kujua ikiwa walimu wote katika shule za upili teule huzungumza lugha ya Kiswahili hasa siku ya Kiswahili. Hii ni kwa sababu, walimu huwa kielelezo kwa wanafunzi ambao wangependa kujifunza Kiswahili sanifu. Imethibitishwa na watafiti wengi kuwa, wanafunzi hupata motisha ya kuzungumza Kiswahili kutoka kwa walimu wao. Kulingana na utafiti wa Koko (2016) akimnukuu Kembo – Sure (1996), walimu huchukuliwa kama watekelezaji wa sera za lugha shuleni. Hivyo basi, wanafunzi huiga wafanyacho walimu wao.

Swali alilouliza mtafiti ni, Je, *walimu huzungumza lugha ya Kiswahili siku ya Kiswahili?* Utafiti ulibaini kuwa, walimu ambao huzungumza lugha ya Kiswahili ni wale wanaofunza somo la Kiswahili. Baadhi ya walimu wanaofunza masomo mengine huchanganya lugha ya Kiswahili na Kiingereza hasa wanapowasiliana na wanafunzi. Baadhi yao, huwasiliana na wanafunzi kwa lugha ya Sheng' huku wakidhani kuwa wanazungumza Kiswahi sanifu. Maoni haya yanafanana na utafiti wa Mekonge (2016) anayesema kuwa, baadhi ya walimu hutumia Sheng' wanapowasiliana na wanafunzi. Hivyo wanafunzi huiga kile wafanyacho walimu wao hasa wa somo la Kiswahili.

Kupitia hojaji mtafiti pia alitaka kujua ikiwa kuna siku ambayo imetengewa lugha ya Kiswahili kwa kuwauliza swali lifuatalo, *Kuna siku ambayo imetengewa kuzungumza kwa lugha ya Kiswahili*. Majibu ya swali hili yamewasilishwa katika chati kama ifuatayo:

### Chati 2.2 Majibu ya wakuu wa idara kuhusu siku ya Kiswahili



Kwa mujibu wa Chati 2.2, asilimia 57 ya wakuu wa idara ya Kiswahili wanakubali kuwa kuna siku ambayo imetengewa wanafunzi kuzungumza kwa lugha ya Kiswahili. Wakuu wa idara 14 hawana uhakika ikiwa kuna siku iliyotengewa wanafunzi kuwasiliana kwa lugha ya Kiswahili. Wakuu wa idara walisema kuwa, wanafunzi wana hiari ya kuwasiliana kwa lugha ya Kiswahili. Asilimia 29 ya wakuu wa idara ya Kiswahili walisema kuwa hakuna siku ya Kiswahili kwa kuwa mawasiliano kwa lugha ya Kiswahili yamepigwa marufuku.

Katika shule ya upili ya wavulana ya Amukura, mwalimu mkuu alipoulizwa, *Eleza sababu za Kiswahili kuwa na idadi ya siku hizo*. Mwalimu mkuu alisema kuwa, wanafunzi wako huru kuzungumza lugha ya Kiswahili au Kiingereza. Hawana siku

iliyotengwa kuwasiliana kwa lugha fulani. Mwalimu huyu pia alisema kuwa, yeye huwahimiza wanafunzi kuwasiliana kwa lugha ya Kiswahili kwa sababu, wanafunzi wengi wanatoka katika jamii ya Wateso, hivyo wasipowasiliana kwa lugha ya Kiswahili, wanaweza kuathirika katika uandishi wa mitihani ya somo la Kiswahili.

Ni wazi kuwa, katika shule saba za utafiti isipokuwa shule ya Upili ya Amukura, Kiswahili kimepewa siku chache katika mawasiliano. Katika mohojiano na walimu wakuu wa shule, mtafiti alitaka kujua sababu ya Kiswahili kupewa siku chache katika mawasiliano. Swali ambalo mtafiti aliuliza ni, *Ni sababu gani lugha ya Kiswahili ikapewa siku chache?* Matokeo ya utafiti yalionyesha kuwa, wakuu wa shule katika kaunti ya Busia huteua siku chache za mawasiliano kwa lugha ya Kiswahili kwa sababu masomo yote hufunzwa na kutahiniwa kwa lugha ya Kiingereza isipokuwa somo la Kiswahili. Kwa hivyo ni muhimu kwa wanafunzi kuwasiliana katika lugha ya Kiingereza ndiposa matokeo ya shule yawe mazuri kwa masomo yote.


### **2.1.3 Mabango na maandishi katika mazingira ya shule**

Kulingana na kamusi ya Kiswahili sanifu ya TUKI (2004), bango ni karatasi gumu au kadi kubwa lenye matangazo au ujumbe maalum. Mtafiti alipotembelea shule saba za utafiti, aliweza kuona mabango tofauti katika uga wa shule. Shule zote saba zilikuwa na aina tofauti ya mabango. Koko (2016) anasema kuwa, mabango huwekwa kwa lengo la kuelimisha wanafunzi, kuelekeza wapita njia na kushauri mwanafunzi yale ambayo anapaswa kufanya (Tazama mfano wa mabango katika kielelezo cha E, 1.1; 1.2; na 1.3). Mabango haya yaliwekwa maeneo mateule kuwakumbusha wanafunzi na wapita njia kwamba wanapaswa kuzungumza kwa

lugha sanifu. Katika kuzuru na kutazama mabango yaliyo shuleni, mtafiti alibaini kuwa, kuna mabango yenye maandishi tofauti katika mazingira ya shule. Ingawa mabango haya yanawiana na kanuni za lugha shuleni, idadi kubwa ya mabango haya yanatukuza lugha ya Kiingereza ishara kuwa lugha ya Kiingereza inathaminiwa sana.

Mtafiti pia alibaini kuwa, katika ubao wa matangazo ya shule, matangazo na maandishi mengi yalikuwa kwa lugha ya Kiingereza. Ni shule ya upili ya Chakol na Mundika ambapo mtafiti alipata insha za wanafunzi bora zimewekwa kwenye ubao wa matangazo. Hii iliwapa wanafunzi motisha ya kufanya vyema hasa kwenye insha. Ili kuibua habari kuhusu umuhimu wa mabango na maandishi kwenye ubao wa matangazo katika kuimarisha lugha ya Kiswahili. Hojaji yenye kauli Mabango na maandishi yana umuhimu katika kuimarisha somo la Kiswahili ilijazwa. Majibu ya kauli hii yaliwasilishwa kwa grafu 2.4.

**Grafu 2.3 Majibu ya wanafunzi kuhusu mabango na maandishi shuleni**



Kulingana na majibu ya wanafunzi katika grafu 2.3, kati ya wanafunzi 560 waliojaza hojaji, asilimia 28.04 ya wanafunzi wanakubali kuwa mabango na maandishi husaidia katika kuimarisha somo la Kiswahili. Wanafunzi hawa walisema kuwa, mabango haya huwakumbusha lugha wanayopaswa kuzungumza wakiwa shuleni. Katika shule ya upili ya Chakol, asilimia 96 ya wanafunzi wanakubali kuwa baadhi ya mabango haya huhimiza wanafunzi kuzungumza lugha sanifu na kujiepusha na matumizi ya lugha ya Sheng'. Huwa ni kama njia ya kuwakumbusha wanafunzi lugha mwafaka katika mawasiliano shuleni. Bango hili linapatikana katika shule ya upili ya Chakol (Tazama kiambatisho 1.4). Kati ya wanafunzi 560 kutoka shule zote saba, asilimia 13.21 ya wanafunzi hawana uhakika ikiwa mabango na maandishi yanaimarisha somo la Kiswahili. Wanafunzi hawa walisema kuwa, katika mazingira ya shule, mabango haya hayana uhusiano wowote na lugha ya Kiswahili. Hivyo, ni vigumu kujua ikiwa yana umuhimu wowote. Asilimia 58.75 ya wanafunzi waliokataa kauli hii wanasema kuwa, ingawa kuna mabango na maandishi katika mazingira ya shule, mabango haya yanasisitiza matumizi ya lugha ya Kiingereza hivyo huwa kikwazo katika uendelezaji wa lugha ya Kiswahili. Katika shule ya upili ya Mundika na Lwanya, mabango haya yanakitukuza lugha ya Kiingereza.

#### **2.1.4 Matumizi ya lugha ya Kiswahili katika mijadala**


Kamusi ya Kiswahili sanifu ya TUKI (2004), inaeleza mijadala kama mazungumzo juu ya jambo maalumu yanayofanywa kwa kutolea hoja kuhusu jambo hilo; mashindano ya maneno au mdahala. Kulingana na Vygotsky (1987), ujifunzaji wa lugha unahitaji matumizi ya lugha hiyo kila wakati. Mwanafunzi akishirikishwa kwa shughuli kama uwasilishaji wa mada fulani, kuuliza na kujibu maswali, basi mwanafunzi huyo atajifunza lugha hiyo. Wanafunzi wanapopewa fursa ya kushiriki

katika mijadala, wao hujifunza na kutumia misamiati mipya na hata kutunga miundo ya sentensi tofauti tofauti. Wanafunzi hujifunza kutoka kwa wanafunzi wengine na hata kurekebisha makosa ya sarufi.

Mtafiti aliwapa wanafunzi 560 kutoka shule saba teule hojaji ili kupata habari kuhusu siku za mijadala shuleni. Kauli iliojazwa ni, *kuna siku za mijadala shuleni mwetu*. Mtafiti alibaini kuwa, shule zote saba zina siku za mijadala kila juma. Kupitia mbinu ya uchunzaji, mtafiti pia aliweza kuhudhuria baadhi ya mijadala katika shule ya upili ili kushuhudia yale yanayotendeka.

Walimu huchangia sana kuendeleza kanuni za lugha shuleni. Kwa hivyo, mtafiti aliwauliza wanafunzi 560 ikiwa walimu huhudhuria mijadala hiyo. Kauli iliojazwa ni; *Walimu wa somo la Kiswahili huhudhuria mijadala ya shule?* Majibu ya kauli hii yaliwasilishwa kwa grafu 2.4.

**Grafu 2.4 Majibu ya wanafunzi kuhusu mijadala kwa lugha ya Kiswahili**




Kwa mujibu wa grafu 2.4, Asilimia 56.96 ya wanafunzi 560 walikubali kuwa walimu wa lugha ya Kiswahili huhudhuria mijadala kwa lugha ya Kiswahili. Hii ni ithibati tosha kuwa wengi wa walimu wa Kiswahili hushiriki katika utekelezaji wa kanuni za lugha shuleni. Utafiti pia ulibaini kuwa, walimu wanapohudhuria mijadala hii, huwasaidia sana wanafunzi. Hurekebisha makosa ya wanafunzi na hata huchangia katika mada husika. Asilimia 3.4 ya wanafunzi hawakuwa na uhakika. Wanafunzi hawa walisema kuwa, ni walimu wa zamu ambao huhudhuria mijadala ya shule. Baadhi ya walimu hawa si wa somo la Kiswahili. Asilimia 39.64 ya wanafunzi kutoka shule saba teule, walikataa kuwa walimu wao huhudhuria mijadala ya shule. Walisema kuwa, mijadala huendeshwa na wanafunzi pekee. Kwa mfano katika shule ya Upili ya Kitaifa ya Butula, mijadala hii huongozwa na wanachama wa CHAKIBU (Chama cha Kiswahili cha Butula).

Mtafiti pia alitaka kujua kutoka kwa wakuu wa idara ya Kiswahili ikiwa kulikuwa na siku ya mijadala shuleni mwao. Kauli waliojaza ni ; *Kuna siku za mijadala shuleni*. Wakuu wa idara ya Kiswahili saba walisema kuwa, kuna siku ambayo imetengwa kuendeshwa mijadala kwa lugha ya Kiswahili.

Mtafiti pia alitaka kujua kutoka kwa wakuu wa idara ikiwa walimu wa somo la Kiswahili huhudhuria mijadala kwa lugha ya Kiswahili. Kauli iliojazwa ni, *Mimi huhudhuria mijadala kwa lugha ya Kiswahili shuleni*. Kati ya wakuu wa idara saba, wakuu wa idara watano, watano wanaowakilisha asilimia 71 walikubali kuwa wao huhudhuria mijadala. Wakuu wa idara wawili wanaowakilisha asilimia 29 walikataa kauli hii kama ilivyoonyeshwa kwa chati 2.3.

### Chati 2.3 Majibu ya wakuu wa idara ya Kiswahili kuhusu mijadala ya lugha ya Kiswahili



Asilimia 29 ya wakuu wa idara ya Kiswahili walikataa kuwa huwa hawahudhuria mijadala hii. Walisema kuwa, mijadala hii huandaliwa wakati wa jioni. Huu ni wakati ambao wao huondoka kwenda nyumbani.

Utafiti pia ulibaini kuwa, ingawa kuna siku za mijada katika shule saba za utafiti, wakati mwingine walimu wa somo la Kiswahili wasipohudhuria mijadala hii, wanafunzi hujiingiza katika shughuli zingine kama kucheza kandanda, mpira wa vikapuni na hata netiboli uwanjani.

Utafiti ulibaini kuwa, wanafunzi katika shule ya upili ya Mundika, Amukura na Makunda, walisema kuwa, ni nadra kumwona mwalimu wa somo la Kiswahili akihudhuria mijadala. Kwa hivyo, ingekuwa bora walimu hawa wangehudhuria ili kuwarekebisha makosa wanayotenda wanapojadili mada. Katika shule za upili za Lwanya, Chakol na Kisoko, wanafunzi walisema kuwa, walimu wa somo la Kiswahili huhudhuria mijadala ya wanafunzi. Mijadala hii huwasaidia wanafunzi

kujibu swali la pili la insha linalohusu kujadili maswala ibuka. Kwa hivyo wao huimarisha ujuzi wao katika kujibu swali hilo

Mijadala ni kanuni mojawapo ya shule, hivyo huwapa wanafunzi fursa ya kujieleza mbele ya wanafunzi wenzao. Kwa hivyo wao huimarisha ujasiri wao wanapotumia lugha ya Kiswahili. Pia huwachochea wanafunzi kufanya utafiti zaidi ili kupata hoja za kutosha. Kulingana na Koko (2016), mijadala huchangia pakubwa katika kuimarisha uwezo wa wanafunzi katika lugha ya Kiswahili. Pia mijadala huwapa nafasi ya kuonyesha ujuzi mpya ambao wamepata au kuonyesha weledi wao kwa wengine. Kupitia njia hii, wengi hufaulu.

### **2.1.5 Shughuli za idara ya Kiswahili**

Kulingana na kamusi sanifu ya Kiswahili ya TUKI (2004), idara ni sehemu inayoshughulikia jambo fulani katika wizara, shirika au kampuni. Shughuli za idara kwa hivyo, ni hali ya idara kuhusika katika utekelezaji wa mambo mbalimbali ya idara. Katika shule teule saba za utafiti, kila shule ina idara ya Kiswahili inayosimamiwa na mwalimu wa somo la Kiswahili ambaye ni Mkuu wa idara ya Kiswahili.

Kupitia mbinu ya mahojiano na wakuu wa idara ya Kiswahili, mtafiti alibaini kuwa, hapo awali masomo ya Kiswahili na Kiingereza yalikuwa katika idara moja lakini sasa Kiswahili kimepewa hadhi ya kujisimamia kama idara. Idara hii imepewa majukumu ya kuweka mikakati ya kuimarisha somo la Kiswahili. Mikakati hii imeshirikishwa pamoja na kanuni za lugha shuleni. Kwa hivyo, ni jukumu la kila mwanafunzi kuhakikisha kuwa ameshiriki katika shughuli za idara.

Utafiti ulibaini kuwa, shughuli za idara ya Kiswahili ni pamoja na vipindi vya ziada, uandaji na uhudhuriaji wa makongamano ya ndani na nje ya shule, kusoma vitabu na magazeti kwa lugha ya Kiswahili na wanafunzi kushiriki katika vyama vya Kiswahili. Kwa hivyo, mtafiti alitaka kujua kutoka kwa walimu iwapo idara ya Kiswahili ina shughuli za aina hii kwa kuwapa hojaji wajaze. Mtafiti pia alitumia njia ya uchunzaji katika kukusanya data hii. Alitazama kumbukumbu za mikutano na ratiba ya idara ya somo la Kiswahili ya muhula. Kumbukumbu za mikutano za idara zilionesha mipangilio ya idara ya kila muhula.

Katika mahojiano na walimu wakuu wa shule za upili katika shule saba teule, mtafiti alipowauliza swali, *Eleza mikakati ambayo kama shule mumeweka ili kuimarisha somo la Kiswahili*. Majibu ya walimu wakuu yalibaini kuwepo kwa idara ya Kiswahili ambayo imeweka mikakati na shughuli mbalimbali ili kuhakikisha kuwa somo la Kiswahili limeimarika. Shughuli hizi ni kama: vipindi vya ziada, makongamano ndani na nje ya shule, kusoma magazeti na vitabu shuleni na vyama vya shule.


#### **2.1.5.1 Vipindi vya ziada**

Kulingana na sera ya wizara ya elimu, mtaala wa Kiswahili una vipindi vitano katika kidato cha kwanza na cha pili, ilihali kidato cha tatu na cha nne una vipindi sita kila wiki. Kiganya (1995) na Odeo (2007) wanasema kuwa, kati ya vipindi 43 na 45 kwa wiki kwa shule za upili, Kiingereza kimetengewa vipindi sita na Kiswahili vipindi vitano katika kidato cha kwanza na cha pili, ilhali vipindi nane kwa Kiingereza na vipindi sita kwa somo la Kiswahili kidato cha tatu na cha nne. Kutokana na sababu hii, vipindi vya ziada ni, vipindi ambavyo hufidia uchache wa vipindi vya somo la Kiswahili. Idadi ya vipindi hivi hutofautiana katika kila shule na huteuliwa na kamati

iliyopewa jukumu hilo na shule ingawa ni kinyume na sheria za wizara ya elimu. Kwa mfano katika kielelezo cha 1.4 katika shule ya upili ya Makunda inaonyesha vipindi vya ziada vya somo la Kiswahili katika kidato cha tatu.

Kauli ambayo wanafunzi walijaza kwenye hojaji ni, *Kuna vipindi vya ziada shuleni*. Wanafunzi 560 kutoka shule saba teule walijibu kauli hii namna ilivyoonyeshwa kwenye chati.


#### **Chati 2.4 Majibu ya wanafunzi kuhusu vipindi vya ziada shuleni**



Katika chati 2.4, asilimia 89 ya wanafunzi kutoka shule saba za utafiti walikubali kuwa, kuna vipindi vya ziada vya Kiswahili. Mtafiti alibaini kuwa, katika baadhi ya shule za bweni, vipindi hivi huratibiwa kuanzia saa kumi na mbili asubuhi, kisha saa moja jioni hadi saa tatu baada ya chajio. Asilimia 9 ya wanafunzi walikataa kauli hii kuwa kuna vipindi vya ziada. Asilimia 2 ya wanafunzi hawana uhakika. Wao walichagua jibu, sikubali wala sikatai kwa sababu walimu wa somo la Kiswahili huwaweka kwenye makundi kujadili badala ya kuwafundisha.

Mtafiti pia alitaka kujua kutoka kwa wakuu wa idara ya Kiswahili ikiwa kuna vipindi vya ziada shuleni mwao. Majibu ya wakuu wa idara kutoka shule saba ni kama yafuatayo kwenye chati.

### **Chati 2.5 Majibu ya wakuu wa idara ya Kiswahili kuhusu vipindi vya ziada shuleni**



Kulingana na chati 2.5, Asilimia 85.71 ya wakuu wa idara ya Kiswahili walikubali kuwa kuna vipindi vya ziada shuleni. Vipindi hivi husaidia katika kumaliza silabasi pana ya somo la Kiswahili. Asilimia 14 ya wakuu wa idara ya Kiswahili walisema kuwa hakuna vipindi vya ziada katika shule yao kwa kuwa ni kinyume na sheria za wizara ya elimu ambayo hairuhusu walimu kufunza vipindi vya ziada.

Kupitia mahojiano na wakuu wa idara ya Kiswahili, mtafiti alibaini kuwa, kwa kuwa ufundishaji wa vipindi hivi ni kinyume cha sheria ya wizara ya elimu, wakati wa vipindi hivi, wanafunzi huwekwa kwenye makundi ili kujadili maswali waliyopewa na mwalimu wa somo la Kiswahili. Hii inawapa fursa ya kuwasiliana miongoni mwao na kurekebisha makosa. Johnson na Johnson katika Richards na Rodgers (2001), wanahimiza wanafunzi kukisia makosa wanapowasiliana na waweze

kujifunza kutokana na makosa yao. Wanahimizwa kuendeleza zaidi ya kile ambacho wamefundishwa ili wawe wabunifu. Mwalimu mkuu katika shule ya Upili ya Makunda, alisema kuwa,

‘Silabasi ya somo la Kiswahili ni pana sana. Somo la Kiswahili lina karatasi tatu ambazo ni insha, sarufi na matumizi ya lugha na fasihi. Karatasi hizi ni pana na muda mwingi unahitajika iwapo silabasi ya somo la Kiswahili itaweza kukamilishwa ipasavyo. Vipindi vilivyotengewa somo la Kiswahili ni vichache na kama shule, ni lazima tuongeze vipindi vingine ili kushughulikia kila kipengele ili mtaala ukamilike wakati unaofaa.’


#### **2.1.5.2 Makongamano ya ndani na nje ya shule**

Kulingana na kamusi ya Kiswahili sanifu (2004), kongamano ni mjadala juu ya jambo fulani unaofanywa na mkusanyiko wa watu kama vile katika mkutano, warsha na kongamano la kitaifa la walimu. Kwa mujibu wa nadharia ya Richards na Rodgers (1995) ya Kijumuia na Kibinadamu, ujifunzaji ni jukumu la jumuiya ya wanafunzi pamoja na walimu. Washiriki wanafaa kujifunza kwa kutangamana na wenzao. Utafiti ulibaini kutoka kwa wakuu wa idara kuwa makongamano ya ndani na nje ni miongoni mwa shughuli za idara ya Kiswahili.

Kulingana na Koko (2016), makongamano hutokea katika viwango tofauti tofauti. Shuleni, wanafunzi wanaweza kukongamana kuanzia kiwango cha madarasa, kati ya mikondo tofauti au kati ya bweni tofauti. Makongamano haya pia yanaweza kuendeshwa kwa kualika shule zingine. Matokeo ya utafiti yalibaini kuwa, katika shule za Kaunti ya Busia, makongamano pia huandaliwa kwa viwango vivi hivi. Kuna makongamano ya ndani mwa shule, na pia kuna makongamano ya nje ya shule. Yale ambayo huandaliwa ndani ya shule, huwa baina ya wanafunzi kwa wanafunzi, ilhali ya nje huandaliwa kwa kuwaalika wanafunzi kutoka shule jirani ili

kujadiliana kuhusu mada mbalimbali. Mtafiti aliwapa wanafunzi 560 kutoka shule saba za utafiti hojaji ili kupata habari ikiwa wana makongamano ya ndani ya shule yao. Kauli iliyojazwa ni, *Shule yetu huandaa makongamano ya ndani ya shule*. Majibu ya kauli hili yamewasilishwa kwa chati.

### Chati 2.6 Majibu ya wanafunzi kuhusu makongamano ya ndani ya shule




Kwa mujibu wa chati 2.6, jumla ya wanafunzi 560 kutoka shule saba za utafiti katika Kaunti ya Busia walijaza hojaji. Asilimia 71 ya wanafunzi walikubali kuwa wana makongamano ya ndani mwa shule. Asilimia 23 ya wanafunzi walikataa na asilimia 6 ya wanafunzi hawana uhakika.

Katika shule ya upili ya wasichana ya Kisoko, lugha ya mawasiliano ni Kiingereza pekee. Wanafunzi hawaruhusiwi kuzungumza kwa lugha ya Kiswahili. Ili kufidia upungufu huu, wametenga siku moja kila muhula inayojulikana kama “*Siku ya Kiswahili*’. Wanafunzi na walimu wa somo la Kiswahili hujumuika pamoja. Shughuli za siku hii huratibiwa na hujumlisha, kuwasiliana kwa lugha sanifu ya Kiswahili, mijadala na midahalo, kufanya mitihani katika somo la Kiswahili na

maswali katika vikundi. Siku hii pia huwapa wanafunzi fursa ya kutangamana na walimu wao kwa ajili ya kurekebisha makosa. Munialo (2010) anasema kuwa, shughuli kama siku ya Kiswahili, huwapa wanafunzi fursa ya kuingiliana na wenzao hivyo kuongeza hatua katika upataji lugha. Siku za Kiswahili pia huwapa wanafunzi fursa ya kuwasiliana siku nzima kwa lugha ya Kiswahili. Hii husaidia wanafunzi hasa wale ambao wana siku chache za kuzungumza Kiswahili kuimarisha ujuzi wao katika lugha hii. Siku hii huongeza mwingiliano kati ya wanafunzi walio na umilisi wa chini katika lugha ya Kiswahili na wale ambao umilisi wao ni wa juu. Aidha siku hii, walimu wa Kiswahili huwa shuleni, hivyo kuwarekebisha wanafunzi wanapokosea wanapowasiliana kwa lugha ya Kiswahili.

Matokeo ya utafiti pia yalionyesha kuwa, Shule za Upili za Butula, Lwanya, Chakol na Mundika huandaa makongamano ya ndani ya shule. Shughuli za siku hii hulenga kuimarisha somo la Kiswahili. Katika shule ya Upili ya Amukura na Makunda, utafiti ulibaini kuwa hawana makongamano ya ndani ya shule. Mtafiti pia alitaka kujua kutoka kwa wakuu wa idara ya Kiswahili ikiwa wana makongamano ya ndani mwa shule. Kauli waliojaza kupitia hojaji ni, *Shule yetu huandaa makongamano ya ndani mwa shule*. Majibu ya kauli hii yaliwasilishwa kwa chati.


**Chati 2.7 Majibu ya wakuu wa idara ya Kiswahili kuhusu maandalizi ya makongamano ya ndani mwa shule**



Katika chati 2.7, Asilimia 71 ya wakuu wa idara ya Kiswahili kutoka shule saba za utafiti walikubali kuwa huandaa makongamano ndani ya shule kama njia mojawapo ya kutekeleza kanuni za lugha za shule. Asilimia 29 ya wakuu wa idara ya Kiswahili walikataa kuwa hawana makongamano ya lugha ya Kiswahili shuleni mwao. Hii ni kwa sababu, makongamano haya huhitaji ufadhili kutoka kwa uongozi wa shule. Shule hizi hukosa hela ya kuendesha shughuli za aina hii.

Mtafiti pia alitaka kujua ikiwa shule teule saba hushiriki katika makongamano ya nje. Kauli aliyouliza mtafiti ni, *Shule yetu hushiriki katika kongamano la nje ya shule*. Majibu ya wanafunzi 560 kutoka shule saba yaliwasilishwa kwa chati ifuatayo :


## Chati 2.8 Majibu ya wanafunzi kuhusu makongamano ya nje ya shule



Kwa mujibu wa chati 2.8, asilimia 75 ya wanafunzi kutoka shule teule saba huhudhuria makongamano ya nje yanayoandaliwa katika shule zingine. Asilimia 18 ya wanafunzi walisema kuwa wao huwa hawahudhuri makongamano ya nje ya shule. Asilimia 7 ya wanafunzi hawakukubali wala kukataa. Wanafunzi hawa walisema kuwa, ingawa kuna makongamano ya nje ya shule, wanafunzi wanaohudhuria makongamano haya ni wale wanaofanya vyema katika somo la Kiswahili. Wanafunzi hawa huteuliwa ili kuwakilisha shule katika mashindano ambayo huandaliwa nje ya shule.

Mtafiti pia aliwapa wakuu wa idara ya Kiswahili saba hojaji ili kupata habari kuhusu uhudhuriaji wa kongamano nje ya shule, kauli aliyowauliza wakuu wa idara ya Kiswahili ni, *Shule yetu huhudhuria kongamano la nje ya shule*. Majibu ya kauli hili yamewasilishwa kwa chati.

## Chati 2.9 Majibu ya wakuu wa idara ya Kiswahili kuhusu makongamano ya nje ya shule



Kulingana na chati 2.9, asilimia 57 ya wakuu wa idara ya Kiswahili walikubali kuwa wao huhudhuria makongamano ya nje ya shule. Asilimia 43 ya wakuu wa idara ya Kiswahili walisema kuwa, huwa hawahudhurii makongamano ya nje ya shule.

Wakuu wa idara ambao walikubali kuwa wao huhudhuria, walisema kuwa, makongamano haya huwapa fursa ya kutangamana na walimu wengine wa somo la Kiswahili. Kupitia njia hii, wao hubadilishana mawazo kuhusu vipengele tata katika somo la Kiswahili. Kando na kuwafaidi walimu, wanafunzi pia hukuza ujuzi wao katika somo la Kiswahili. Katika utafiti wa Ouma (2015), anasema kuwa, wanafunzi wanaposhirikiana katika makongamano haya, hukuza vipaji vyao na huwasaidia kunoa ujuzi wao katika mazungumzo na uandishi katika somo la Kiswahili.

Utafiti pia uligundua kuwa, kando na makongamano ya nje yanayoshirikisha wanafunzi, kuna warsha za walimu wa Kiswahili kila muhula. Ouma (2015) anasema kuwa warsha hizi ni muhimu kwa kuwa walimu hupata mbinu mpya za kusoma na kufunza. Habari ambazo walimu hupata katika warsha hizi zinahusu mitindo mipya ya utahini na usahihishaji wa mitihani ya Kitaifa. Mwalimu pia hupata vitabu vipya vya kiada au vya kutahiniwa, hivyo huimarisha ujuzi wa mwalimu huyo katika utahini na usahihishaji. (Tazama kielelezo 1.5). Asilimia 43 ya wakuu wa idara ambao huwa hawahudhuri makongamano ya nje na warsha za aina hii, hutokana na ukosefu wa ufadhili kutoka uongozi wa shule au wizara ya elimu. Walimu hawa walisema kuwa, ingekuwa vyema ikiwa wizara ya elimu ingeweza kuandaa na kufadhili warsha za aina hii ili walimu wote waweze kufaidika.


Katika nadharia ya kijumuia na kibinadamu, kutomakinika kwa wanafunzi kunaweza kupunguzwa kwa kuwapa majukumu tofauti katika ufundishaji. Makongamano ya ndani na nje ya shule hutoa ujifunzaji kutoka kwa utegemezi wa vitabu. Mhimili wa tatu unasema kuwa, wanafunzi wanafaa kujifunza lugha kwa njia mbalimbali kwa hivyo badala ya kusoma kuhusu tukio kama mijadala kwenye vitabu, wanafunzi wanaweza kushiriki katika mijadala itakayowachangamsha wanapohudhuria makongamano ya nje.

### **2.1.5.3 Kusoma vitabu na magazeti ya Kiswahili**

Kulingana na Kamusi ya Karne ya 21 (2019), gazeti ni mkusanyiko wa karatasi zilizochapwa ndani yake mkiwa na habari, Makala na matangazo yanayotolewa kwa kipindi maalumu kama vile kila siku, kila wiki au kila mwezi. Gazeti la Taifa leo ndilo gazeti la kipekee ambalo lina utambulisho mkubwa nchini Kenya na limeandikwa kwa lugha ya Kiswahili. Ni gazeti ambalo hununuliwa katika shule

nyingi nchini Kenya. Kwa hivyo, kupitia hojaji za wanafunzi na wakuu wa idara ya Kiswahili, mtafiti alitaka kujua ikiwa usomaji wa magazeti na vitabu katika lugha ya Kiswahili ni mojawapo ya shughuli za idara ya Kiswahili. Kauli waliojibu wanafunzi 560 kutoka shule teule saba kaunti ya Busia ni, *Sisi husoma vitabu na magazeti shuleni mwetu*. Majibu ya kauli hii yalipangwa kwenye chati.

**Chati 2.10 Majibu ya wanafunzi kuhusu usomaji wa vitabu na magazeti shuleni**




Katika chati 2.10, asilimia 57 ya wanafunzi walikubali kuwa wao husoma vitabu na magazeti wakiwa shuleni. Asilimia 14 hawakuonyesha msimamo wowote. Asilimia 29 ya wanafunzi kutoka shule hizi walikataa kuwa wao husoma gazeti wakiwa shuleni. Katika shule ya upili ya Chakol na Butula, wanafunzi husoma vitabu na magazeti kwa lugha ya Kiswahili siku ya Jumamosi na Jumapili mtawalia. Katika shule ya Upili ya wasichana ya Lwanya na Kisoko, mtafiti alipata habari kuwa, kati ya vipindi vya somo la Kiswahili, kipindi kimoja huwa kimetengwa kwa minajili ya kusoma vitabu vya Kiswahili au magazeti kwenye maktaba. Mwanafunzi anayepatikana akifanya shughuli nyingine kando na kusoma magazeti au vitabu vya

hadithi wakati huu huadhibiwa. Wanafunzi ambao hawakuonyesha msimamo wowote, walisema kuwa, magazeti ambayo wao husoma ni ya lugha ya Kiingereza na sio ya Kiswahili kwa kuwa ni ya Kiingereza tu hununuliwa. Asilimia 29 ya wanafunzi waliojibu kuwa hawasomi magazeti au vitabu walisema kuwa, hawajawahi kununuliwa gazeti la Kiswahili hivyo hakuna gazeti la kusoma.

Mtafiti pia alitaka kujua kutoka kwa wakuu wa idara saba kutoka shule saba ikiwa wanafunzi wao husoma vitabu na magazeti ya Kiswahili shuleni mwao. Kauli iliyojibiwa na wakuu wa idara ni, *Wanafunzi husoma vitabu na magazeti shuleni*. Majibu ya kauli hii yaliwasilishwa kwa chati.

**Chati 2.11 Majibu ya wakuu wa idara ya Kiswahili kuhusu usomaji wa vitabu na magazeti shuleni**



Asilimia 71 ya wakuu wa idara ya Kiswahili walikubali kuwa wanafunzi husoma vitabu na magazeti ya Kiswahili wakiwa shuleni. Asilimia 29 ya wakuu wa idara ya Kiswahili kutoka shule saba za utafiti Kaunti ya Busia walikataa kuwa wanafunzi husoma vitabu na magazeti wakiwa shuleni.


Haugen (1983), anasema kuwa, lugha inafaa kufunzwa, kufafanuliwa kwa undani na kutekelezwa katika shule. Njia ya utekelezaji wa sera za lugha inatokana na taasisi zinazochapisha magazeti, vitabu vya kiada na machapisho mengine. Robin (1973) anaunga kauli hii kwa kusema kuwa, matumizi ya lugha katika vyombo vya habari na machapisho ya makala hukuza kiwango cha wanafunzi katika kupata ujuzi. Ujuzi wa lugha ni kama njia mojawapo ya kutekeleza sera za lugha. Kwa mujibu wa Muruguru (2000), kuna uhusiano mkubwa kati ya uwepo wa vitabu ambavyo ni vyanzo muhimu katika ufundishaji na utendaji katika somo la lugha. Shule zenye vitabu vya kiada na ziada vya kutosha hupata matokeo mazuri kuliko zile zisizo na vitabu vya kutosha.

Kutokana na matokeo ya utafiti, swala la uwepo wa vitabu vya kusoma vya Kiswahili na magazeti ni muhimu ili kukuza ujuzi wa wanafunzi katika lugha.

#### **2.1.5.4 Vyama vya Kiswahili**

Kulingana na kamusi ya Kiswahili sanifu (2004), chama ni kikundi cha watu walioungana pamoja kwa lengo la kutekeleza matakwa yao ya kisiasa, kiuchumi au kijamii. Koko (2016) anasema kuwa, vyama vya Kiswahili huhakikisha kuwa lugha sanifu inatumiwa shuleni. Husaidia walimu kupiga marufuku uzungumzi wa sheng', kuandaa mijadala na makongamano ya ndani na nje ya shule. Ili kupata habari ikiwa shule za utafiti saba katika Kaunti ya Busia zina vyama vya Kiswahili, mtafiti kupitia hojaji aliwauliza wanafunzi 560 kutoka shule zote saba kauli ifuatayo, *Kuna vyama vya Kiswahili shuleni mwenu*. Majibu ya swali hili yameonyeshwa kwa chati.

### Chati 2.12 Majibu ya wanafunzi kuhusu uwepo wa vyama vya Kiswahili shuleni



Katika chati 2.12, asilimia 81 ya wanafunzi walikubali kuwa kuna vyama vya Kiswahili shuleni mwao. Kwa mfano, katika shule ya upili ya Kitaifa ya Butula, ilibainika kuwa kuna Chama cha Kiswahili kinachoitwa CHAKIBU (Chama Cha Kiswahili cha Butula). Chama hiki hushughulika na utunzi wa mashairi, kuandaa mijadala na kuhakikisha kuwa wanafunzi wanawasiliana kwa lugha sanifu ya Kiswahili siku ya Kiswahili. Utafiti pia ulibaini kuwa chama cha wanahabari kinapatikana katika shule zote saba za upili zilizoteuliwa kwa utafiti Kaunti ya Busia. Chama cha wanahabari kina jukumu la kukusanya matukio yanayotendeka shuleni kisha kuyawasilisha kwenye gwaride kwa lugha sanifu ya Kiswahili. Mtafiti aligundua kuwa, kabla ya wanafunzi kutoa habari kwenye gwaride, mwalimu wa somo la Kiswahili hurekebisha baadhi ya makosa katika uandishi wao. Habari hizi huwasilishwa siku ya Ijumaa kwa shule ya upili ya Butula, Lwanya, Chakol na Makunda.

Matokeo ya utafiti huu yaliwiana na yale ya Nyakeoga (2018). Mtafiti huyu anasema kuwa, katika kanuni za lugha za shule, vyama vya wanahabari ni kati ya kanuni za lugha. Vyama hivi huwaandaa wanafunzi katika upataji wa ujuzi katika mawasiliano yao kwa lugha sanifu shuleni. Pia hulea talanta za wanafunzi wanaotaka kuwa wasomaji na waandishi wa habari siku zijazo.

Asilimia 9.64 ya wanafunzi hawakuwa na msimamo katika swali hili. Wanafunzi hawa walisema kuwa, ingawa kuna vyama vya Kiswahili na Uanahabari, huwa havina mikutano. Kwa mfano mwanafunzi mmoja katika shule ya upili ya Makunda alisema kuwa ;

‘Nilipojiunga na shule hii katika kidato cha kwanza, nilijiunga na kikundi cha wanahabari kwa kuwa ni ndoto yangu kuwa mwanahabari. Niko kidato cha tatu lakini sisi hukutana tu kukiwa na ziara ya kwenda shule ya nje, pia ni nadra sana kuona wanafunzi wakihudhuria shughuli za vyama hivi siku za shule’.

Asilimia 9.64 ya wanafunzi walisema kuwa hakuna vyama vya Kiswahili shuleni mwao ila chama cha Wanahabari kinachoshughulikia maswala ya somo la Kiingereza na Kiswahili. Kutokana na utafiti, vyama vya Kiswahili ni muhimu katika kuimarisha lugha ya Kiswahili. Vyama hivi huwapa wanafunzi fursa ya kuwasiliana na kujieleza katika lugha ya Kiswahili hivyo kuimarisha ujuzi wao katika lugha hii.

Matokeo ya utafiti huu kupitia mbinu ya mahojiano na wakuu wa idara yalionyesha kuwa, shule za upili katika Kaunti ya Busia, hutilia sana mkazo stadi ya kusoma na kuandika kwani ndizo hutahiniwa kwenye mtihani wa KCSE. Baada ya hapo, wanafunzi hawa husahau lugha ya Kiswahili. Utafiti ulionelea kuwa ingekuwa

vyema, ikiwa walimu wa somo la Kiswahili wangetilia mkazo stadi zote nne za lugha, kusoma, kuandika, kusikiliza na kuongea ili baada ya kufanya mtihani, wanafunzi wanaopata alama nzuri katika mtihani wa mwisho wawe na ujuzi wa kuzungumza lugha ya Kiswahili sanifu. Hii inawezekana tu ikiwa kanuni za lugha za shule zilizojadiliwa zitatekelezwa.

## **2.2 Hitimisho**

Katika sura hii, utafiti ulilenga kubainisha kanuni za lugha katika shule za upili. Utafiti ulibaini kuwa, shule tofauti zina sheria za lugha tofauti. Sheria hizi ni kama siku ya Kiswahili, maandishi katika mabango, mijadala, na shughuli za idara. Shughuli hizi za idara zinajumuisha vipindi vya ziada, vyama vya Kiswahili, usomaji wa vitabu na magazeti na nyinginezo. Utafiti pia ulibaini kuwa, sababu kuu ya uteuzi wa kanuni za lugha shuleni ni kuimarisha somo la Kiswahili na kufanya wanafunzi wawe na mielekeo chanya kuhusu lugha ya Kiswahili. Mihimili ya nadharia ya Kijumuia na Kibinadamu ilifaa katika kueleza kanuni za lugha shuleni.

Utafiti pia ulibaini kuwa, ingawa kila shule ina sheria za lugha tofauti, utekelezaji wake hasa lugha ya mawasiliano unategemea viwango vya shule. Katika shule za bweni, ni rahisi kwa wanafunzi hawa kuwasiliana kwa lugha ya Kiswahili kwa kuwa wanatoka sehemu tofauti za nchi. Lugha ambayo huwaunga pamoja ni Kiswahili. Pia kuna walimu wanaoishi shuleni, hivyo shughuli za idara kama mijadala zinakuwa rahisi kutekelezwa bila kuhofia muda ambao mijadala huchukua. Wanafunzi katika shule za kutwa wanapofika nyumbani, wao huwasiliana na wanakijiji kwa lugha ya kiasili. Pale hakuna mwalimu wa kuhakikisha kuwa lugha ya mawasiliano ni Kiswahili. Mtafiti pia aligundua kuwa, ili kanuni hizi ziweze

kutekelezwa, zinahitaji ufadhili kutoka kwa shule au wizara ya elimu hasa warsha ya walimu wa Kiswahili na makongamano ya ndani na nje ya shule kwa wanafunzi. Ni shule tu za Kitaifa na Zaidi ya Kaunti ambazo zina uwezo wa kutoa ufadhili kwa walimu na wanafunzi. Kwa hivyo, ingawa kila shule ina kanuni za lugha za shule katika ratiba na kumbukumbu za mikutano ya idara, kanuni hizi zimebakia tu kwenye maandishi bila kutekelezwa na baadhi ya shule za upili. Sura inayofuata imechanganua mielekeo ya wanafunzi na walimu kuhusu kanuni za lugha shuleni.

## **SURA YA TATU**

### **MIELEKEO YA WANAFUNZI NA WALIMU KUHUSU KANUNI ZA**

#### **LUGHA SHULENI**

#### **3.0 Utangulizi**

Sura iliyotangulia ilianguzia kanuni za lugha shuleni katika shule za upili katika Kaunti ya Busia. Kanuni za lugha mbalimbali zilijitokeza. Katika sura hii, mielekeo ya walimu na wanafunzi kuhusu kanuni za lugha shuleni katika Kaunti ya Busia, nchini Kenya ilichunguzwa. Mielekeo hii ilipimwa kwa kutumia mbinu tatu za utafiti ambazo ni hojaji likati kwa wanafunzi na walimu ambao ni wakuu wa idara ya Kiswahili, majadiliano elekezi yenye kauli 14 kwa wanafunzi, na maswali 14 ya mahojiano kwa wakuu wa idara ya Kiswahili. Maswali haya yalimsaidia mtafiti kuibua habari muhimu kuhusiana na mielekeo tofauti kuhusu kanuni za lugha katika shule za upili. Hojaji hizi zilipewa wanafunzi na walimu ambao walijaza kwa lugha ya Kiswahili. Aidha, mtafiti alirejelea mihimili ya nadharia ya vitendo vilivyofikiriwa ya Ajzen na Fishbein (1980) ili kupima mielekeo ya walimu na wanafunzi wa shule za upili kuhusu kanuni za lugha za shule. Katika nadharia hii, ikiwa binadamu anafanya jambo ambalo litamnufaisha, huwa na mtazamo kubalifu kuhusu jambo hilo. Ikiwa halitakuwa na manufaa kwake, huwa na msimamo usiokubalifu. Swali ambalo binadamu hujiuliza kila wakati ni kwa namna gani atakavyofaidika na tendo kubalifu? Nadharia hii ilisaidia katika utafiti kueleza tabia na mielekeo ya walimu na wanafunzi wa shule za upili kuhusu kanuni za lugha shuleni. Kanuni za lugha za shule ilivyoielezwa katika sura iliyotangulia ni ; Lugha ya mawasiliano katika mazingira ya shule, Siku za Kiswahili, Mabango na

maandishi katika mazingira ya shule, Matumizi ya lugha ya Kiswahili katika mijadala, Shughuli za idara ambazo ni ; vipindi vya ziada, makongamano ndani na nje ya shule, usomaji wa vitabu na magazeti na vyama vya Kiswahili.

### **3.1 Uchanganuzi wa mielekeo ya wanafunzi kuhusu kanuni za lugha shuleni**

Katika sehemu hii, matokeo ya uchanganuzi wa hojaji likati yalionyeshwa kwa kurejelea kauli 15 ambazo zililenga kubainisha mielekeo ya wanafunzi kuhusu kanuni za lugha za shule. Kauli hizi zote zilikuwa na majibu ya kuchagua matano ambayo yalikuwa: Nakubali kabisa, nakubali, sikubali wala sikatai, nakataa na nakataa kabisa. Nakubali kabisa na nakubali ilionyesha mielekeo chanya ilhali nakataa na nakataa kabisa ilionyesha mielekeo hasi. Matokeo ya utafiti yaliwasilishwa kwa majedwali ifuatavyo.

#### **3.1.1 Lugha ya mawasiliano katika mazingira ya shule**

Misiko (2008), anasema kuwa, lugha ni muhimu katika mawasiliano ya binadamu kwani ni chombo cha kupasha habari na kuwasiliana. Lugha ya mawasiliano kwa hivyo, ni lugha iliyoteuliwa katika mazingira ya shule ili itumike na wanafunzi kupitisha ujumbe au habari kwa njia ya maandishi au mazungumzo. Kwa mujibu wa Katiba ya Kenya (2010), Kiswahili na Kiingereza ni lugha rasmi na hutumika katika mazingira rasmi ya kielimu. Kwa mfano katika shule saba zilizoteuliwa katika utafiti huu. Matumizi ya lugha ya kiasili na sheng' haziruhusiwi katika mazingira rasmi ya shule. Utafiti huu ulitambua lugha waipendao wanafunzi katika mawasiliano ya shule. Mtafiti pia aliwapa swali katika mjadala elekezi wa makundi, *Eleza manufaa ya kuzungumza kwa lugha ya Kiswahili na wenzako*. Majibu ya makundi ya wanafunzi na kauli kutoka kwenye hojaji likati yalimwezesha mtafiti kubaini

mielekeo ya wanafunzi kuhusu lugha ya mawasiliano katika mazingira ya shule.

Kauli aliyowauliza wanafunzi ni;

**Jedwali 3.1 Mimi huzungumza kwa lugha ya Kiswahili na wenzangu nikiwa shuleni**

| Shule        | Mimi huzungumza na wenzangu lugha ya Kiswahili nikiwa shuleni | Nakubali kabisa | Nakubali      | Sikubali wala sikatai | Nakataa    | Nakataa kabisa |
|--------------|---|-----------------|---------------|-----------------------|------------|----------------|
| Butula       | Idadi   | 23              | 37            | 11                    | 05         | 04             |
|              | Asilimia  | 28.75%          | 46.25%        | 13.75%                | 6.25%      | 5%             |
| Mundika      | Idadi   | 27              | 42            | 08                    | 02         | 01             |
|              | Asilimia  | 33.75%          | 52.5%         | 10%                   | 2.5%       | 1.25%          |
| Amukura      | Idadi   | 32              | 24            | 17                    | 04         | 03             |
|              | Asilimia  | 40%             | 30%           | 21.25%                | 5%         | 3.75%          |
| Kisoko       | Idadi   | 13              | 14            | 13                    | 35         | 05             |
|              | Asilimia  | 16.25%          | 17.5%         | 16.25%                | 43.75%     | 6.25%          |
| Chakol       | Idadi   | 44              | 20            | 08                    | 06         | 02             |
|              | Asilimia  | 55%             | 25%           | 10%                   | 7.5%       | 2.5%           |
| Lwanya       | Idadi   | 43              | 26            | 04                    | 03         | 04             |
|              | Asilimia  | 53.75%          | 32.5%         | 5%                    | 3.75%      | 5%             |
| Makunda      | Idadi   | 46              | 23            | 07                    | 01         | 03             |
|              | Asilimia  | 57.5%           | 28.75%        | 8.75%                 | 1.25%      | 3.75%          |
| <b>Jumla</b> | <b>Idadi</b>  | <b>228</b>      | <b>186</b>    | <b>68</b>             | <b>56</b>  | <b>22</b>      |
|              | <b>Asilimia</b>   | <b>40.71%</b>   | <b>32.21%</b> | <b>12.14%</b>         | <b>10%</b> | <b>3.91%</b>   |

Katika shule za upili zilizofanyiwa utafiti, wanafunzi 560 walijaza hojaji likati.

Asilimia 72.92 ya wanafunzi walikubali kuwa wanapenda kuzungumza kwa lugha

ya Kiswahili shuleni na wenzao hivyo wana mwelekeo chanya wa kuwasiliana kwa

lugha ya Kiswahili. Manufaa ya kuwasiliana kwa lugha ya Kiswahili na wenzako ni

kuwa hurahisisha mawasiliano hasa kati ya wanafunzi wanaotoka sehemu tofauti za

nchi. Asilimia 12.14 hawakuonyesha mwelekeo wowote. Asilimia 13.91 ya

wanafunzi hawapendi kuzungumza kwa lugha ya Kiswahili, hivyo wana mwelekeo

hasi dhidi ya matumizi ya lugha ya Kiswahili wanapowasiliana. Wanafunzi hawa

walisema kuwa, lugha ya Kiswahili ni kigumu na kina upungufu wa msamiati. Pia walisema kuwa, sheria za shule haziharuhusu kuwasiliana kwa lugha ya Kiswahili. Maoni haya yanafanana na ya Ndung'u (2014) ambaye aligundua kuwa, katika sekta ya elimu, wakuu wa shule huweka sheria ambazo zinabana matumizi ya lugha ya Kiswahili, licha ya kuwa Kiswahili ni somo la lazima na kutahiniwa hivyo kuchangia mielekeo hasi. Hali hii pia imeshuhudiwa katika shule za Upili za Kisoko na Mundika katika kaunti ya Busia. Katika shule hizi, mawasiliano kwa lugha ya Kiswahili yamepigwa marufuku, hivyo sheria hii imefanya mwelekeo wao kuhusu mawasiliano kwa lugha ya Kiswahili kuwa hasi.

Matokeo ya utafiti katika shule hizi pia yalibaini kuwa, mielekeo hasi kuhusu lugha ya Kiswahili yanatokana na lugha hii kuhusishwa na watu ambao si wasomi. Hii mielekeo imekuwepo tangu ukoloni ambapo lugha ya Kiingereza ilichukuliwa kama lugha ya wasomi. Chiraghdin na Mnyapala (1977) wanasema kuwa, mielekeo hasi ya Wakenya inatokana na athari ya ukoloni. Lugha ya Kiingereza inahusishwa na tabaka la wasomi. Kiingereza kinachukuliwa kama daraja ya kujiinua kiuchumi na kupata elimu.

Ingawa majibu ya wanafunzi katika shule ya Upili ya Makunda yanaonyesha kuwa wanapenda kuwasiliana kwa lugha ya Kiswahili, mtafiti aligundua kuwa, kuna baadhi ya wanafunzi ambao huzungumza lugha za kienyeji au asili wakati wa mapumziko. Hivyo kuonyesha kuwa kando na lugha ya Kiingereza na Kiswahili, kuna wanafunzi katika shule za kutwa ambao wanapenda lugha za kienyeji au asili.

Ili kuibua habari zaidi kuhusu mwelekeo wa wanafunzi kuhusu lugha ya mawasiliano wakiwa shuleni, mtafiti aliwauliza swali lifuatalo;

**Jedwali 3.2 Napenda Kiswahili kizungumzwe kila siku shuleni**

| Shule        | Napenda Kiswahili kizungumzwe kila siku na wanafunzi shuleni | Nakubali kabisa | Nakubali      | Sikubali wala sikatai | Nakataa      | Nakataa kabisa |
|--------------|--|-----------------|---------------|-----------------------|--------------|----------------|
| Butula       | Idadi  | 43              | 21            | 02                    | 11           | 03             |
|              | Asilimia   | 53.75%          | 26.25%        | 2.5%                  | 13.75%       | 3.75%          |
| Mundika      | Idadi  | 38              | 26            | 07                    | 03           | 06             |
|              | Asilimia   | 47.5%           | 32.5%         | 8.75%                 | 3.75%        | 7.5%           |
| Amukura      | Idadi  | 39              | 23            | 16                    | 02           | 00             |
|              | Asilimia   | 48.75%          | 28.75%        | 20%                   | 2.5%         | 00%            |
| Kisoko       | Idadi  | 46              | 18            | 01                    | 07           | 08             |
|              | Asilimia   | 57.5%           | 22.5%         | 1.25%                 | 8.75%        | 10%            |
| Chakol       | Idadi  | 47              | 14            | 05                    | 06           | 08             |
|              | Asilimia   | 58.75%          | 17.5%         | 6.25%                 | 7.5%         | 10%            |
| Lwanya       | Idadi  | 43              | 11            | 04                    | 13           | 09             |
|              | Asilimia   | 53.75%          | 13.75%        | 5%                    | 16.25%       | 11.25%         |
| Makunda      | Idadi  | 43              | 14            | 09                    | 11           | 03             |
|              | Asilimia   | 53.75%          | 17.5%         | 11.25%                | 13.75%       | 3.75%          |
| <b>Jumla</b> | <b>Idadi</b>   | <b>299</b>      | <b>127</b>    | <b>44</b>             | <b>53</b>    | <b>37</b>      |
|              | <b>Asilimia</b>  | <b>53.39%</b>   | <b>22.68%</b> | <b>7.86%</b>          | <b>9.46%</b> | <b>6.61%</b>   |

Matokeo ya utafiti katika jedwali 3.2 yalidhihirisha kuwa asilimia 76.07 ya wanafunzi wana mielekeo chanya kuhusu lugha Kiswahili. Wanataka Kiswahili kizungumzwe kila siku shuleni. Wanafunzi hawa huionea lugha ya Kiswahili fahari wanapowasiliana. Wanafunzi hawa walisema kuwa, wao hueleweka vema wanapowasiliana kwa lugha ya Kiswahili. Asilimia 7.86 ya wanafunzi hawakuonyesha mwelekeo wowote. Asilimia 16.07 walikuwa na mielekeo hasi kuhusu mawasiliano kwa lugha ya Kiswahili kila siku. Wao walisema kuwa, ni somo la pekee ambalo hutahiniwa kwa lugha ya Kiswahili. Kwa hivyo, wakizungumza Kiswahili kila siku watasahau lugha ya Kiingereza. Aidha, walisema kuwa, baadhi

ya wanafunzi wanaporuhusiwa kuzungumza lugha ya Kiswahili, wao huzungumza sheng hasa wanapokosa misamiati mwafaka ya kurejelea wanachotaka kusema.

Katika shule teule za utafiti, wanafunzi walikiri kuwa, kanuni za lugha za shule zimepuuza mawasiliano katika lugha ya Kiswahili. Unapata shule nyingi zimekipa Kiingereza kipaumbele kwa kupewa siku nyingi ikilinganishwa na Kiswahili hivyo kufanya mielekeo yao kuhusu lugha ya Kiswahili kuwa hasi.

Katika nadharia ya vitendo vilivyofikirika ya Ajzen na Fishbein (1980), mwelekeo wa binadamu hutokana na manufaa ya jambo analotenda. Katika utafiti huu, mtafiti alitaka kujua ikiwa kuwasiliana kwa lugha ya Kiswahili kuna manufaa kwa mwanafunzi. Swali alilouliza ni;

**Jedwali 3.3 Kuwasiliana kwa lugha ya Kiswahili kuna manufaa katika somo la Kiswahili**

| Shule        | Kuwasiliana kwa lugha ya Kiswahili kuna manufaa katika somo la Kiswahili | Nakubali kabisa | Nakubali      | Sikubali wala sikatai | Nakataa      | Nakataa kabisa |
|--------------|--|-----------------|---------------|-----------------------|--------------|----------------|
| Butula       | Idadi  | 31              | 28            | 04                    | 11           | 06             |
|              | Asilimia   | 38.75%          | 35%           | 5%                    | 13.75%       | 7.5%           |
| Mundika      | Idadi  | 27              | 16            | 14                    | 12           | 11             |
|              | Asilimia   | 33.75%          | 20%           | 17.5%                 | 15%          | 13.75%         |
| Amukura      | Idadi  | 38              | 31            | 03                    | 07           | 01             |
|              | Asilimia   | 47.5%           | 38.75%        | 3.75%                 | 8.75%        | 1.25%          |
| Kisoko       | Idadi  | 16              | 43            | 06                    | 09           | 06             |
|              | Asilimia   | 20%             | 53.75%        | 7.5%                  | 11.25%       | 7.5%           |
| Chakol       | Idadi  | 53              | 21            | 01                    | 02           | 03             |
|              | Asilimia   | 66.25%          | 26.25%        | 1.25%                 | 2.5%         | 3.75%          |
| Lwanya       | Idadi  | 42              | 24            | 05                    | 08           | 01             |
|              | Asilimia   | 52.5%           | 30%           | 6.25%                 | 10%          | 1.25%          |
| Makunda      | Idadi  | 41              | 32            | 04                    | 01           | 02             |
|              | Asilimia   | 51.25%          | 40%           | 5%                    | 1.25%        | 2.5%           |
| <b>Jumla</b> | <b>Idadi</b>   | <b>248</b>      | <b>195</b>    | <b>37</b>             | <b>50</b>    | <b>30</b>      |
|              | <b>Asilimia</b>  | <b>44.28%</b>   | <b>34.82%</b> | <b>6.61%</b>          | <b>8.93%</b> | <b>5.36%</b>   |

Kwa mujibu wa jedwali 3.3, Asilimia 79.1 ya wanafunzi wanakubaliana kuwa, kuwasiliana kwa lugha ya Kiswahili kumewasaidia katika kuimarisha somo la Kiswahili. Hii imechangia wao kuwa na mielekeo chanya kuhusu kanuni za lugha ambazo zinawaruhusu kuzungumza kwa lugha ya Kiswahili. Asilimia 6.61 ya wanafunzi hawana uhakika ikiwa kuna uhusiano kati ya mawasiliano kwa lugha ya Kiswahili na somo la Kiswahili. Hivyo hawakuonyesha mwelekeo wowote. Asilimia 14.29 ya wanafunzi wanasema kuwa, hakuna uhusiano kati ya kuzungumza lugha ya Kiswahili na yale wanayojifunza katika somo la Kiswahili. Hivyo wana mielekeo hasi kuhusu kanuni zinazowaruhusu kuzungumza lugha ya Kiswahili. Pia wanasema kuwa, badala ya wanafunzi kuzungumza lugha sanifu ya Kiswahili, wao huzungumza sheng'. Sheng' hujitokeza katika katika uandishi wao wa insha hivyo kuchangia wao kutofanya vyema katika somo la Kiswahili. Kulingana na utafiti wa Ogolla (1990), katika mazingira ya nyumbani au yasio rasmi, lugha ya kiasili husisitizwa sana. Wanafunzi wanapoenda nyumbani au kwenye bweni wakati wa jioni, hujipata katika mazingira yasio rasmi, hivyo huwa huru kutumia lugha wanayoipenda. Mazingira haya hayana walimu wa kuhakikisha kuwa kanuni za lugha za shule zinazingatiwa. Kwa hivyo, mtafiti alitaka kujua mielekeo ya wanafunzi kuhusu lugha ya mawasiliano wanapojipata katika mazingira haya. Kupitia mjadala elekezi wa vikundi. Swali alilowauliza wanafunzi ni, *Eleza sababu za kutumia lugha ya Kiswahili ukiwa nyumbani na bweni*. Majibu ya swali hili pamoja na kauli ifuatayo ilitubainishia mielekeo ya wanafunzi.

**Jedwali 3.4 Mimi hutumia lugha ya Kiswahili nikiwa nyumbani au kwenye bweni**

| Shule   | Mimi hutumia lugha ya Kiswahili nikiwa nyumbani au bweni | Nakubali kabisa | Nakubali | Sikubali wala sikatai | Nakataa | Nakataa kabisa |
|---------|--|-----------------|----------|-----------------------|---------|----------------|
| Butula  | Idadi  | 43              | 31       | 01                    | 05      | 00             |
|         | Asilimia   | 53.75%          | 38.75%   | 1.25%                 | 6.25%   | 00%            |
| Mundika | Idadi  | 36              | 29       | 14                    | 01      | 00             |
|         | Asilimia   | 45%             | 36.25%   | 17.5%                 | 1.25%   | 00%            |
| Amukura | Idadi  | 32              | 31       | 13                    | 02      | 02             |
|         | Asilimia   | 40%             | 38.75%   | 16.25%                | 2.5%    | 2.5%           |
| Kisoko  | Idadi  | 16              | 13       | 03                    | 43      | 05             |
|         | Asilimia   | 20%             | 16.25%   | 3.75%                 | 53.75%  | 6.25%          |
| Chakol  | Idadi  | 43              | 20       | 16                    | 00      | 01             |
|         | Asilimia   | 53.75%          | 3.57%    | 20%                   | 00%     | 1.25%          |
| Lwanya  | Idadi  | 51              | 14       | 05                    | 04      | 06             |
|         | Asilimia   | 63.75%          | 17.5%    | 6.25%                 | 5%      | 7.5%           |
| Makunda | Idadi  | 17              | 19       | 24                    | 14      | 06             |
|         | Asilimia   | 21.25%          | 23.75%   | 30%                   | 17.5%   | 7.5%           |
| Jumla   | Idadi  | 238             | 157      | 76                    | 69      | 20             |
|         | Asilimia   | 42.5%           | 28.04%   | 13.57%                | 12.32%  | 3.57%          |

Utafiti ulibaini kuwa, kati ya wanafunzi 560 waliojaza hojaji likati, asilimia 70.54 ya wanafunzi wanapenda kuzungumza lugha ya Kiswahili wakiwa katika mazingira ya bweni au nyumbani hasa wale wa kutwa (Angalia jedwali 3.4). Katika mazingira haya, kuna uhuru wa kutumia lugha yoyote hasa wanafunzi wa shule za kutwa. Hii inaonyesha mielekeo chanya kwa lugha ya Kiswahili. Asilimia 13.57 hawakuonyesha mwelekeo wowote kwa sababu katika mazingira ya nyumbani au bweni, mwanafunzi ana uhuru wa kuzungumza lugha yoyote. Katika shule ya upili ya Mundika, mtafiti aligundua kuwa, ingawa kuna sheria inayohusu matumizi ya lugha katika mawasiliano, wanafunzi hutumia lugha ya Kiingereza, Kiswahili au sheng'. Hivyo ni ngumu kubaini mwelekeo wao kuhusu lugha ya mawasiliano.

Asilimia 15.89 ya wanafunzi wana mielekeo hasi dhidi ya matumizi ya lugha ya Kiswahili wakiwa nyumbani au bweni. Asilimia 25 ya wanafunzi kutoka shule ya Upili ya Makunda ambayo ni shule ya kutwa walisema kuwa wanapokuwa nyumbani, lugha ya mawasiliano ni lugha asilia au za kwanza. Baadhi ya watu wanaotangamana nao kule nyumbani hawana ujuzi katika lugha ya Kiswahili. Hivyo lugha inayorahisisha mawasiliano ni ile ya kiasili au ya kwanza. Katika shule ya upili ya wasichana ya Kisoko ambapo lugha ya Kiswahili huzungumzwa darasani wakati wa somo la Kiswahili, asilimia 60 ya wanafunzi hawa huzungumza lugha ya Kiingereza wakiwa kwenye bweni na 36.25 huzungumza lugha ya Kiswahili wakiwa katika mazingira ya bweni. Licha ya kukosekana walimu wa kuwachunguza ikiwa wanafuata kanuni za lugha kuhusu lugha ya mawasiliano ambayo ni Kiingereza tu, kupitia mjadala elekezi wa makundi, wanafunzi hawa walipoulizwa, walisema kuwa, kuna viranja wa shule ambao huandika majina ya wale wanaozungumza lugha ya Kiswahili kisha huadhibiwa. Hii huwafanya kuwa na mwelekeo hasi kuhusu lugha ya Kiswahili.

Utafiti ulibaini kutoka kwa wanafunzi kuwa, mielekeo yao kuhusu lugha ya Kiswahili kwa kiasi iliathiri mielekeo yao kuhusu somo somo la Kiswahili. Mielekeo hii iliathiri alama walizopata katika somo la Kiswahili. Matokeo haya yanawiana na ya Hunsen (1977) na kutofautiana na ya Babusa (2010) aliyesema kuwa, baadhi ya wanafunzi waliokuwa na mielekeo hasi kuhusu Kiswahili, walikuwa na viwango vya chini vya umilisi wa lugha, ilihali waliokuwa na mielekeo chanya walikuwa na viwango vya juu vya umilisi wa lugha. Kulingana na Hunsen (1977) anasema kuwa, wanafunzi walio na mielekeo chanya kuhusu somo fulani hupata alama za juu kuliko wale wenye mielekeo hasi. Vilevile, wanafunzi wenye

mielekeo chanya kuhusu somo hilo hutumia muda mwingi sana kufanya mazoezi kwa somo hilo. Hali hii kwa hivyo kuinua alama zao. Kutokana na matokeo haya ya utafiti, mtafiti alitaka kujua ikiwa wanafunzi wanapenda somo la Kiswahili kwa kubainisha mielekeo yao. Aidha katika makundi ya mjadala elekezi, mtafiti aliwapa swali, *Taja manufaa ya somo la Kiswahili*. Matokeo ya utafiti ni kama ifuatavyo;

### Jedwali 3.5 Napenda somo la Kiswahili

| Shule        | Napenda somo la Kiswahili | Nakubali kabisa | Nakubali      | Sikubali wala sikatai | Nakataa      | Nakataa kabisa |
|--------------|---------------------------|-----------------|---------------|-----------------------|--------------|----------------|
| Butula       | Idadi                     | 43              | 21            | 03                    | 12           | 01             |
|              | Asilimia                  | 53.75%          | 26.25%        | 3.75%                 | 15%          | 1.25%          |
| Mundika      | Idadi                     | 51              | 18            | 07                    | 03           | 01             |
|              | Asilimia                  | 63.75%          | 22.5%         | 8.75%                 | 3.75%        | 1.25%          |
| Amukura      | Idadi                     | 44              | 23            | 08                    | 04           | 01             |
|              | Asilimia                  | 55%             | 28.75%        | 10%                   | 5%           | 1.25%          |
| Kisoko       | Idadi                     | 32              | 26            | 13                    | 05           | 04             |
|              | Asilimia                  | 40%             | 32.5%         | 16.25%                | 6.25%        | 5%             |
| Chakol       | Idadi                     | 53              | 19            | 01                    | 03           | 04             |
|              | Asilimia                  | 66.25%          | 23.75%        | 1.25%                 | 3.75%        | 5%             |
| Lwanya       | Idadi                     | 45              | 27            | 03                    | 02           | 03             |
|              | Asilimia                  | 56.25%          | 33.75%        | 3.75%                 | 2.5%         | 3.75%          |
| Makunda      | Idadi                     | 34              | 18            | 06                    | 16           | 06             |
|              | Asilimia                  | 42.5%           | 22.5%         | 7.5%                  | 20%          | 7.5%           |
| <b>Jumla</b> | <b>Idadi</b>              | <b>302</b>      | <b>152</b>    | <b>41</b>             | <b>45</b>    | <b>20</b>      |
|              | <b>Asilimia</b>           | <b>53.93%</b>   | <b>27.14%</b> | <b>7.32%</b>          | <b>8.04%</b> | <b>3.57%</b>   |

Kati ya wanafunzi 560, asilimia 454(80.07%) wanapenda somo la Kiswahili. Wanafunzi hawa wana mielekeo chanya kuhusu somo la Kiswahili. Mielekeo chanya ya Somo la Kiswahili ni kwa kuwa hueleweka na ni rahisi kufuzu ikilinganishwa na masomo mengine. Asilimia 7.32% ya wanafunzi walichagua kauli sikubali wa sikatai. Asilimia 11.61% ya wanafunzi wana mielekeo hasi kwa somo la Kiswahili. Kulingana na wanafunzi hawa, somo la Kiswahili lina silabasi pana na ni ngumu kuelewa.

Katika hali ya kutangamana na wanafunzi, mtafiti aligundua kuwa, mielekeo ya wanafunzi kuhusu somo la Kiswahili ulichangia mwelekeo wake kwa kanuni za lugha za shule hasa zile ambazo zinahusu matumizi ya lugha shuleni. Mwanafunzi ambaye anapenda kuwasiliana kwa lugha sanifu, mwelekeo wake kuhusu somo la Kiswahili ulikuwa chanya.

Mtafiti pia alitaka kujua namna mwanafunzi huhisi anapowasiliana kwa lugha ya Kiswahili. Majibu ya wanafunzi kwa kauli hii yalimsaidia mtafiti kubaini mwelekeo wa mwanafunzi kuhusu lugha ya Kiswahili. Kauli ilioibua habari hii ni;

### Jedwali 3.6 Nikitumia lugha ya Kiswahili mimi huhisi raha sana

| Shule        | Nikitumia<br>a<br>Kiswahili<br>mimi<br>huhisi<br>raha sana | Nakubal<br>i kabisa | Nakubal<br>i  | Sikubal<br>i wala<br>sikatai | Nakata<br>a   | Nakata<br>a kabisa |
|--------------|--|---------------------|---------------|------------------------------|---------------|--------------------|
| Butula       | Idadi  | 23                  | 35            | 14                           | 06            | 02                 |
|              | Asilimia   | 28.75%              | 43.75%        | 17.5%                        | 7.5%          | 2.5%               |
| Mundika      | Idadi  | 17                  | 37            | 09                           | 10            | 07                 |
|              | Asilimia   | 21.25%              | 46.25%        | 11.25%                       | 12.5%         | 8.75%              |
| Amukura      | Idadi  | 25                  | 23            | 13                           | 14            | 05                 |
|              | Asilimia   | 31.25%              | 28.75%        | 16.25%                       | 17.5%         | 6.25%              |
| Kisoko       | Idadi  | 11                  | 08            | 03                           | 43            | 15                 |
|              | Asilimia   | 13.75%              | 10%           | 3.75%                        | 53.75%        | 18.75%             |
| Chakol       | Idadi  | 34                  | 26            | 04                           | 12            | 04                 |
|              | Asilimia   | 42.5%               | 32.5%         | 5%                           | 15%           | 5%                 |
| Lwanya       | Idadi  | 37                  | 32            | 02                           | 06            | 03                 |
|              | Asilimia   | 46.25%              | 40%           | 2.5%                         | 7.5%          | 3.75%              |
| Makunda      | Idadi  | 23                  | 11            | 17                           | 24            | 05                 |
|              | Asilimia   | 28.75%              | 13.75%        | 21.25%                       | 30%           | 6.25%              |
| <b>Jumla</b> | <b>Idadi</b>   | <b>170</b>          | <b>172</b>    | <b>62</b>                    | <b>115</b>    | <b>41</b>          |
|              | <b>Asilimia</b>  | <b>30.36%</b>       | <b>30.71%</b> | <b>11.07%</b>                | <b>20.54%</b> | <b>7.32%</b>       |

Kwa mujibu wa jedwali 3.6, Asilimia 61.07 ya wanafunzi hujivunia na huhisi raha wanapowasiliana kwa lugha ya Kiswahili. Hii inaonyesha kuwa wana mielekeo chanya wanapowasiliana kwa lugha ya Kiswahili. Katika shule za upili za Kitaifa na za zaidi ya Kaunti, lugha ya Kiswahili huwaunganisha wanafunzi hawa wanaotoka sehemu tofauti za nchi. Hii ndio lugha ambayo huwafanya kuhisi kuwa ndugu. Asilimia 11.07 ya wanafunzi hawakuonyesha mwelekeo wowote. Asilimia 27.86 ya wanafunzi wana mielekeo hasi kuhusu lugha ya Kiswahili. Katika shule ya Upili ya Kisoko, wanafunzi walisema kuwa, Kiswahili kimepigwa marafuku, hivyo hawaoni raha ya kuzungumza lugha ya Kiswahili kwa kuwa wataadhibiwa. Mueni (2017) anasema kuwa, lugha ya Kiswahili haitumiki katika hadhi sawa na lugha ya Kiingereza. Katika baadhi ya shule wanafunzi hawaruhusiwi kuzungumza lugha ya Kiswahili. Hali hii huwafanya wanafunzi kuwa na mazoea ya kuongea lugha ya Kiingereza na kuona lugha ya Kiswahili kama lugha ambayo haina umuhimu wowote. Hali hii inawafanya wanafunzi kuwa na mielekeo hasi kuhusu lugha ya Kiswahili.

Lugha ya Kiswahili imetengewa siku chache za kuwasiliana katika shule za upili za Kaunti ya Busia kama ilivyo katika kaunti nyinginezo. Utafiti ulionyesha kuwa, wanafunzi kutoka shule teule saba ambao walionyesha mielekeo hasi kuhusu mawasiliano kwa lugha ya Kiswahili ni kwa sababu Kiswahili kupewa siku chache za mawasiliano.

Kulingana na Mirianga (2014) Wakenya hasa waliosoma hupendelea na huionea fahari matumizi ya lugha ya Kiingereza hasa katika miktadha rasmi, huku wakiipaza lugha ya Kiswahili. Anaendelea kusema kuwa, ili matumizi ya lugha ya Kiswahili iweze kutekelezwa, ni muhimu kuipa nafasi nzuri katika mfumo wa elimu. Dhana

kuwa lugha ya Kiswahili ni lugha ya kiwango cha chini inafaa kuondolewa kwa sababu ni dhana iliyoenezwa na sera ya lugha ya wakoloni nchini Kenya ili kuangamiza mawasiliano kwa lugha ya Kiswahili. Matokeo ya uchunguzi huu yalibaini kuwa, dhana hizi zinapatikana pia kwa wanafunzi katika shule za upili Kaunti ya Busia walio na mielekeo hasi kuhusu lugha ya Kiswahili. Wao huhusisha lugha ya Kiswahili na watu wa hadhi ya chini, hivyo ili kuhisi raha, wao huzungumza Kiingereza au lugha za kigeni kama Kifaransa na Kijerumani ili kuinua hadhi yao wanapokuwa shuleni. Mielekeo kama hii inasikitisha sana hasa wakati ambapo Kiswahili ni lugha rasmi na ya Kitaifa.

### **3.1.2 Siku za Kiswahili**

Siku za Kiswahili ni siku ambazo lugha ya Kiswahili hutengwa ili itumike katika mawasiliano kati ya wanafunzi na wanafunzi au hata walimu katika mazingira ya shule. Kulingana na matokeo ya utafiti wa Mutua (2015), kila shule ina kanuni za lugha za shule tofauti. Kanuni hizi hutenga siku maalum ambapo wanafunzi huhitajika kuwasiliana kwa lugha ya Kiingereza au Kiswahili. Katika utafiti huu, mtafiti pia aligundua kuwa, katika shule za Upili Kaunti ya Busia, kuna siku imetengewa kuzungumza katika lugha ya Kiswahili. Ingawa wanafunzi katika Shule ya Upili ya wasichana ya Kisoko na shule ya Upili ya wavulana ya Mundika hawaruhusiwi kuwasiliana kwa lugha ya Kiswahili, katika shule hizi, kila muhula, wana siku iitwayo ‘Siku ya *Kiswahili*’, siku nzima hutengewa idara ya Kiswahili kuendeleza shughuli ambazo zinaimarisha somo la Kiswahili. Shughuli hizi ni kama, mijadala, makongamano ya ndani ya shule na lugha ya mawasiliano huwa lugha ya Kiswahili sanifu. Kwa hivyo, mtafiti alitaka kujua umuhimu wa siku za Kiswahili kwa kuwauliza katika makundi ya mijadala elekezi, *Eleza umuhimu wa*

siku za Kiswahili shuleni. Aidha alitaka kujua mielekeo ya wanafunzi 560 kutoka shule zote saba kuhusu siku za Kiswahili katika shule yao. Swala alilouliza ni;

**Jedwali 3.7 Napenda siku za Kiswahili shuleni mwetu**

| Shule        | Napenda siku za Kiswahili shuleni mwetu | Nakubali kabisa | Nakubali      | Sikubali wala sikatai | Nakataa      | Nakataa kabisa |
|--------------|---|-----------------|---------------|-----------------------|--------------|----------------|
| Butula       | Idadi                                   | 43              | 21            | 03                    | 07           | 06             |
|              | Asilimia                                | 53.75%          | 26.25%        | 3.75%                 | 8.75%        | 7.5%           |
| Mundika      | Idadi                                   | 42              | 23            | 08                    | 06           | 01             |
|              | Asilimia                                | 52.5%           | 28.75%        | 10%                   | 7.5%         | 1.25%          |
| Amukura      | Idadi                                   | 34              | 31            | 06                    | 08           | 01             |
|              | Asilimia                                | 42.5%           | 38.75%        | 7.5%                  | 10%          | 1.25%          |
| Kisoko       | Idadi                                   | 44              | 29            | 02                    | 03           | 02             |
|              | Asilimia                                | 55%             | 36.25%        | 2.5%                  | 3.75%        | 2.5%           |
| Chakol       | Idadi                                   | 43              | 26            | 01                    | 07           | 03             |
|              | Asilimia                                | 53.75%          | 32.5%         | 1.25%                 | 8.75%        | 3.75%          |
| Lwanya       | Idadi                                   | 46              | 18            | 05                    | 07           | 04             |
|              | Asilimia                                | 57.5%           | 22.5%         | 6.25%                 | 8.75%        | 05%            |
| Makunda      | Idadi                                   | 37              | 28            | 11                    | 03           | 01             |
|              | Asilimia                                | 46.25%          | 35%           | 13.75%                | 3.75%        | 1.25%          |
| <b>Jumla</b> | <b>Idadi</b>                            | <b>289</b>      | <b>176</b>    | <b>36</b>             | <b>41</b>    | <b>18</b>      |
|              | <b>Asilimia</b>                         | <b>51.61%</b>   | <b>31.43%</b> | <b>6.43%</b>          | <b>7.32%</b> | <b>3.21%</b>   |

Katika jedwali 3.7, Asilimia 83.04 ya wanafunzi wanapenda siku ya Kiswahili. Hii ina maana kuwa wana mwelekeo chanya kuhusu siku za Kiswahili shuleni mwao. Katika shule ya upili ya Kisoko, wanafunzi walisema kuwa, wanapenda siku hii kwa kuwa, huwapa fursa ya kipekee ya kuzungumza lugha ya Kiswahili baada ya muda mrefu. Aidha, wanafunzi walionyesha mwelekeo chanya walisema kuwa, ni siku ambayo walimu wa masomo mengine huzungumza lugha ya Kiswahili kwenye gwaride. Kulingana na Wanjiku (2014) anasema kuwa, walimu wa somo la Kiswahili wanapozungumza lugha sanifu darasani au kwenye gwaride, jambo hili huwafurahisha na huwapa motisha wanafunzi kuendelea kuzungumza lugha ya Kiswahili. Utafiti wa wataalamu Kobia na Ndwiga (2013), ulibaini kuwa, mielekeo

chanya ya walimu kuhusu lugha huathiri mielekeo ya wanafunzi kuwa chanya, na mielekeo hasi ya walimu kuhusu lugha ya Kiswahili itasababisha mielekeo hasi ya wanafunzi. Hivyo wanafunzi wanapoona walimu wakizungumza kwa lugha ya Kiswahili siku ya Kiswahili, huwa na mielekeo chanya kuhusu siku hii.

Asilimia 6.43 ya wanafunzi hawakuonyesha mwelekeo wowote. Asilimia 10.53 ya wanafunzi walionyesha mwelekeo hasi dhidi ya siku hii walisema kuwa, wao hulazimishwa na walimu wa somo la Kiswahili kuzungumza Kiswahili sanifu. Wasipozungumza lugha sanifu siku hii, walimu huwaadhibu. Adhabu hizi husababisha mielekeo hasi kuhusu siku ya Kiswahili. Kutokana na sababu hii, mtafiti alitaka kujua mwelekeo wa wanafunzi na maoni yao kuhusu adhabu hizi.

### **3.1.2.1 Adhabu za ukiukaji wa kanuni za lugha za shule kuhusu siku ya Kiswahili.**

Katika kamusi ya Kiswahili sanifu (2004), adhabu ni mateso anayopewa mtu aliyevunja kanuni au sheria. Wanjiku (2014), anasema kuwa, adhabu huwa na athari chanya au hasi kwa mwanafunzi. Ikiwa mwanafunzi ataadhibiwa kwa kuwa mawasiliano yao kwa kuwa wataogopa kuadhibiwa. Katika utafiti huu kupitia mbinu ya mjadala elekezi, mtafiti aliwauliza, *Una maoni yapi kuhusu adhabu za ukiukaji wa kanuni za lugha*. Mtafiti aligundua kuwa, wanafunzi walio na mielekeo hasi kuhusu siku ya Kiswahili, hawapendi adhabu wanayopewa wanapozungumza lugha tofauti na Kiswahili sanifu. Wanafunzi hawa walisema kuwa, wakati wa uwasilishaji wa mada fulani wao hukumbana na misamiati migumu ya lugha ya Kiswahili, hivyo huwalazimu kuchanganya lugha, jambo ambalo huwafanya kuadhibiwa na walimu wa somo la Kiswahili badala ya kuwarekebisha. Kulingana na Ingale na wengineo (1996), anasema kuwa, binadamu hupata motisha ya kufanya jambo linalosababisha

matokeo yanayofurahisha. Adhabu husababisha mielekeo hasi, hivyo matokeo ya adhabu hizi inaweza kuwafanya wanafunzi wanaojifunza lugha ya Kiswahili kuwa na uoga wa kuchanganya misamiati wanapokuwa shuleni. Ili kupata mielekeo ya wanafunzi kuhusu adhabu hizi, Swali waliloulizwa ni;

**Jedwali 3.8 Unakubaliana na adhabu za ukiukaji wa kanuni za lugha shuleni**

| Shule        | Nakubaliana na adhabu za ukiukaji wa kanuni za lugha shuleni | Nakubali kabisa | Nakubali      | Sikubali wala sikatai | Nakataa       | Nakataa kabisa |
|--------------|--|-----------------|---------------|-----------------------|---------------|----------------|
| Butula       | Idadi  | 11              | 18            | 02                    | 11            | 38             |
|              | Asilimia   | 13.75%          | 22.5%         | 2.5%                  | 13.75%        | 47.5%          |
| Mundika      | Idadi  | 09              | 13            | 01                    | 24            | 33             |
|              | Asilimia   | 11.25%          | 16.25%        | 1.25%                 | 30%           | 41.25%         |
| Amukura      | Idadi  | 04              | 10            | 06                    | 43            | 17             |
|              | Asilimia   | 5%              | 12.5%         | 7.5%                  | 53.75%        | 21.25%         |
| Kisoko       | Idadi  | 14              | 11            | 00                    | 40            | 15             |
|              | Asilimia   | 17.5%           | 13.75%        | 00%                   | 50%           | 18.75%         |
| Chakol       | Idadi  | 13              | 08            | 00                    | 46            | 13             |
|              | Asilimia   | 16.25%          | 10%           | 00%                   | 57.5%         | 16.25%         |
| Lwanya       | Idadi  | 07              | 06            | 00                    | 32            | 35             |
|              | Asilimia   | 8.75%           | 7.5%          | 00%                   | 40%           | 43.75%         |
| Makunda      | Idadi  | 12              | 17            | 03                    | 26            | 22             |
|              | Asilimia   | 15%             | 21.25%        | 3.75%                 | 32.5%         | 27.5%          |
| <b>Jumla</b> | <b>Idadi</b>   | <b>70</b>       | <b>83</b>     | <b>12</b>             | <b>222</b>    | <b>173</b>     |
|              | <b>Asilimia</b>  | <b>12.5%</b>    | <b>14.83%</b> | <b>2.14%</b>          | <b>39.64%</b> | <b>30.89%</b>  |

Kutokana na majibu ya wanafunzi 560 kutoka shule saba za utafiti, mtafiti alibaini kuwa, asilimia 27.33 ya wanafunzi wanakubaliana na adhabu hizi. Kwa hivyo wana mielekeo chanya kuhusu adhabu hizi. Maoni yao yalikuwa, adhabu huwasaidia kuzungumza lugha sanifu siku ya Kiswahili hivyo kuimarisha ujuzi wao katika somo la Kiswahili. Mwanafunzi wa shule ya Upili ya Chakol alisema kuwa;

‘Kila wanapoenda kinyume na kanuni za lugha za shule, wao huhitajika kuandika insha kumi kwa siku au kusoma vitabu vya riwaya na kujibu maswali kutokana na vitabu hivyo. Usipojibu maswali haya utapewa adhabu ya kuleta mzazi. Ili kuepuka adhabu hii, itabidi ujifunze kuzungumza Kiswahili sanifu. Hii humsaidia mwanafunzi kuimarisha ujuzi wake katika somo la Kiswahili na kutii kanuni za lugha shuleni’.

Asilimia 2.14 ya wanafunzi hawakuonyesha mwelekeo wowote. Asilimia 70.53 ya wanafunzi walionyesha mielekeo hasi hasa kuhusu adhabu zinazowapa fedheha kama zile za kuvalia mavazi ya aibu. Katika shule ya upili ya Lwanya, mtafiti alipoingia darasani ili kuwapa hojaji likati, alikumbana na wanafunzi wawili waliovalia gunia yenye maandishi ‘*Language breakers*.’ Jambo hili huwafanya kuchukua kanuni za lugha za shule. Adhabu za kuwatuma nyumbani hasa kununua vitabu teule vya riwaya haziwafurahishi pia. Gharama hii humwendea mzazi ilihali ni mwanafunzi aliyezungumza lugha tofauti na lugha ya Kiswahili siku hii.

Katika nadharia ya Kijumuia na Kibinadamu ya Richards na Rodgers (1995), mhimili wa kwanza unasema kuwa, usalama wa mwanafunzi ni muhimu kwani, mwanafunzi anapokuwa na wasiwasi na kutojisikia salama, hawezi kujifunza lugha vizuri. Adhabu zinazompa mwanafunzi uoga kama za kuvalia mavazi ya aibu zilizoandikwa maneno kama ‘*I am a fool ama I am a language policy breaker*’ hufanya wanafunzi kuwa na wasiwasi hivyo kuchangia mielekeo hasi kuhusu lugha. Kwa hivyo hatajifunza lugha hiyo.

Utafiti huu pia uligundua kuwa, katika shule ya upili ya Chakol, hakuna mwanafunzi ambaye aliadhibiwa alipozungumza Lugha ya Kiingereza siku za Kiswahili. Walimu hasa wa masomo mengine ambayo si wa Kiswahili, walikuwa makini sana kuwaadhibu wanafunzi waliozungumza lugha ya Kiswahili siku ya lugha ya

Kiingereza. Jambo hili liliathiri mielekeo ya wanafunzi kuwa hasi dhidi ya lugha ya Kiswahili. Wanafunzi waliona lugha ya Kiswahili kama lugha duni. Katika utafiti wa Timammy na Oduor (2016), wanasema kuwa, ingawa lugha ya Kiswahili na Kiingereza kuwa lugha rasmi nchini Kenya, masomo ya lazima na ya kutahiniwa, lugha ya Kiingereza imekwezwa kihadhi. Wanasema kuwa, wanafunzi wengi huadhibiwa wanapozungumza lugha ya Kiswahili. Jambo hili huchangia wanafunzi kutopenda kuwasiliana kwa lugha ya Kiswahili.

### **3.3.3 Mabango na maandishi katika mazingira ya shule.**

Kulingana na Kamusi ya karne ya 21 (2019), bango ni karatasi kubwa au bao kubwa lenye matangazo ya biashara au ujumbe maalumu. Koko (2016) anasema kuwa, hutumiwa kuwakumbusha wanafunzi na wapita njia kuzungumza kwa lugha sanifu. Katika uainishaji wa kanuni za lugha za shule, mabango na maandishi ni kati ya kanuni za lugha za shule zinazopatikana katika mazingira ya shule za upili. Katika shule za utafiti, mtafiti alipokuwa akiingia, aliweza kukutana na mabango na maandishi tofauti katika mazingira haya. Ili kutambua umuhimu wa mabango na maandishi katika mazingira ya shule, mtafiti aliwapa swali la mjadala elekezi wa makundi; *Taja umuhimu wa mabango na maandishi katika mazingira ya shule.* Mielekeo ya wanafunzi nayo ilibainishwa kupitia swali;

**Jedwali 3.9 Mabango na maandishi yanayohusu matumizi ya lugha shuleni ni ya mahufaa**

| Shule        | Mabango na maandishi yanayohusu matumizi ya lugha shuleni ni ya manufaa | Nakubali kabisa | Nakubali      | Sikubali wala sikatai | Nakataa       | Nakataa kabisa |
|--------------|---|-----------------|---------------|-----------------------|---------------|----------------|
| Butula       | Idadi   | 32              | 11            | 24                    | 13            | 00             |
|              | Asilimia  | 40%             | 13.75%        | 30%                   | 16.25%        | 00%            |
| Mundika      | Idadi   | 18              | 14            | 08                    | 34            | 06             |
|              | Asilimia  | 22.5%           | 17.5%         | 10%                   | 42.5%         | 7.5%           |
| Amukura      | Idadi   | 17              | 11            | 19                    | 28            | 05             |
|              | Asilimia  | 21.25%          | 13.75%        | 23.75%                | 35%           | 6.25%          |
| Kisoko       | Idadi   | 07              | 21            | 06                    | 33            | 13             |
|              | Asilimia  | 8.75%           | 26.25%        | 7.5%                  | 41.25%        | 16.25%         |
| Chakol       | Idadi   | 31              | 24            | 02                    | 17            | 06             |
|              | Asilimia  | 38.75%          | 30%           | 2.5%                  | 21.25%        | 7.5%           |
| Lwanya       | Idadi   | 34              | 32            | 03                    | 11            | 00             |
|              | Asilimia  | 42.5%           | 40%           | 3.75%                 | 13.75%        | 00%            |
| Makunda      | Idadi   | 19              | 23            | 24                    | 07            | 07             |
|              | Asilimia  | 23.75%          | 28.75%        | 30%                   | 8.75%         | 8.75%          |
| <b>Jumla</b> | <b>Idadi</b>  | <b>158</b>      | <b>136</b>    | <b>86</b>             | <b>143</b>    | <b>37</b>      |
|              | <b>Asilimia</b>   | <b>28.2%</b>    | <b>24.29%</b> | <b>15.36%</b>         | <b>25.54%</b> | <b>6.61%</b>   |

Majibu ya wanafunzi katika jedwali 3.9 yalionyesha kuwa, asilimia 52.49 ya wanafunzi wana mielekeo chanya kuhusu kuwepo kwa mabango na maandishi yanayohusu matumizi ya lugha. Asilimia 15.36 ya wanafunzi hawakuonyesha mielekeo yoyote ilihali asilimia 32.15 ya wanafunzi walionyesha mielekeo hasi kuhusiana na mabango haya. Wanafunzi hasa kutoka shule ya wasichana ya Chakol walionyesha mielekeo chanya. Wanafunzi hawa walisema kuwa, kuna baadhi ya mabango ambayo huwakumbusha kuzungumza lugha inayostahili na sanifu hivyo yana manufaa. Kwa mfano, katika Kielelezo cha 1.3 katika shule ya upili ya Chakol. Wale wanafunzi waliyoonyesha mielekeo hasi walisema kuwa, mabango katika shule zao huwakumbusha tu kuzungumza lugha ya Kiingereza na kutukuza masomo

mengine. Kwa mfano katika shule ya Upili ya Mundika na shule ya Upili ya Lwanya, mabango yanayohusu matumizi ya lugha yameandikwa '*Speak English*'. Mabango kama haya yanayotukuza lugha ya Kiingereza hufanya wanafunzi kuchukia lugha ya Kiswahili na kuiona isiyofaa. Ingekuwa bora zaidi ikiwa maandishi haya pia yangekitukuza somo la Kiswahili.

Kupitia mbinu ya uchunzaji katika mazingira ya shule, mtafiti alibaini kuwa, kwenye ubao, maandishi huwa ni ya Kiingereza. Hii inaonyesha kuwa lugha ya Kiingereza ndiyo inayothaminiwa sana. Katika shule ya upili ya Chakol na Mundika, kuna sehemu katika ubao wa matangazo ambayo huwekwa vielelezo vya insha bora ya wanafunzi. Wanafunzi katika shule hizi walionyesha mielekeo chanya kwa lugha ya Kiswahili hasa wale ambao insha zao ziliwekwa pale.

#### **3.1.4 Matumizi ya lugha ya Kiswahili katika mijadala**

Kulingana na Kamusi ya Kiswahili sanifu (2004), mijadala ni mazungumzo juu ya jambo maalum yanayofanywa kwa kutolea hoja kuhusu jambo ama mada fulani. Katika shule za upili zilizoteuliwa katika utafiti huu, shule zote saba zina siku za mijadala. Ili kubaini mielekeo ya wanafunzi pamoja na umuhimu wa mijadala, mtafiti aliuliza swali lifuatalo;

**Jedwali 3.10 Mijadala inayoendeshwa kwa lugha ya Kiswahili ni muhimu**

| Shule        | Mijadala inayoendeshwa kwa lugha ya Kiswahili ni muhimu. | Nakubali kabisa | Nakubali      | Sikubali wala sikatai | Nakataa      | Nakataa kabisa |
|--------------|--|-----------------|---------------|-----------------------|--------------|----------------|
| Butula       | Idadi  | 44              | 28            | 00                    | 07           | 01             |
|              | Asilimia   | 55%             | 35%           | 00%                   | 8.75%        | 1.25%          |
| Mundika      | Idadi  | 29              | 42            | 01                    | 06           | 02             |
|              | Asilimia   | 36.25%          | 52.5%         | 1.25%                 | 7.5%         | 2.5%           |
| Amukura      | Idadi  | 21              | 48            | 00                    | 04           | 07             |
|              | Asilimia   | 26.25%          | 60%           | 00%                   | 5%           | 8.75%          |
| Kisoko       | Idadi  | 54              | 19            | 01                    | 02           | 04             |
|              | Asilimia   | 67.5%           | 23.75%        | 1.25%                 | 2.5%         | 5%             |
| Chakol       | Idadi  | 46              | 27            | 00                    | 05           | 02             |
|              | Asilimia   | 57.5%           | 33.75%        | 00%                   | 6.25%        | 2.5%           |
| Lwanya       | Idadi  | 33              | 38            | 00                    | 08           | 01             |
|              | Asilimia   | 41.25%          | 47.5%         | 00%                   | 10%          | 1.25%          |
| Makunda      | Idadi  | 31              | 26            | 09                    | 13           | 01             |
|              | Asilimia   | 38.75%          | 32.5%         | 11.25%                | 16.25%       | 1.25%          |
| <b>Jumla</b> | <b>Idadi</b>   | <b>258</b>      | <b>228</b>    | <b>11</b>             | <b>45</b>    | <b>18</b>      |
|              | <b>Asilimia</b>  | <b>46.07%</b>   | <b>40.71%</b> | <b>1.96%</b>          | <b>8.04%</b> | <b>3.22%</b>   |

Kulingana na majibu ya wanafunzi kutoka shule saba za utafiti, asilimia 86.78 ya wanafunzi wana mielekeo chanya kuhusu mijadala kwa lugha ya Kiswahili. Wanafunzi hawa walisema kuwa, mijadala huwafaidi hasa katika karatasi la kwanza la somo la Kiswahili. Katika karatasi hili, swali la pili la insha linahitaji mwanafunzi kujadili mada inayohusu maswali ibuka. Baadhi ya mada hizi huwa zimejadiliwa siku za mijadala hivyo wao hupenda siku za mijadala. Aidha walimu wa somo la Kiswahili huwaelekeza namna ya kujadili hoja hizi siku hiyo ya mijadala. Katika nadharia ya vitendo vilivyofikiriwa ya Ajzen na Fishbein (1980) mhimili wa kwanza wa nadharia hii hutabiri na kuelewa tabia za watu. Ikiwa jambo fulani litamnufaisha mtu, ataweza kubadilisha tabia yake na kuwa na mwelekeo chanya kuhusiana na

jambo hilo. Mijadala hii huwafaidi wanafunzi hasa katika mitihani ya somo la Kiswahili, hivyo wao huwa na mwelekeo chanya.

Licha ya utafiti huu kulenga habari kuhusu mijadala, Katika shule ya Kitaifa ya Butula, Shule ya Upili ya Wasichana ya Lwanya na shule ya Upili ya Wasichana ya Kisoko wakati mwingine badala ya mijadala wao huwa na midahalo kama njia moja ya kuimarisha ujuzi wao katika somo la Kiswahili. Wanafunzi ambao hushiriki katika mijadala na midahalo huzawadiwa ili kuwapa motisha. Gardener (1985), anasema kuwa, wakati mtu anapojifunza kuhusu lugha, basi kigezo cha motisha kitakuwa muhimu katika kufanya mtu huyo kuwa na mwelekeo chanya. Kulingana na utafiti wa Kinya (2020), katika mashindano ya lugha ya Kiswahili, motisha na tuzo kwa wanafunzi hufanya wanafunzi kuwa na mieleko chanya kuhusu somo la Kiswahili.

Asilimia 1.96 ya wanafunzi hawakuonyesha mielekeo yoyote ilhali asilimia 11.26 ya wanafunzi hawapendi siku ya mijadala kwa lugha ya Kiswahili. Wanafunzi hawa walisema kuwa, mwalimu wa somo la Kiswahili asipohudhuria, wanafunzi hupiga tu kelele badala ya kushiriki katika mijadala.

### **3.1.5 Shughuli za idara**

Idara ni sehemu inayoshughulikia jambo fulani katika wizara, shirika au kampuni kulingana na Kamusi sanifu ya Kiswahili (2004). Katika shule za upili, Idara ya Kiswahili imepewa jukumu na uongozi wa shule kutekeleza shughuli mbalimbali zinazohusu idara hii. Lengo kuu ni kuweka mikakati itakayoimarisha somo la Kiswahili. Kupitia mbinu ya mahojiano na wakuu wa idara ya Kiswahili, utazamaji wa kumbukumbu za mikutano na ratiba ya idara ya Kiswahili, shughuli za idara

katika kipindi cha muhula fulani zimebainishwa. Shughuli hizi ni kama vyama vya Kiswahili, vipindi vya ziada, makongamano ndani na nje ya shule, usomaji wa vitabu na magazeti. Unapotazama kumbukumbuza mikutano katika idara ya Kiswahili, kwa kila Shughuli, kando yake kuna majina ya walimu katika kumbukumbu hizi kuonyesha watakaotekeleza shughuli hizo. Shughuli za idara zimejadiliwa kama ifuatavyo;

### 3.1.5.1 Vyama vya Kiswahili

Kulingana na kamusi sanifu ya Kiswahili (2004), chama ni kikundi cha watu walioungana pamoja kwa lengo la kutekeleza matakwa yao ya kisiasa, kiuchumi au kijamii. Katika shule za upili katika kaunti ya Busia, mtafiti aligundua kuwa, kuna shule ambazo zina vyama ambavyo vinaimarisha somo la Kiswahili. Kuna chama cha Kiswahili na chama cha wanahabari. Kutokana na sababu hii, mtafiti alitaka kujua umuhimu wa vyama hivi pamoja na mielekeo ya wanafunzi 560 kutoka shule saba za upili kuhusu vyama hivi. Kauli waliojibu ni;

#### Jedwali 3.11 Vyama vya Kiswahili vina manufaa shuleni

| Shule   | Vyama vya Kiswahili vina manufaa shuleni | Nakubali kabisa | Nakubali      | Sikubali wala sikatai | Nakataa      | Nakataa kabisa |
|---------|--|-----------------|---------------|-----------------------|--------------|----------------|
| Butula  | Idadi                                    | 34              | 37            | 00                    | 08           | 01             |
|         | Asilimia                                 | 42.5%           | 46.25%        | 00%                   | 10%          | 1.25%          |
| Mundika | Idadi                                    | 27              | 43            | 07                    | 03           | 00             |
|         | Asilimia                                 | 33.75%          | 53.75%        | 8.75%                 | 3.75%        | 00%            |
| Amukura | Idadi                                    | 34              | 23            | 17                    | 06           | 00             |
|         | Asilimia                                 | 42.5%           | 28.75%        | 21.25%                | 7.5%         | 00%            |
| Kisoko  | Idadi                                    | 39              | 28            | 04                    | 08           | 01             |
|         | Asilimia                                 | 48.75%          | 35%           | 5%                    | 10%          | 1.25%          |
| Chakol  | Idadi                                    | 49              | 25            | 00                    | 04           | 02             |
|         | Asilimia                                 | 61.25%          | 31.25%        | 00%                   | 5%           | 2.5%           |
| Lwanya  | Idadi                                    | 52              | 16            | 01                    | 07           | 04             |
|         | Asilimia                                 | 65%             | 20%           | 1.25%                 | 8.75%        | 5%             |
| Makunda | Idadi                                    | 34              | 32            | 11                    | 03           | 00             |
|         | Asilimia                                 | 42.5%           | 40%           | 13.75%                | 3.75%        | 00%            |
| Jumla   | <b>Idadi</b>                             | <b>269</b>      | <b>204</b>    | <b>40</b>             | <b>39</b>    | <b>08</b>      |
|         | <b>Asilimia</b>                          | <b>48.04%</b>   | <b>36.43%</b> | <b>7.14%</b>          | <b>6.96%</b> | <b>1.43%</b>   |

Kulingana na jedwali 3.11, asilimia 84.47 ya jumla ya wanafunzi wanapenda vyama vya Kiswahili. Hii inaonyesha mielekeo chanya ya wanafunzi kuhusu vyama vya Kiswahili. Katika shule ya Upili ya Kitaifa ya Butula, wana chama cha Kiswahili kwa jina (CHAKIBU). Wanafunzi hawa kupitia mbinu ya mjadala elekezi, mtafiti alitaka kujua manufaa ya chama cha Kiswahili shuleni mwao. Swali alilowauliza ni, *Eleza manufaa ya chama cha Kiswahili shuleni mwenu?* Wanafunzi walisema kuwa, chama hiki kimekuwa cha manufaa kwao. Chama hiki kimepewa jukumu la kuandaa mijadala shuleni na kuhakikisha kuwa kila mwanafunzi anawasiliana kwa lugha sanifu. Wanachama hawa pia huandaa habari kila Ijumaa na kuwasilisha kwenye gwaride. Husaidiana pia na idara ya Kiswahili kuandaa makongamano ya ndani ya shule. Wanafunzi wa chama cha Uanahabari walionyesha mielekeo chanya kuhusu lugha ya Kiswahili, walisema kuwa vyama vimewapa fursa ya kunoa ujuzi wao katika uwasilishaji wa habari. Asilimia 7.14 ya wanafunzi hawakuonyesha mwelekeo wowote nao asilimia 8.39 ya wanafunzi walisema kuwa hawapendi vyama vya Kiswahili, hivyo kuonyesha mwelekeo hasi. Wanafunzi wenye mielekeo hasi walisema kuwa, vyama hivi vimebaki kuwa kati ya kanuni za shule ambazo hazitiliwi maanani na uongozi wa shule.

### **3.1.5.2 Vipindi vya ziada**

Kulingana na utafiti wa Kimaro (2013), somo la Kiswahili halijatendewa haki katika ugawaji wa vipindi kwa ratiba ya shule. Anasema kuwa, walimu wa somo la Kiswahili wanadai kuwa, silabasi ya somo la Kiswahili ni pana sana ikilinganishwa na somo la Kiingereza lakini Kiingereza kimepewa idadi nyingi ya vipindi ikilinganishwa na somo la Kiswahili. Madai kama haya yameshuhudiwa katika shule za upili katika Kaunti ya Busia. Shule hizi huongeza vipindi vya ziada ili kuhitimisha

silabasi pana ya somo la Kiswahili. Ili kuibua habari kuhusu umuhimu wa vipindi vya ziada, kupitia mjadala elekezi, swali lililoulizwa ni, *Fafanua manufaa ya vipindi vya ziada vya somo la Kiswahili.* Aidha mielekeo ya wanafunzi kuhusu vipindi vya ziada ilibainishwa kupitia kauli ifuatayo kwa wanafunzi;

**Jedwali 3.12 Vipindi vya ziada vya somo la Kiswahili ni muhimu**

| Shule        | Vipindi vya ziada vya somo la Kiswahili ni muhimu | Nakubali kabisa | Nakubali      | Sikubali wala sikatai | Nakataa      | Nakataa kabisa |
|--------------|---|-----------------|---------------|-----------------------|--------------|----------------|
| Butula       | Idadi   | 31              | 23            | 16                    | 05           | 05             |
|              | Asilimia  | 38.75%          | 28.75%        | 20%                   | 6.25%        | 6.25%          |
| Mundika      | Idadi   | 24              | 35            | 11                    | 07           | 03             |
|              | Asilimia  | 30%             | 43.75%        | 13.75%                | 8.75%        | 3.75%          |
| Amukura      | Idadi   | 16              | 38            | 23                    | 01           | 02             |
|              | Asilimia  | 20%             | 47.5%         | 28.75%                | 1.25%        | 2.5%           |
| Kisoko       | Idadi   | 34              | 14            | 13                    | 11           | 08             |
|              | Asilimia  | 42.5%           | 17.5%         | 16.25%                | 13.75%       | 10%            |
| Chakol       | Idadi   | 46              | 19            | 07                    | 06           | 02             |
|              | Asilimia  | 57.5%           | 23.75%        | 8.75%                 | 7.5%         | 2.5%           |
| Lwanya       | Idadi   | 43              | 26            | 07                    | 03           | 01             |
|              | Asilimia  | 53.75%          | 32.5%         | 8.75%                 | 3.75%        | 1.25%          |
| Makunda      | Idadi   | 26              | 17            | 19                    | 12           | 06             |
|              | Asilimia  | 32.5%           | 21.25%        | 23.75                 | 15%          | 7.5%           |
| <b>Jumla</b> | <b>Idadi</b>                                      | <b>220</b>      | <b>172</b>    | <b>96</b>             | <b>45</b>    | <b>27</b>      |
|              | <b>Asilimia</b>                                   | <b>39.29%</b>   | <b>30.71%</b> | <b>17.14%</b>         | <b>8.04%</b> | <b>4.82%</b>   |

Kulingana na matokeo ya utafiti huu, asilimia 70 ya wanafunzi wana mielekeo chanya kuhusu vipindi vya ziada vya somo la Kiswahili. Vipindi hivi husaidia katika kukamilisha silabasi kwa wakati hivyo kumpa mwanafunzi muda zaidi wa kufanya mazoezi ili kuimarisha ujuzi wao katika somo la Kiswahili. Katika shule ya upili ya Chakol, wao hutumia vipindi hivi kuweka wanafunzi kwenye makundi. Mwanafunzi hupata fursa ya kuuliza mwalimu wa somo maswali na kutangamana

nao. Hali hii ni tofauti na vipindi vya kawaida. Asilimia 17.14 ya wanafunzi hawakuonyesha mielekeo yoyote. Asilimia 12.86 ya wanafunzi wana mielekeo hasi dhidi ya vipindi vya ziada kwa sababu huwanyima fursa ya kufanya kazi zao za kibinafsi. Kwa mfano kuna mwanafunzi mmoja kutoka shule ya Upili ya Amukura alisema kuwa;

‘Vipindi vya ziada shuleni mwetu, huanza asubuhi na mapema kuanzia saa kumi na mbili hadi saa moja asubuhi. Wakati huu ndio wakati mwafaka wa kufanya kazi ya ziada ya walimu na kujisomea. Hivyo mwalimu wa somo anapokuja kufunza, ni vigumu sana kufanya kazi ya binafsi’.

Mwalimu mkuu wa shule ya Mseto ya Makunda, alisema kuwa, silabasi ya somo la Kiswahili ni pana sana, ili kufidia upungufu huu, kuna vipindi vya ziada vya somo la Kiswahili katika ratiba ya kawaida ya shule. Katika shule hii, hawana masomo kama ya uchoraji, somo la sayansi ya nyumbani, lugha za kigeni au la ujenzi, hivyo ili kufidia upungufu huu, vipindi vya somo la Kiswahili vimeongezwa na huendeshwa saa ambayo inakubaliwa na wizara ya Elimu, kuanzia saa mbili hadi saa kumi jioni. (Tazama kielelezo 1.4). Hii inaonyesha mwelekeo chanya kuhusu vipindi vya ziada.

Katika shughuli za idara, mtafiti pia aligundua kuwa, wanafunzi huhudhuria makongamano yanayoandaliwa ndani na nje ya shule.

### **3.1.5.3 Makongamano ya ndani na nje ya shule**

Kwa mujibu wa kamusi sanifu ya Kiswahili (2004), kongamano ni mjadala juu ya jambo fulani unaofanywa na mkusanyiko wa watu. Hujumuisha warsha, mkutano au kongamano la kitaifa la walimu. Katika shule saba za utafiti, mtafiti aligundua kuwa, kuna makongamano ya ndani ya shule ambayo huandaliwa na idara ya Kiswahili.

mtafiti katika makundi ya mjadala elekezi aliwauliza swali, *Taja umuhimu wa kushiriki katika makongamano ya Kiswahili ya ndani mwa shule*. Ili kubainisha mielekeo ya wanafunzi kuhusu makongamano ya ndani ya shule, swali ambalo mtafiti aliuliza ni ;

**Jedwali 3.13 Mimi hushiriki katika makongamano ya Kiswahili ya ndani mwa shule**

| Shule        | Mimi hushiriki katika makongamano ya Kiswahili ya ndani mwa shule. | Nakubali kabisa | Nakubali      | Sikubali wala sikatai | Nakataa      | Nakataa kabisa |
|--------------|--|-----------------|---------------|-----------------------|--------------|----------------|
| Butula       | Idadi  | 57              | 14            | 01                    | 06           | 02             |
|              | Asilimia   | 71.25%          | 17.5%         | 1.25%                 | 7.5%         | 2.5%           |
| Mundika      | Idadi  | 46              | 18            | 03                    | 07           | 06             |
|              | Asilimia   | 57.5%           | 22.5%         | 3.75%                 | 8.75%        | 7.5%           |
| Amukura      | Idadi  | 48              | 23            | 04                    | 03           | 02             |
|              | Asilimia   | 60%             | 28.75%        | 5%                    | 3.75%        | 2.5%           |
| Kisoko       | Idadi  | 53              | 16            | 06                    | 04           | 01             |
|              | Asilimia   | 66.25%          | 20%           | 7.5%                  | 5%           | 1.25%          |
| Chakol       | Idadi  | 61              | 13            | 01                    | 03           | 02             |
|              | Asilimia   | 76.25%          | 16.25%        | 1.25%                 | 3.75%        | 2.5%           |
| Lwanya       | Idadi  | 57              | 21            | 00                    | 02           | 00             |
|              | Asilimia   | 71.25%          | 26.25%        | 00%                   | 2.5%         | 00%            |
| Makunda      | Idadi  | 34              | 37            | 03                    | 04           | 02             |
|              | Asilimia   | 42.5%           | 46.25%        | 3.75%                 | 5%           | 2.5%           |
| <b>Jumla</b> | <b>Idadi</b>   | <b>356</b>      | <b>142</b>    | <b>18</b>             | <b>29</b>    | <b>15</b>      |
|              | <b>Asilimia</b>  | <b>63.57%</b>   | <b>25.36%</b> | <b>3.21%</b>          | <b>5.18%</b> | <b>2.68%</b>   |

Kutokana na matokeo katika jedwali 3.13 wanafunzi 498(88.93%) waliohojiwa walikiri kwamba wanapenda makongamano ya ndani mwa shule. Kwa hivyo kuwa na mwelekeo chanya kuyahusu. Kupitia mjadala elekekezi wa makundi, mtafiti aliwauliza, *Eleza umuhimu wa kushiriki katika makongamano ya ndani mwa*

*shule*.wanafunzi hawa walisema kuwa, makongamano huwapa fursa ya kujenga stadi zote za lugha. Aidha, huwatoa katika mazingira ya kila siku ya darasani ambayo yanachosha. Kimemia (2001) anasema kuwa, mtindo wa kufundisha Kiswahili katika shule kwa njia ya ubao na chaki tu umepitwa na wakati. Kiswahili kinafaa kufundishwa kwa kujenga stadi zote za lugha. Stadi za lugha zinajumuisha kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika. Katika shule ya Upili ya Lwanya, wanafunzi walisema kuwa, wanapenda sana siku hii kwa sababu shughuli mbalimbali kama mijadala, uandishi wa insha, kuuliza na kujibu maswali kwa vikundi na hata kuripoti matukio au kusoma habari kwa lugha sanifu hutekelezwa. Mwalimu mkuu wa shule hii alisema kuwa, tangu aanze kufadhili shughuli za aina hii, ameona somo la Kiswahili likiimarika, hivyo kuwa na mwelekeo chanya. Asilimia 3.21 ya wanafunzi hawakuonyesha mwelekeo wowote ilihali asilimia 7.86 ya wanafunzi wana mielekeo hasi dhidi ya makongamano ya ndani mwa shule. Mwanafunzi mmoja kutoka shule ya upili ya Chakol alisema kuwa siku hii huchosha hasa wanapohitajika kufanya mitihani. Atafurahia sana ikiwa shughuli nyingine kama vile tamasha za muziki na uigizaji zingejumuishwa. Mtafiti pia alitaka kujua mielekeo wa wanafunzi kuhusu makongamano ya nje ya shule. Swali alilouliza ni;

**Jedwali 3.14 Mimi huhudhuria makongamano ya Kiswahili ya nje ya shule**

| Shule        | Mimi huhudhuria makongamano ya nje ya shule | Nakubali kabisa | Nakubali      | Sikubali wala sikatai | Nakataa      | Nakataa kabisa |
|--------------|---|-----------------|---------------|-----------------------|--------------|----------------|
| Butula       | Idadi                                       | 63              | 11            | 04                    | 01           | 01             |
|              | Asilimia                                    | 78.75%          | 13.75%        | 5%                    | 1.25%        | 1.25%          |
| Mundika      | Idadi                                       | 52              | 26            | 02                    | 00           | 00             |
|              | Asilimia                                    | 65%             | 32.5%         | 2.5%                  | 00%          | 00%            |
| Amukura      | Idadi                                       | 53              | 24            | 01                    | 02           | 00             |
|              | Asilimia                                    | 66.25%          | 30%           | 1.25%                 | 2.5%         | 00%            |
| Kisoko       | Idadi                                       | 61              | 18            | 00                    | 01           | 00             |
|              | Asilimia                                    | 76.25%          | 22.5%         | 00%                   | 1.25%        | 00%            |
| Chakol       | Idadi                                       | 43              | 32            | 03                    | 02           | 00             |
|              | Asilimia                                    | 53.75%          | 40%           | 3.75%                 | 2.5%         | 00%            |
| Lwanya       | Idadi                                       | 56              | 18            | 04                    | 01           | 01             |
|              | Asilimia                                    | 70%             | 22.5%         | 5%                    | 1.25%        | 1.25%          |
| Makunda      | Idadi                                       | 49              | 27            | 02                    | 02           | 00             |
|              | Asilimia                                    | 61.25%          | 33.75%        | 2.5%                  | 2.5%         | 00%            |
| <b>Jumla</b> | <b>Idadi</b>                                | <b>377</b>      | <b>156</b>    | <b>16</b>             | <b>09</b>    | <b>02</b>      |
|              | <b>Asilimia</b>                             | <b>67.32%</b>   | <b>27.86%</b> | <b>2.86%</b>          | <b>1.61%</b> | <b>0.36%</b>   |

Kwa mujibu wa jedwali 3.14, asilimia 95.18 ya wanafunzi waliohojiwa wana mielekeo chanya kuhusu makongamano ya nje ya shule. Wanafunzi walionyesha mielekeo chanya walisema kuwa, wanapotangamana na wanafunzi kutoka shule nyingine, hujadiliana mada tofauti katika somo la Kiswahili. Jambo hili limekuwa kama motisha kwa wanafunzi hivyo kufanya mielekeo yao kuhusu somo la Kiswahili kuwa chanya. Mtafiti pia kupitia vikundi vya mijadala elekezi aliwauliza swali lifuatalo, *Eleza manufaa ya makongamano ya nje ya shule?*

Mtafiti alibaini kuwa, wanafunzi wengi hufurahia kwenda shule nyinginezo ili kushiriki katika makongamano ya nje. Kwa hivyo makongamano haya yamekuwa kama motisha kwa wanafunzi. Katika shule ya Upili ya Kitaifa ya Butula, wanafunzi wengi wamejiunga na chama cha Kiswahili ili wapate fursa ya kushiriki makongamano ya nje ya shule. Hii imechangia mielekeo chanya kwa somo la

Kiswahili. Makongamano ya nje pia humpa mwanafunzi fursa ya kutumia njia mbalimbali za usomaji. Njia hizi ni kama kujadiliana na wanafunzi kutoka shule zingine mada mpya ambazo hawajafunzwa shuleni mwao.

Asilimia 1.97 ya wanafunzi wana mwelekeo hasi dhidi ya makongamano ya nje ya shule. Wanafunzi hawa ni wale ambao huwa hawapewi nafasi ya kushiriki katika makongamano ya nje. Matokeo ya utafiti wa Munialo (2010) yalionyesha kuwa, wanafunzi wa eneo la Rachuonyo huwa na mielekeo hasi katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili, lakini mielekeo hii inaweza kubadilishwa kupitia matembezi ya nje na kushiriki katika makongamano. Kwa hivyo ni bora ikiwa shule zitawafadhili wanafunzi hasa walio na mielekeo hasi kuhusu lugha ya Kiswahili kushiriki katika makongamano ya nje ili kubadilisha mielekeo yao.

#### **3.1.5.4 Usomaji wa vitabu vya hadithi na magazeti ya Lugha ya Kiswahili**

Gazeti ni mkusanyiko wa karatasi zilizochapishwa ndani yake mkiwa na habari, makala na matangazo yanayotolewa kwa kipindi maalumu kama vile kila siku, kila wiki au kila mwezi (Kamusi ya Karne ya 21, 2019). Usomaji wa vitabu vya hadithi na magazeti pia huwa mojawapo wa shughuli za idara. Hivyo mtafiti alitaka kujua mwelekeo wa wanafunzi kuhusu usomaji wa vitabu vya hadithi na magazeti ya Kiswahili. Swali alilouliza ni;

**Jedwali 3.15 Mimi husoma vitabu vya hadithi na magazeti ya lugha ya Kiswahili shuleni**

| Shule        | Mimi husoma vitabu na magazeti ya lugha ya Kiswahili | Nakubali kabisa | Nakubali      | Sikubali wala sikatai | Nakataa       | Nakataa kabisa |
|--------------|--|-----------------|---------------|-----------------------|---------------|----------------|
| Butula       | Idadi  | 27              | 26            | 07                    | 13            | 07             |
|              | Asilimia   | 33.75%          | 32.5%         | 8.75%                 | 16.25%        | 8.75%          |
| Mundika      | Idadi  | 18              | 34            | 15                    | 10            | 03             |
|              | Asilimia   | 22.5%           | 42.5%         | 18.75%                | 12.5%         | 3.75%          |
| Amukura      | Idadi  | 11              | 27            | 23                    | 16            | 03             |
|              | Asilimia   | 13.75%          | 33.75%        | 28.75%                | 20%           | 3.75%          |
| Kisoko       | Idadi  | 36              | 27            | 08                    | 08            | 01             |
|              | Asilimia   | 45%             | 33.75%        | 10%                   | 10%           | 1.25%          |
| Chakol       | Idadi  | 43              | 21            | 02                    | 14            | 00             |
|              | Asilimia   | 53.75%          | 26.25%        | 2.5%                  | 17.5%         | 00%            |
| Lwanya       | Idadi  | 33              | 26            | 09                    | 11            | 01             |
|              | Asilimia   | 41.25%          | 32.5%         | 11.25%                | 13.75%        | 1.25%          |
| Makunda      | Idadi  | 24              | 16            | 31                    | 07            | 02             |
|              | Asilimia   | 30%             | 20%           | 38.75%                | 8.75%         | 2.5%           |
| <b>Jumla</b> | <b>Idadi</b>   | <b>192</b>      | <b>177</b>    | <b>95</b>             | <b>79</b>     | <b>17</b>      |
|              | <b>Asilimia</b>                                      | <b>34.29%</b>   | <b>31.61%</b> | <b>16.96%</b>         | <b>14.11%</b> | <b>3.03%</b>   |

Kwa mujibu wa jedwali 3.15. Asilimia 65.9 ya wanafunzi kutoka shule saba za utafiti walionyesha mielekeo chanya kuhusu usomaji wa vitabu vya hadithi na magazeti kwa lugha ya Kiswahili. Mtafiti aligundua kuwa, kuna baadhi ya shule ambazo zimetenga siku ili kusoma vitabu na magazeti. Katika shule ya Upili ya Lwanya, kuna kipindi kimoja ambacho kimetengewa somo la maktaba. Wanafunzi husoma vitabu teule vya hadithi au magazeti. Katika shule ya Upili ya Chakol kila Jumapili saa kumi jioni kila mwanafunzi anafaa kusoma vitabu vya fasihi andishi. Kupitia mijadala elekezi wa vikundi, mtafiti aliwauliza wanafunzi swali lifuatalo, *Taja umuhimu wa kusoma vitabu vya hadithi na magazeti ya lugha ya Kiswahili shuleni.*

Mtafiti alibaini kuwa, wanafunzi hufurahia siku hizi kwa sababu huweza kuimarisha ujuzi wao katika somo la Kiswahili. Misamiati wanayoipata huwasaidia katika uandishi wa insha. Vilevile, usomaji wa magazeti huwasaidia wanafunzi kujibu swali la pili la insha ambalo huhusu maswali ibuka. Mielekeo chanya kuhusiana na usomaji wa vitabu na magazeti pia imechangiwa na ripoti ya KNEC (2019), inayosema kuwa, wanafunzi wanahimizwa kusoma kwa mapana na kwa kina magazeti, majarida, kazi za fasihi na vitabu katika nyanja anuwai. Hii humfahamisha mwanafunzi kuhusu matukio ya kila siku katika jamii na mazingira yao, kitaifa na pia kimataifa. Hili litapalilia ubunifu wao na kuwawezesha kumudu maswali yanayohusu maswala ibuka iwapo yatatahiniwa. Asilimia 16.96 ya wanafunzi kutoka shule saba za utafiti katika Kaunti ya Busia hawakuonyesha mwelekeo wowote. Wanafunzi hawa walisema kuwa hawajawahi kuomba vitabu au magazeti kutoka kwa maktaba ya shule au mwalimu wa somo la Kiswahili.

Hata hivyo, mtafiti aligundua kuwa, asilimia 17.14 ya wanafunzi walioonyesha mielekeo hasi kuhusu usomaji wa vitabu vya hadithi na magazeti. Mielekeo hasi ni kutokana na kulazimishwa na walimu wa somo la Kiswahili kusoma magazeti na vitabu hivi. Mwanafunzi asiyesoma magazeti au vitabu vya Kiswahili huadhibiwa. Isitoshe, utafiti ulibaini kuwa, katika shule ya Upili ya Mundika, Magazeti ambayo hununuliwa ni ya lugha ya Kiingereza tu hivyo kuchangia mielekeo hasi dhidi ya lugha ya Kiswahili.

Kulingana na utafiti wa Babusa (2010), matokeo ya utafiti wake yalionyesha kuwa, kusoma riwaya, magazeti na majarida ya Kiswahili yanazidisha umilisi wao wa lugha ya Kiswahili. Hii huchangia wanafunzi hawa kuwa na mielekeo chanya kuhusu shughuli za aina hii kwa kuwa zitawafaidi katika somo la Kiswahili.

### **3.2 Uchanganuzi wa mielekeo ya walimu kuhusu kanuni za lugha shuleni**

Mielekeo ya walimu kuhusu kanuni za lugha za shule ni muhimu katika utafiti huu kwa sababu mielekeo yao huathiri pia mielekeo ya wanafunzi (Onyango, 2008). Katika nadharia ya Ajzen na Fishbein (1980) ya vitendo vilivyofikiriwa katika mhimili wa pili, anasema kuwa, nia ya mtu hutathminiwa na nia yake binafsi na ushawishi kutoka kwa jamii. Katika utafiti huu, walimu ni wanajamii, hivyo mielekeo yao kuhusu kanuni hizi itaathiri pia mielekeo ya wanafunzi wa shule za upili kuwa chanya au hasi.

Katika sura hii, matokeo ya uchanganuzi wa hojaji likati yalionyeshwa kwa kurejelea kauli 14 ambazo zililenga kubainisha mielekeo ya walimu kuhusu kanuni za lugha za shule. Kauli hizi zote zilikuwa na majibu ya kuchagua matatu ambayo yalikuwa: Kauli ya Nakubali ilionyesha mielekeo chanya ilhali Nakataa ilionyesha mielekeo hasi.

Utafiti huu ulilenga mwalimu mmoja ambaye ni mkuu wa idara ya Kiswahili kutoka kila shule saba teule. Idadi hiyo ikawa wakuu wa idara ya Kiswahili saba. Hojaji hizi zilijazwa na kurejeshwa kwa mtafiti. Ili kubainisha mielekeo ya walimu hawa kuhusiana na kanuni za lugha shuleni, majibu kutoka kwenye hojaji likati na mahojiano ya moja kwa moja kati ya mtafiti na mkuu wa idara ya Kiswahili yaliwasilishwa kwenye majedwali kama ifuatavyo:

#### **3.2.1. Lugha ya mawasiliano katika mazingira ya Shule**

Lugha ya mawasiliano katika shule za upili katika Kaunti ya Busia ni Kiswahili na Kiingereza. Lugha za kienyeji au kiasili na Sheng haziruhusiwi kuzungumzwa hasa katika mazingira ya shule. Kulingana na utafiti wa Wanjiku (2014), nusu ya walimu

katika eneo la Kapseret hutumia lugha sanifu wanapofunza au kuwasiliana katika mazingira ya shule. Walimu wengine huchanganya lugha ya Kiingereza na Kiswahili au hata hutumia Sheng. Hii hufanya wanafunzi kuiga kile ambacho walimu wao wanafanya. Aidha utafiti wa Kobia na Ndwiga (2013) ulionyesha kuwa, mielekeo hasi ya walimu kuhusu lugha ya Kiswahili husababisha mielekeo hasi ya wanafunzi kuhusu lugha hiyo. Mieleko chanya ya walimu kuhusu lugha pia huathiri mielekeo ya wanafunzi kuwa chanya. Ni kutokana na matokeo kama haya ambapo mtafiti alitaka kujua mielekeo ya walimu wa somo la Kiswahili kuhusu lugha ya Kiswahili kama lugha ya mawasiliano. Kauli zifuatazo ndizo zilizobainisha mielekeo ya walimu wa somo la Kiswahili.

**Jedwali 3.16 Mimi huwasiliana na walimu wenzangu kwa lugha ya Kiswahili shuleni**

| Shule           | Mimi huwasiliana na walimu wenzangu kwa lugha ya Kiswahili nikiwa shuleni | Nakubali      | Sikubali wala sikatai | Nakataa   |
|-----------------|---|---------------|-----------------------|-----------|
| Butula          |   | 1             | 0                     | 0         |
| Mundika         |   | 1             | 0                     | 0         |
| Amukura         |   | 0             | 1                     | 0         |
| Kisoko          |   | 1             | 0                     | 0         |
| Chakol          |   | 1             | 0                     | 0         |
| Lwanya          |   | 1             | 0                     | 0         |
| Makunda         |   | 0             | 1                     | 0         |
| <b>Jumla</b>    |   | <b>5</b>      | <b>2</b>              | <b>0</b>  |
| <b>Asilimia</b> |   | <b>71.43%</b> | <b>28.57%</b>         | <b>0%</b> |

Kulingana na jedwali 3.16, Asilimia 71.4 ya wakuu wa idara ya Kiswahili wanapenda kuwasiliana na walimu wengine kwa lugha ya Kiswahili ili wawe mfano mwema wa kuigwa, si kwa walimu tu bali pia wanafunzi. Ili kuibua habari zaidi, mtafiti kupitia mahojiano aliwauliza, *Eleza sababu ya kuwasiliana na walimu wenzako kwa lugha ya Kiswahili ukiwa shuleni.* Mkuu wa idara katika shule ya

Upili ya Mundika alisema kuwa, wanafunzi huiga kile ambacho mwalimu anafanya. Kwa hivyo, anapowasiliana na walimu wenzake katika lugha ya Kiswahili, wanafunzi pia watawaiga. Aidha mwalimu wa somo la Kiswahili anapojivunia kuzungumza lugha ya Kiswahili na wenzake, huwa motisha kwa walimu wa masomo mengine. Walimu hawa hubadilisha mielekeo yao kuhusu lugha ya Kiswahili. Asilimia 28.57 ya walimu wa Kiswahili hawakuonyesha mwelekeo wowote. Walimu hawa hutumia lugha yoyote kutegemea ni nani ambaye wanazungumza naye. Inaweza kuwa Kiingereza, Kiswahili au hata lugha asili au kienyeji.

Mtafiti pia alitaka kujua kutoka kwa walimu wa somo la Kiswahili, kando na mazingira ya nje ya darasa, ni lugha gani ambayo wao hutumia wanapofundisha somo la Kiswahili;

**Jedwali 3.17 Mimi hufundisha kwa lugha sanifu ya Kiswahili**

| <b>Shule</b>    | <b>Mimi hufundisha kwa lugha sanifu ya Kiswahili</b> | <b>Nakubali</b> | <b>Sikubali wala sikatai</b> | <b>Nakataa</b> |
|-----------------|--|-----------------|------------------------------|----------------|
| Butula          |  | 1               |                              | 0              |
| Mundika         |  | 1               |                              | 0              |
| Amukura         |  |                 | 1                            | 0              |
| Kisoko          |  | 1               |                              | 0              |
| Chakol          |  | 1               |                              | 0              |
| Lwanya          |  | 1               |                              | 0              |
| Makunda         |  |                 | 1                            | 0              |
| <b>Jumla</b>    |  | <b>5</b>        | <b>2</b>                     | <b>0</b>       |
| <b>Asilimia</b> |  | <b>71.43%</b>   | <b>28.57%</b>                | <b>0</b>       |

Kulingana na jedwali la 3.17, utafiti ulionyesha kuwa, kati ya walimu saba waliohojiwa, tano (71.43%) hufundisha kwa lugha sanifu hivyo kuonyesha mwelekeo chanya kuwasiliana kwa lugha ya Kiswahili. Mtafiti kupitia njia ya mahojiano aliwauliza swali lifuatalo, *Eleza sababu ya kufundisha kwa lugha sanifu*

ya Kiswahili. Walimu hawa walisema kuwa, mwanafunzi huiga kile ambacho mwalimu wake anafanya. Hivyo basi, unapotaka mwanafunzi azungumze lugha sanifu na awe na mwelekeo chanya, kama mwalimu ni sharti uwe kielelezo bora kwao. Aidha mwanafunzi hujifunza misamiati bora kutoka kwa mwalimu na kuitumia katika uandishi wake hasa karatasi la kwanza ambalo ni la insha. Walimu wawili hawakuonyesha ikiwa wanapenda au hawapendi kutumia lugha sanifu wanapofundisha. Walimu hawa walisema kuwa, kuna wakati ambao wao husahau msamiati mwafaka wa kurejelea kitu fulani. Hivyo, huwabidi kutohoa neno la Kiingereza au kuchanganya lugha ili wanafunzi waweze kuelewa kiurahisi. Walisema kuwa, Kiswahili kina misamiati michache hasa ukirejelea vitu vinavyobuniwa. Kile wanachosahau walimu hawa ni kuwa, wanafunzi wataiga tabia hii ya kutohoa maneno katika mawasiliano na hata uandishi wao.

Mtafiti aidha alitaka kujua maoni ya walimu wa somo la Kiswahili kuhusu lugha ya Kiswahili kama lugha ya mawasiliano ya kila siku shuleni. Majibu ya kauli hii yaliwekwa kwenye jedwali kama ifuatavyo.

**Jedwali 3.18 Lugha ya Kiswahili inafaa kuwa lugha ya mawasiliano ya kila siku shuleni**

| Shule           | Lugha ya Kiswahili inafaa kuwa lugha ya mawasiliano ya kila siku shuleni | Nakubali      | Sikubali wala sikatai | Nakataa  |
|-----------------|--|---------------|-----------------------|----------|
| Butula          |  | 1             |                       | 0        |
| Mundika         |  | 1             |                       | 0        |
| Amukura         |  | 1             |                       | 0        |
| Kisoko          |  |               | 1                     | 0        |
| Chakol          |  |               | 1                     | 0        |
| Lwanya          |  | 1             |                       | 0        |
| Makunda         |  | 1             |                       | 0        |
| <b>Jumla</b>    |  | <b>5</b>      | <b>2</b>              | <b>0</b> |
| <b>Asilimia</b> |  | <b>71.43%</b> | <b>28.57%</b>         | <b>0</b> |

Kulingana na majibu ya jedwali hili, utafiti ulibaini kuwa asilimia 71.43 ya wakuu wa idara ya Kiswahili wangependa sana lugha ya mawasiliano iwe Kiswahili. Kupitia njia ya mahojiano na wakuu wa idara ya Kiswahili alipouliza swali, *Fafanua umuhimu wa lugha ya Kiswahili kuwa lugha ya mawasiliano shuleni*. Wakuu wa idara walioonyesha mwelekeo chanya walisema kuwa, lugha ya Kiswahili ni lugha rasmi na ya taifa, hivyo ni vizuri ikiwa wanafunzi wataizungumza kila siku shuleni. Matokeo haya yawiana na ya Mirianga (2014), ambaye anasema kuwa, asilimia kubwa ya walimu walionyesha mielekeo chanya kuhusu matumizi ya Kiswahili kama lugha rasmi katika mazingira rasmi. Walimu waliohojiwa walionyesha mielekeo chanya kuhusu dhima ya Kiswahili kama lugha ya taifa na rasmi nchini Kenya. Walimu wa somo la Kiswahili walisema kuwa, wananchi wengi hutumia lugha hii katika kufanikisha mawasiliano yao, hivyo ni bora ikitumiwa katika mawasiliano. Katika shule za Kitaifa na zaidi ya Kaunti, Kiswahili kama lugha ya taifa huwaunganisha wanafunzi kutoka sehemu mbalimbali ikilinganishwa na lugha za kigeni. Pia, wanachangia kwa kusema kuwa, kukiwa na mikutano ya wazazi au wageni shuleni, lugha ya matumizi huwa Lugha ya Kiswahili, hivyo hawaoni ni sababu gani mwanafunzi kushurutishwa kuwasiliana tu kwa lugha ya Kiingereza. Asilimia 28.57 ya walimu wa somo la Kiswahili wanakataa kauli hii. Kwa mfano maoni ya mkuu wa idara katika shule ya upili ya Chakol ni kuwa, ikiwa wanafunzi watakubaliwa kuzungumza tu Kiswahili, wataathirika katika masomo yanayotahiwa kwa lugha ya Kiingereza. Aidha ajira nyingi zinamhitaji mwanafunzi kujieleza vyema kwa lugha ya Kiingereza, na ikiwa mwanafunzi atakubaliwa tu kuzungumza kwa lugha ya Kiswahili, ujuzi wake kwa lugha ya Kiingereza utaathirika. Ikumbukwe kuwa, walimu hawa pia hufunza masomo mengine kando na somo la Kiswahili. Hii pia inaweza kuwa sababu ya kuchangia mielekeo hasi dhidi ya

kutokubaliana na lugha ya mawasiliano kuwa Kiswahili tu. Matokeo ya utafiti wa Ogolla (1990), yalionyesha kuwa, taasisi muhimu katika uchipukaji wa mielekeo kuhusu lugha ni ile ya elimu. Katika mazingira ya elimu ya msomi, lugha ya Kiingereza ndiyo lugha inayosisitizwa sana, hivyo basi, watu ambao wamepitia taasisi hii huwa na mielekeo fulani kuhusu mambo yanayozingatiwa katika elimu. Mitazamo hii ya kuiona lugha ya Kiingereza kuwa muhimu katika taasisi ya elimu pia imeshuhudiwa kupitia baadhi ya wakuu wa idara ya Kiswahili katika shule za Upili kaunti ya Busia.

### 3.2.2 Siku za Kiswahili

Utafiti wa awali katika shule teule saba, ulionyesha kuwa, Shule ya Upili ya Mundika na Shule ya Upili ya Kisoko, zimepiga marufuku mawasiliano kwa lugha ya Kiswahili ingawa kuna siku moja katika muhula ambapo wanafunzi huruhusiwa kutekeleza shughuli zote za siku kwa lugha ya Kiswahili. Shule za Upili za Lwanya, Chakol, Butula na Makunda wana siku tatu kwa wiki za kuwasiliana kwa lugha ya Kiswahili. Katika shule ya upili ya Amukura wako huru kuwasiliana kwa lugha ya Kiswahili. Hivyo, mtafiti alitaka kujua mwelekeo wa wakuu wa idara ya Kiswahili hasa kuhusu kanuni hii ya lugha.

**Jedwali 3.19 Siku za Kiswahili shuleni zina manufaa**

| Shule           | Siku za Kiswahili shuleni zina manufaa | Nakubali    | Sikubali wala sikatai | Nakataa  |
|-----------------|--|-------------|-----------------------|----------|
| Butula          |  | 1           | 0                     | 0        |
| Mundika         |  | 1           | 0                     | 0        |
| Amukura         |  | 1           | 0                     | 0        |
| Kisoko          |  | 1           | 0                     | 0        |
| Chakol          |  | 1           | 0                     | 0        |
| Lwanya          |  | 1           | 0                     | 0        |
| Makunda         |  | 1           | 0                     | 0        |
| Jumla           |  | 7           | 0                     | 0        |
| <b>Asilimia</b> |  | <b>100%</b> | <b>0</b>              | <b>0</b> |

Asilimia 100 ya walimu wa somo la Kiswahili wana mielekeo chanya kuhusu siku za Kiswahili shuleni. Hii ni kwa sababu, hii ndio siku ambayo lugha ya Kiswahili hupeleleka nafasi ya kutumiwa katika mawasiliano katika mazingira ya shule. Siku hii humpa mwalimu fursa ya kutambua magwiji wa lugha kupitia namna wanavyowasilisha habari kwenye gwaride na katika mawasiliano yao ya kawaida na wanafunzi wengine. Mtafiti pia alitambua kuwa, katika shule ya Upili ya Chakol, Lwanya, Makunda na hata Butula ni sheria kwa kila mwalimu, awe wa somo la Kiswahili au la kuwahutubia wanafunzi kwa lugha ya Kiswahili sanifu kwenye gwaride. Walimu wakuu katika shule hizi huwa mstari wa kwanza kuhutubu kwa lugha sanifu ya Kiswahili. Jambo hili huinua hadhi ya lugha ya Kiswahili, kwa hivyo mielekeo chanya ya walimu huchangia mielekeo chanya ya wanafunzi.

Ingawa sheria hii inatekelezwa katika shule nyingi, kuna baadhi ya shule ambapo walimu wa masomo mengine hutoa hotuba kwa lugha ya Kiingereza. Hii huchangia mwelekeo hasi kwa wanafunzi.

Matokeo ya utafiti ya watafiti kama Dell Hymes (1966) yalionyesha kuwa, wanafunzi hujifunza lugha zaidi kwa kuitumia lugha hiyo. Katika shule ya upili ya Amukura, kila siku ni siku ya kuwasiliana kwa lugha ya Kiswahili. Walimu katika shule hii walisema kuwa, idadi kubwa ya wanafunzi katika shule hii ni Wateso ambayo si lugha ya Kibantu, hivyo wanaamini kuwa, ili mwanafunzi aweze kujifunza na kuipenda lugha ya Kiswahili, ni bora ikiwa ataizungumza kila siku. Kulingana na utafiti wa Okwany (1993), wanafunzi wenye asili ya makabila ya Kibantu walionyesha mielekeo chanya zaidi kushinda wale wenye asili isiyo ya Kibantu. Kwa hivyo, itakuwa bora wakiwasiliana kwa lugha ya Kiswahili.

### 3.2.3 Mabango na maandishi katika mazingira ya shule

Kulingana na kamusi ya Kiswahili sanifu (2004), bango ni karatasi gumu au kadi kubwa lenye matangazo au ujumbe maalumu. Koko (2016), anasema kuwa, mabango haya na maandishi huandikwa ili kuelimisha, kuelekeza na kushauri wapita njia na wanafunzi mambo muhimu wanapaswa kuyafanya. Katika shule za upili Kaunti ya Busia, kuna mabango na maandishi tofauti yanayohusu lugha na masomo mengine. Mtafiti alipotembelea Idara ya Kiswahili, alitaka kujua mwelekeo wa wakuu wa idara ya Kiswahili kuhusu mabango na maandishi yaliyokuwa shuleni. Kupitia njia ya uchunzaji, mtafiti alibaini kuwa, mabango na maandishi mengi ni kwa lugha ya Kiingereza. Hivyo, mtafiti akataka kujua mwelekeo wao kuhusu mabango haya pamoja na maandishi katika mazingira ya shule. Kauli iliojazwa ni;

#### Jedwali 3.20 Mabango na maandishi yaliyo katika mazingira ya shule yana manufaa

| Shule           | Mabango na maandishi yaliyo katika mazingira ya shule yana manufaa | Nakubali      | Sikubali wala sikatai | Nakataa       |
|-----------------|--|---------------|-----------------------|---------------|
| Butula          |  | 0             |                       | 1             |
| Mundika         |  | 1             | 0                     | 0             |
| Amukura         |  | 0             | 1                     | 0             |
| Kisoko          |  | 1             | 0                     | 0             |
| Chakol          |  | 1             | 0                     | 0             |
| Lwanya          |  | 0             | 0                     | 1             |
| Makunda         |  | 0             | 0                     | 1             |
| <b>Jumla</b>    |  | <b>3</b>      | <b>1</b>              | <b>3</b>      |
| <b>Asilimia</b> |  | <b>42.86%</b> | <b>14.28%</b>         | <b>42.86%</b> |

Katika hojaji waliyopewa walimu wa somo la Kiswahili, utafiti ulibaini kuwa, asilimia 42.86% ya walimu wana mielekeo chanya kuhusu mabango haya. Katika shule ya Upili ya Chakol, Kisoko na Mundika kuna maandishi yanayowahimiza wanafunzi kutumia lugha sanifu na ubao wa matangazo ambapo insha za wanafunzi bora huwekwa.

Kupitia njia ya mahojiano walipoulizwa swali, *Eleza umuhimu wa mabango na maandishi yaliyo katika mazingira ya shule*. Wakuu wa idara ya Kiswahili walisema kuwa, maandishi kama haya yanachangia mielekeo chanya kuhusu lugha ya Kiswahili. Mfano kielelezo 1.3 katika shule ya Upili ya Chakol, kinasisitiza matumizi ya lugha sanifu na kuepuka sheng'. Mkuu wa idara katika shule ya Upili ya Amukura hakuonyesha mwelekeo wowote. Alisema kuwa, haoni ikiwa mabango haya yakiathiri mwelekeo wa wanafunzi kuhusu somo la Kiswahili. Asilimia 42.86 ya walimu wa somo la Kiswahili wana mielekeo hasi dhidi ya mabango haya kwa sababu yanachangia mielekeo hasi dhidi ya lugha ya Kiswahili. Mabango na maandishi hutukuza tu lugha ya Kiingereza na masomo mengine. Mkuu wa idara katika shule ya mseto ya Makunda alisema kuwa, juhudi za kumtaka mwalimu mkuu kuleta mabango yanayokitukuza somo la Kiswahili zimeambulia patupu. Jambo hili limesababisha mielekeo ya wanafunzi na walimu kuwa hasi kwa sababu hawawezi kuwa na mielekeo chanya kwa kile wasichokiona wala kukisoma katika mazingira yao.

#### **3.2.4 Matumizi ya lugha ya Kiswahili katika mijadala shuleni**

Katika kamusi ya Kiswahili sanifu (2004), mijadala ni mazungumzo juu ya jambo maalumu yanayofanywa kwa kutolea hoja kuhusu jambo hilo. Matokeo ya utafiti yalionyesha kuwa, kuna siku ya mijadala katika shule saba teule. Mtafiti pia alipata fursa ya kushiriki katika baadhi ya mijadala inayoendeshwa katika shule za Upili. Ili kubaini mielekeo ya walimu wa somo la Kiswahili kuhusu uhudhuriaji wa mijadala hii. Swali ambalo mtafiti aliuliza ni;

**Jedwali 3.21 Mimi huhudhuria siku za mijadala kwa lugha ya Kiswahili**

| <b>Shule</b>    | <b>Mimi huhudhuria siku za mijadala kwa lugha ya Kiswahili</b> | <b>Nakubali</b> | <b>Sikubali wala sikatai</b> | <b>Nakataa</b> |
|-----------------|--|-----------------|------------------------------|----------------|
| Butula          |  | 1               |                              | 0              |
| Mundika         |  | 1               |                              | 0              |
| Amukura         |  |                 | 1                            | 0              |
| Kisoko          |  | 1               |                              | 0              |
| Chakol          |  | 1               |                              | 0              |
| Lwanya          |  | 1               |                              | 0              |
| Makunda         |  |                 | 1                            | 0              |
| Jumla           |  | 5               | 2                            | 0              |
| <b>Asilimia</b> |  | <b>71.43%</b>   | <b>28.57%</b>                | <b>0</b>       |

Matokeo ya utafiti kulingana na jedwali 3.21 yalionyesha kuwa, asilimia 71.43 ya wakuu wa idara ya Kiswahili wanapenda kuhudhuria mijadala kwa lugha ya Kiswahili. Kupitia njia ya mahojiano, walimu hawa walipoulizwa swali, *Taja sababu za kuhudhuria siku za mijadala kwa lugha ya Kiswahili*. Walisema kuwa, mijadala humsaidia mwanafunzi katika uandishi wa insha. Walimu wa somo la Kiswahili wanapohudhuria, huwaelekeza wanafunzi namna ya kueleza hoja zao na wanapopungukiwa hoja walimu hawa huwaongeza hoja. Pia humsaidia mwalimu kuwarekebisha wanafunzi wanapofanya makosa ya kisarufi. Mkuu wa idara ya Kiswahili katika shule ya upili ya Lwanya alisema kuwa, anapohudhuria siku ya mijadala, huwapa wanafunzi motisha ya kuzungumza kwa lugha sanifu. Makosa wanayofanya si ya kusudia ikilinganishwa na ile mijadala inayoendeshwa tu na wanafunzi. Asilimia 28.57 ya walimu hawakuonyesha mwelekeo wowote. Walimu hawa walisema kuwa, ingawa kuhudhuria mijadala ni muhimu sana, wakati wa mijadala huwa jioni wanapojitayarisha kuondoka kwenda nyumbani. Hivyo huwa vigumu kuhudhuria kila wakati. Katika shule ya Upili ya Makunda, walimu wengi wanaishi nje ya shule, hivyo kuwa vigumu kuhudhuria hasa baada ya vipindi kuisha.

Katika shule za bweni, walimu wengi wanaishi ndani ya shule, hivyo ni rahisi kuhudhuria mijadala hii.

### **3.2.5 Shughuli za idara ya Kiswahili**

Kulingana na Sunnarbog (2002), ili kubadilisha mielekeo ya wanafunzi, walimu wana jukumu la kupeana nyenzo ambazo zitasababisha mielekeo hasi ya wanafunzi kubadilika. Katika utafiti huu, idara ya Kiswahili katika shule za upili imepewa jukumu la kubuni njia tofauti katika idara hii ili kubadilisha mielekeo ya wanafunzi kuhusu somo la Kiswahili. Mtafiti alipotembelea Idara ya Kiswahili, kupitia mbinu ya uchunzaji, aliweza kupata habari ya shughuli za idara ya Kiswahili katika kumbukumbu za mikutano na ratiba iliyowekwa kwa afisi ya idara. Shughuli za idara ya Kiswahili ziliweza kubainishwa. Shughuli hizi ni kama, vipindi vya ziada, makongamano ya ndani na nje ya shule, usomaji wa vitabu na magazeti ya shule pamoja na vyama vya Kiswahili shuleni.

#### **3.2.5.1 Vipindi vya ziada**

Kulingana na sera ya Wizara ya Elimu, mtaala wa Kiswahili una vipindi vitano katika kidato cha kwanza na cha pili, ilihali kidato cha tatu na cha nne una vipindi sita kila wiki. Kimaro (2013), katika utafiti wake anasema kuwa, Kiswahili kimepewa vipindi vichache katika ratiba ya Shule ilhali silabasi ya Somo la Kiswahili ni pana. Wakuu wa idara ya Kiswahili katika shule saba zilizofanyiwa utafiti walikubaliana na utafiti huu kuwa silabasi ya Kiswahili ni pana na muda huo uliopewa hautoshi kushughulikia kila kipengele katika silabasi. Ni kutokana na matokeo kama haya, ambapo shule za upili zimebuni njia mwafaka ya kumaliza silabasi ya Somo la Kiswahili kwa kuongeza vipindi vya ziada. Kwa hivyo mtafiti

aliuliza kauli zifuatazo kwa mkuu wa idara ili kuchunguza mielekeo yao kuhusu vipindi vya ziada,

**Jedwali 3.22 Vipindi vya ziada shuleni mwetu vina manufaa**

| <b>Shule</b>    | <b>Vipindi vya ziada shuleni mwetu vina manufaa</b> | <b>Nakubali</b> | <b>Sikubali wala sikatai</b> | <b>Nakataa</b> |
|-----------------|---|-----------------|------------------------------|----------------|
| Butula          |   | 1               | 0                            | 0              |
| Mundika         |   | 1               | 0                            | 0              |
| Amukura         |   | 0               | 1                            | 0              |
| Kisoko          |   | 1               | 0                            | 0              |
| Chakol          |   | 1               | 0                            | 0              |
| Lwanya          |   | 1               | 0                            | 0              |
| Makunda         |   | 0               | 1                            | 0              |
| Jumla           |   | 5               | 2                            | 0              |
| <b>Asilimia</b> |   | <b>71.43%</b>   | <b>28.57%</b>                | <b>0</b>       |

Kwa mujibu wa Jedwali 3.22, Asilimia 71.43 wanapenda vipindi vya ziada vya somo la Kiswahili hivyo kuonyesha mielekeo chanya. Mielekeo hii chanya ni kwa sababu vipindi hivi husaidia katika kumaliza silabasi pana ya Somo la Kiswahili na baadaye kuanza kufanya marudio ya vipengele vigumu. Katika shule ya Upili ya Butula, Mundika, Kisoko, Chakol na Lwanya, mtafiti aligundua kuwa, vipindi hivi hulipiwa. Hii ni njia moja ya kuwapa walimu motisha ya kufunza vipindi hivi. Asilimia 28.57 hawakuonyesha mwelekeo wowote. Walimu hawa walisema kuwa, ingawa vipindi vya ziada vina manufaa, kufika shuleni mapema kunahitaji motisha na ufadhili kutoka kwa kwa mamlaka ya shule, jambo ambalo huwa halitekezwi. Pia vipindi hivi hundeshwa wakati mwingine jioni, hivyo walimu wanaoishi mbali na shule kuwa vigumu kwao kufunza, hivyo kufanya mielekeo ya walimu kuwa hasi.

Makongamano ndani na nje ya shule pia ni shughuli za idara ambazo huendelezwa. Hivyo mtafiti alitaka kujua mwelekeo wa walimu wa somo la Kiswahili kuhusiana na shughuli hizi.

### 3.2.5.2 Makongamano ya ndani na nje ya shule

Makongamano ni mjadala juu ya jambo fulani yanayofanywa na mkusanyiko wa watu kama vile mkutano, warsha; kongamano la kitaifa (Kamusi sanifu 2004). Ili kujua mielekeo ya wakuu wa idara ya Kiswahili kuhusu makongamano haya, maswali ya utafiti yafuatayo yaliulizwa;

#### Jedwali 3.23 Mimi huhudhuria makongamano ya nje ya shule

| Shule           | Mimi huhudhuria makongamano ya nje ya shule | Nakubali    | Nakataa  |
|-----------------|---|-------------|----------|
| Butula          |   | 1           | 0        |
| Mundika         |   | 1           | 0        |
| Amukura         |   | 1           | 0        |
| Kisoko          |   | 1           | 0        |
| Chakol          |   | 1           | 0        |
| Lwanya          |   | 1           | 0        |
| Makunda         |   | 1           | 0        |
| <b>Jumla</b>    |   | <b>7</b>    | <b>0</b> |
| <b>Asilimia</b> |   | <b>100%</b> | <b>0</b> |

Asilimia 100% ya wakuu wa idara ya Kiswahili kutoka shule saba teule wanapenda kuhudhuria makongamano ya nje ya shule hivyo kuonyesha mielekeo chanya. Walipoulizwa kupitia mahojiano, *Eleza umuhimu wa makongamano ya nje ya shule.* Wakuu wa idara ya Kiswahili walisema kuwa, makongamano haya ni muhimu kwa mwalimu kwa sababu humpa fursa ya kutangamana na kubadilishana mawazo na walimu kutoka shule zingine. Mara nyingi makongamano haya hujumuisha wanafunzi kutoka shule za kitaifa, za zaidi ya Kaunti, Kaunti na hata Kaunti ndogo hivyo walimu na wanafunzi wanapata nafasi ya kubadilishana mawazo na mitindo ya kufunza wanapotangamana.

Ingawa utafiti huu ulinuia kuchunguza makongamano yanayohusu wanafunzi na walimu, ilibainika kuwa, kando na makongamano ya nje ya shule yanayowahusu wanafunzi na walimu, kuna makongamano ambayo huandaliwa kwa walimu wa somo la Kiswahili pekee ambayo hupendwa na walimu wa somo la Kiswahili. Mielekeo chanya ya walimu ni kutokana na umuhimu wa makongamano ya aina hii. Kwa mujibu wa uchunguzi wa Moseti (2003), Maandalizi bora ya mapema huwezesha kufanikiwa au kufaulu kwa mpango au mradi wowote. Shughuli hizi hupanua uwezo wa mwalimu wa kuifasiri silabasi na hata utendaji halisi darasani. Kwa mfano Kielelezo cha 1.5. Makongamano haya hushughulikia ufundishaji, utahini na usahihishaji wa mitihani. Hii humpa mwalimu ujuzi wa kuimarisha somo la Kiswahili. Wakuu wa idara kutoka shule teule saba walikubaliana kuwa, makongamano ya aina hii huimarisha ujuzi wao kuhusu somo la Kiswahili. Ingawa makongamano haya yanapendwa, walimu wengine waliohojiwa walisema kwamba hawajawahi kupata mawasiliano yoyote kuhusu shughuli za kitaaluma kama vile semina, warsha na makongamano kuhusu ufundishaji wa maswala ibuka yatakayowasaidia kubadilisha mielekeo ya wanafunzi wao. Hali hii inaonyesha udhaifu katika maandalizi ya walimu nyanjani jambo ambalo linaathiri mielekeo yao kuwa hasi. Matokeo ya Utafiti wa Aluoch (2018) yalionyesha kuwa, wizara ya elimu haikuhusika katika kugharamia mafunzo yoyote ya somo la Kiswahili katika Kaunti ya Kisumu. Hali hii pia imebainika katika Kaunti ya Busia. Jambo hili linaonyesha udhaifu katika sekta ya wizara ya elimu kwa sababu wizara ya elimu ndiyo inayofaa kushughulikia mafunzo ya walimu ya kupiga msasa.

Aidha mtafiti pia alitaka kubaini mwelekeo wa wakuu wa idara ya Kiswahili kuhusu makongamano ya ndani ya shule. Kauli waliojibu ni;

**Jedwali 3.24 Mimi hushiriki katika makongamano ya ndani ya shule**

| <b>Shule</b> | <b>Mimi hushiriki katika makongamano ya ndani ya shule</b> | <b>Nakubali</b> | <b>Sikubali wala sikatai</b> | <b>Nakataa</b> |
|--------------|--|-----------------|------------------------------|----------------|
| Butula       |  | 1               | 0                            | 0              |
| Mundika      |  | 1               | 0                            | 0              |
| Amukura      |  | 0               | 1                            | 0              |
| Kisoko       |  | 1               | 0                            | 0              |
| Chakol       |  | 1               | 0                            | 0              |
| Lwanya       |  | 1               | 0                            | 0              |
| Makunda      |  | 0               | 1                            | 0              |
| Jumla        |  | 5               | 2                            | 0              |
| Asilimia     |  | 71.43%          | 28.57%                       | 0%             |

Kulingana na jedwali 3.24, asilimia 71.43 ya walimu wanapenda kushiriki katika makongamano ya ndani ya shule, hivyo kuonyesha mwelekeo chanya. Kupitia majojiano ya mtafiti na wakuu wa idara, swali alilowauliza ni, *Taja sababu za kushiriki katika makongamano ya ndani ya shule*. Wakuu wa idara ya Kiswahili walisema kuwa, siku hii huwapa fursa ya kutangamana na wanafunzi wao na kujibu maswali katika sehemu zinazowapa utata. Aidha wanafunzi hupata fursa ya kuonyesha ujuzi wao katika somo la Kiswahili. Wanafunzi bora katika vitengo mbalimbali huzawadiwa kama njia ya kuwapa motisha. Katika utafiti wa Nyongesa na wengineo (2022), Motisha huwafanya wanafunzi kupenda kanuni za lugha za shule. Wanasema kuwa, wanafunzi wanapozawadiwa kwa kuibuka washindi katika warsha za aina hii, huchangia wao kuwasiliana kwa lugha ya Kiswahili wakiwa shuleni. Asilimia 28.57 ya walimu hawakuonyesha mwelekeo wowote. Walimu kutoka shule za Upili za Amukura na Makunda walisema kuwa, ili kufanikisha shughuli ya aina hii, wanahitaji ufadhili kutoka kwa mamlaka ya shule. Ufadhili huu utasaidia pia kufadhili walimu na wanafunzi watakaoshiriki. Ufadhili huu ndio kikwazo kikuu katika shule hizi. Ni vigumu kupata ufadhili kutoka mamlaka ya shule hizi kutokana na kukosa uwezo wa kifedha.

Uso maji wa magazeti na vitabu vya hadithi kwa lugha ya Kiswahili pia ni shughuli muhimu katika idara ya Kiswahili. Mtafiti alitaka kujua mwelekeo wa mwalimu wa somo la Kiswahili kuhusiana na kanuni hii ya lugha shuleni.

### 3.2.5.3 Usomaji wa magazeti na vitabu vya hadithi kwa lugha ya Kiswahili

Katika shule za upili katika Kaunti ya Busia, ilitambuliwa kuwa, kuna shule ambazo huwa na kanuni ya kuhakikisha kuwa wanafunzi wanasoma magazeti na vitabu vya hadithi ili waimarishe ujuzi wao katika somo la Kiswahili. Walimu kama vielelezo bora kwa wanafunzi, mielekeo yao kuhusu usomaji wa magazeti na vitabu vya hadithi hivyo kuwa muhimu katika utafiti huu. Kwa hivyo kauli ya utafiti ambayo mtafiti aliuliza ni;

**Jedwali 3.25 Kuna manufaa katika usomaji wa magazeti na vitabu vya hadithi kwa lugha ya Kiswahili**

| Shule    | Kuna manufaa katika usomaji wa magazeti na vitabu vya kwa lugha ya Kiswahili | Nakubali | Sikubali wala sikatai | Nakataa |
|----------|--|----------|-----------------------|---------|
| Butula   |  | 1        | 0                     | 0       |
| Mundika  |  | 1        | 0                     | 0       |
| Amukura  |  | 1        | 0                     | 0       |
| Kisoko   |  | 1        | 0                     | 0       |
| Chakol   |  | 1        | 0                     | 0       |
| Lwanya   |  | 1        | 0                     | 0       |
| Makunda  |  | 1        | 0                     | 0       |
| Jumla    |  | 7        | 0                     | 0       |
| Asilimia |  | 100%     | 0                     | 0       |

Kwa mujibu wa jedwali 3.25, Mtafiti alibaini kuwa asilimia 100 ya walimu wa somo la Kiswahili walikubaliana kuwa, kuna manufaa katika kusoma magazeti na vitabu vya hadithi vya Kiswahili, hivyo kuonyesha mwelekeo chanya. Licha ya mwelekeo huu, mtafiti alibaini kuwa, kuna baadhi ya shule zinapenda kununua magazeti kwa lugha ya Kiingereza hivyo kumnyima mwalimu fursa ya kusoma gazeti la Kiswahili.

Jambo hili huchangia mielekeo hasi dhidi ya gazeti la Kiswahili hasa kwa wanafunzi ambao hutegemea shule iwanunulie gazeti. Aidha tabia hii imechangia mielekeo hasi kwa lugha ya Kiswahili hasa kwa walimu wanaofunza masomo mengine.

#### 3.2.5.4. Vyama vya Kiswahili

Chama ni kikundi cha watu walioungana pamoja kwa lengo la kutekeleza matakwa yao ya kisiasa, kiuchumi na kijamii (Kamusi sanifu 2004). Shughuli za idara pia hujumuisha vyama vya wanafunzi vya Kiswahili. Mwalimu hupewa jukumu la kuwaelekeza wanafunzi wanaojiunga na vyama hivi. Mtafiti alitaka kujua mwelekeo wa mkuu wa idara ambaye ni mwalimu wa Kiswahili kuhusu kanuni hii ya lugha. Swali alilouliza ni;

**Jedwali 3.26 Kuwepo kwa vyama vya Kiswahili shuleni vina manufaa**

| Shule           | Kuwepo kwa vyama vya Kiswahili shuleni vina manufaa | Nakubali      | Sikubali wala sikatai | Nakataa  |
|-----------------|---|---------------|-----------------------|----------|
| Butula          |   | 1             | 0                     | 0        |
| Mundika         |   | 0             | 0                     | 1        |
| Amukura         |   | 0             | 0                     | 1        |
| Kisoko          |   | 1             | 0                     | 0        |
| Chakol          |   | 1             | 0                     | 0        |
| Lwanya          |   | 1             |                       | 0        |
| Makunda         |   | 1             | 0                     | 0        |
| <b>Jumla</b>    |   | <b>5</b>      | <b>2</b>              | <b>0</b> |
| <b>Asilimia</b> |   | <b>71.43%</b> | <b>28.57%</b>         |          |

Asilimia 71.43 ya wakuu wa idara ya Kiswahili katika jedwali 3.26, walikubali kuwa wanapenda kuwepo katika vyama vya Kiswahili hivyo kuonyesha mwelekeo chanya kuhusiana na kuwepo kwa vyama hivi. Wakuu wa idara ya Kiswahili kupitia mahojiano walipoulizwa, *Orodhesha manufaa ya vyama vya Kiswahili*, walisema kuwa, vyama ni muhimu katika kuendeleza somo la Kiswahili na hata huimarisha vipawa vya wanafunzi katika kujieleza katika lugha sanifu ya Kiswahili. Matokeo

ya utafiti yalibaini kuwa, walimu huwaelekeza wanafunzi katika kuandika habari watakazosoma kwenye gwaride kwa kukosoa makosa ya sarufi na hijai. Pia hushirikiana na wanafunzi kuweka mikakati ambayo itasaidia kuimarisha somo la Kiswahili kama kuandaa mijadala, makongamano ya ndani na nje mwa shule. Aidha vyama hivi hujihusisha katika uandishi wa mashairi na insha na kuchapisha katika gazeti la taifa leo. Vyama hivi hufanya kazi ya idara ya Kiswahili kuwa rahisi. Asilimia 14.29 ya wakuu wa idara ya Kiswahili hawakuonyesha mwelekeo wowote. Walimu hawa walisema kuwa, ingawa vyama vya Kiswahili ni muhimu katika uimarishaji wa somo la Kiswahili, wao hukosa kuhudhuria vyama kwa sababu ya shughuli nyingi shuleni.

Katika kutangamana na wakuu wa idara ya Kiswahili, kando na shughuli za idara ya Kiswahili, mtafiti pia aliuliza maswali ambayo yalimsaidia katika utafiti kubainisha mielekeo ya walimu wa somo la Kiswahili kuhusu kanuni za lugha za shule kwa jumla. Maswali haya yalikuwa;

### **3.2.5.5 Uteuzi wa kanuni za lugha za shule**

Kulingana na Odeo (2007), anasema kuwa, silabasi iliopo ya Kiswahili haikuhusisha walimu wa somo la Kiswahili, hivyo akapendekeza kuwa, silabasi inapofanyiwa mageuzi wadau wote washirikishwe kikamilifu na majaribio yafanywe kabla haijatumwa shuleni. Walimu wanapohusishwa huchangia kwa njia chanya. Katika uteuzi wa kanuni za lugha za shule, hali ya kutoshirikisha walimu wa somo la Kiswahili pia imebainika kupitia tafiti zilizofanywa. Kwa mfano, Ndun'gu (2014) aligundua kuwa, katika sekta ya elimu, wakuu wa shule wameweka sheria ambazo zinabana matumizi ya lugha ya Kiswahili licha ya kuwa ni somo la lazima na la kutahiniwa. Wakuu hawa wa shule huteua kanuni hizi bila kumhusisha mwalimu wa

somo la Kiswahili. Hali hii huchangia mielekeo hasi. Kwa sababu hii, wakuu wa idara ya Kiswahili walijaza kauli ifuatayo;

**Jedwali 3.27 Nilihusishwa katika uteuzi wa kanuni za lugha shuleni**

| <b>Shule</b>    | <b>Nilihusishwa katika uteuzi wa kanuni za lugha shuleni</b> | <b>Nakubali</b> | <b>Sikubali wala sikatai</b> | <b>Nakataa</b> |
|-----------------|--|-----------------|------------------------------|----------------|
| Butula          |  | 1               |                              |                |
| Mundika         |  | 1               |                              |                |
| Amukura         |  | 1               |                              |                |
| Kisoko          |  |                 |                              | 1              |
| Chakol          |  |                 |                              | 1              |
| Lwanya          |  | 1               |                              |                |
| Makunda         |  |                 | 1                            |                |
| Jumla           |  | 4               | 1                            | 2              |
| <b>Asilimia</b> |  | <b>57.14%</b>   | <b>14.29%</b>                | <b>28.57%</b>  |

Kwa mujibu wa jedwali 3.27 Asilimia 57.14 ya wakuu wa idara ya Kiswahili walikubali kuwa walihusishwa katika uteuzi wa kanuni za lugha za shule. Jambo hili limechangia wao kuwa na mielekeo chanya kuhusu kanuzi hizi. Asilimia 14.29 ya wakuu wa idara ya Kiswahili hawakuitikia. Walimu hawa walisema kuwa, walipata sheria hizi zikitumika. Asilimia 28.57 ya wakuu wa idara ya Kiswahili walikataa kauli hii. Wanasema kuwa, mara nyingi mamlaka ya shule inapotaka kutunga sheria zinazodunisha somo la Kiswahili, walimu wa somo la Kiswahili huwa hawahusishwi. Sheria kama kupiga marufuku mawasiliano kwa lugha ya Kiswahili au Kiswahili kupewa siku chache za mawasiliano hutungwa bila wao kuhusishwa. Wao hutarajiwa tu kutekeleza yale ambayo yamepitishwa.

Mtafiti kupitia mahojiano ya ana kwa ana aliwauliza, *Eleza umuhimu wa kuhusishwa katika uteuzi wa kanuni za lugha za shule*. Mkuu wa idara ya Kiswahili katika shule ya upili ya Kisoko alisema kuwa, kupigwa marufuku kuwasiliana kwa lugha ya Kiswahili haikuchukuliwa vyema na walimu wa somo la Kiswahili. Jambo hili limechangia walimu kuwa na mielekeo hasi dhidi ya sheria hizi. Kwa hivyo, ingekuwa bora kabla ya sheria kama hizi kutungwa, walimu wa somo wahusishwe.

Mtafiti pia aligundua kuwa, katika shule ambazo walimu wa somo la Kiswahili walihusishwa katika uteuzi wa kanuni za lugha za shule, utekelezaji wake huwa ni jukumu la kila mwalimu. Wao hufurahia sana ikilinganishwa na shule ambazo mamlaka hutunga sheria bila kuwahusisha.

### **3.3 Hitimisho**

Katika sura hii, mtafiti alichunguza mielekeo ya wanafunzi na walimu kuhusu kanuni za lugha za shule. Matokeo ya utafiti yalionyesha kuwa, walimu na wanafunzi wa shule za upili katika kaunti ya Busia wana mielekeo chanya kuhusu kanuni za lugha za shule. Ingawa mielekeo yao ni chanya, matokeo pia yalionyesha kuwa, shule zilizohusishwa katika utafiti zilipendelea lugha ya Kiingereza. Kwa hivyo utafiti huu unapendekeza kuwa na mabadiliko katika kanuni za lugha ili kuipa Kiswahili nafasi sawa na Kiingereza katika mawasiliano shuleni. Mabadiliko haya yatabadilisha mielekeo ya wanafunzi kuwa chanya.

Katika hali ya mtafiti kutangamana na walimu wa somo la Kiswahili, walimu hawa walisema kuwa, iwapo kila mwalimu atazingatia kanuni za lugha za shule, watakuwa kielelezo bora kwa wanafunzi na bila shaka watakuwa na mielekeo chanya. Wanasema kuwa, kanuni hizi ni muhimu sana kwa sababu huwaelekeza

wanafunzi katika matumizi yao ya lugha wakiwa shuleni. Ikiwa shule haitakuwa na sheria kama hizi, basi shule hizo zitakosa mwelekeo mwafaka na kutakuwa na athari hasi kwa masomo.

Matokeo ya utafiti pia yalionyesha kuwa, jukumu la utekelezaji wa kanuni za lugha za shule na wanafunzi, linatekelezwa na walimu wa somo la Kiingereza au Kiswahili tu. Walimu wengine hawaoni haja ya kujihusisha katika utekelezaji. Mzigo huu huwa mzito kwa walimu hawa. Kwa hivyo, kanuni hizi husalia tu kuwa kwenye maandishi. Itakuwa vyema zaidi ikiwa kila mwalimu atahusika katika kuhakikisha kuwa kanuni hizi zimetokelezwa na kila mwanafunzi. Wanafunzi watakapoona ushirikiano wa walimu wote, mielekeo yao itakuwa chanya.

Mtafiti pia aligundua kuwa, shule ambazo zinafadhili shughuli za idara na kuwapa motisha, walimu na wanafunzi, mielekeo yao kuhusu kanuni za lugha ya Kiswahili huwa chanya. Wao hujitolea kuhakikisha kuwa shughuli hizi zimefanikishwa. Kwa hivyo, itakuwa vyema ikiwa walimu wakuu watajitolea kutoa ufadhili na motisha kwa walimu na wanafunzi ili kubadilisha mielekeo ya walimu na wanafunzi. Wizara ya elimu pia ina jukumu la kufadhili shughuli kama makongamano ya nje ya shule ili kufaidi walimu wote hasa wale wanaotoka shule ambazo hazina uwezo wa kifedha wa kufadhili walimu wao. Sura inayofuata imefafanua athari ya kanuni za lugha shuleni kwa somo la Kiswahili.

## **SURA YA NNE**

### **ATHARI YA KANUNI ZA LUGHA SHULENI KWA SOMO LA**

#### **KISWAHILI**

#### **4.0. Utangulizi.**

Sura hii imeangazia namna kanuni za lugha za shule zinavyoathiri somo la Kiswahili katika shule za upili Kaunti ya Busia. Matokeo ya mtihani wa kitaifa kuanzia mwaka 2020 hadi 2023 yalitumika ili kubaini athari ya kanuni za lugha za shule kwa somo la Kiswahili. Aidha, mtafiti alifanya mahojiano ya ana kwa ana na walimu wakuu pamoja na wakuu wa idara ya Kiswahili wa shule saba za utafiti. Mihimili ya nadharia ya Kijumuia na kibinadamu ya Richards na Rodgers (1995) pia ilichangia kufanikisha lengo la utafiti huu. Sura hii imechanganua matokeo ya mtihani ya wanafunzi katika somo la Kiswahili na athari ya kanuni za lugha za shule tofauti katika somo la Kiswahili.

#### **4.1 Matokeo ya mtihani wa wanafunzi katika somo la Kiswahili**

Kwa mujibu wa ripoti ya KNEC ya mwaka 2019 baada ya matokeo ya mtihani wa somo la Kiswahili, ilipendekeza kwamba, walimu waendeleo kuwapa wanafunzi mazoezi katika vipengele vyote vya kisarufi. Matokeo ya baraza la KNEC yalionyesha kuwa, utendaji wa watahiniwa katika karatasi la fasihi andishi unaendelea kudorora kutokana na wanafunzi kutosoma vitabu viteule. Aidha matokeo yalibainisha kwamba asilimia kubwa ya watahiniwa hata wale wanaopata alama za juu zaidi, hawajui kuwasilisha hoja kwa njia komavu. Lugha yao ya mawasiliano ni mbovu. Ni kwa misingi hii ambapo matokeo ya mtihani yalitumika kubainisha ikiwa kanuni za lugha za shule zinazohusu matumizi ya lugha ya

Kiswahili katika shughuli mbalimbali za shule zinaathiri somo la Kiswahili. Matokeo ya mtihani kutoka idara ya Kiswahili kuanzia mwaka wa 2020 hadi 2023 yalichunguzwa na kuwasilishwa katika jedwali 4.1.1.

**Jedwali 4.1 Matokeo ya mtihani wa Kitaifa katika somo la Kiswahili kati ya mwaka 2020-2023**

| <b>Shule / Mwaka</b> | <b>2020</b> | <b>2021</b> | <b>2022</b> | <b>2023</b> |
|----------------------|-------------|-------------|-------------|-------------|
| <b>Butula</b>        | 8.904       | 9.101       | 9.327       | 10.45       |
| <b>Mundika</b>       | 5.395       | 5.725       | 8.32        | 7.37        |
| <b>Amukura</b>       | 5.98        | 5.29        | 5.58        | 7.01        |
| <b>Lwanya</b>        | 8.776       | 8.949       | 8.500       | 9.625       |
| <b>Chakol</b>        | 6.245       | 7.871       | 8.775       | 8.819       |
| <b>Kisoko</b>        | 6.8073      | 8.430       | 7.836       | 8.4223      |
| <b>Makunda</b>       | 4.750       | 3.5029      | 4.700       | 4.232       |

Katika jedwali 4.1, matokeo ya mtihani wa Kiswahili yanatofautiana kwa kiasi kikubwa katika shule teule. Shule ya upili ya Kitaifa ya Butula na Shule ya upili Wasichana ya Lwanya zimedumisha matokeo mazuri kila mwaka katika somo la Kiswahili. Matokeo mazuri pia yameshuhudiwa katika shule ya upili ya Chakol na Kisoko. Katika shule ya upili ya Mseto ya Makunda matokeo ya mtihani katika somo la Kiswahili ni ya kusikitisha ikilinganishwa na shule zingine zilizoteuliwa kwenye utafiti huu. Ingawa matokeo ya mtihani katika shule ya upili ya wavulana ya Amukura na Mundika yamekuwa ya wastani, matokeo ya mtihani wa somo la Kiswahili katika shule ya upili ya Mundika yaliimarika mwaka 2022 na 2023 nayo ya Amukura yakaimarika mwaka 2023. Mtafiti kupitia mahojiano kwa wakuu wa shule za upili na wakuu wa idara, alitaka kujua sababu ya matokeo haya na ikiwa kuna uhusiano wowote na kanuni za lugha za shule zilizopo. Swali alilouliza ni, *Eleza athari ya kanuni za lugha za shule katika somo la Kiswahili.* Majibu ya kauli hii yamejadiliwa katika sehemu zinazofuata.

## **4.2 Athari ya kanuni za lugha za shule katika somo la Kiswahili**

Watafiti mbalimbali kama Nyakeoga 2018, Wanjiku 2014, Nyongesa na wenzake 2022 wanaafikiana kuwa, shule nyingi nchini Kenya, zimeanzisha kanuni za lugha za shule ambazo madhumuni yake ni kukukuza mawasiliano katika lugha ya Kiswahili na Kiingereza kama njia ya kuimarisha matokeo katika masomo haya. Utafiti ulibaini kuwa, shule saba zilizoteuliwa kufanyiwa utafiti zina kanuni za lugha za shule ingawa utekelezaji wake ulitofautiana. Katika shule za utafiti, matokeo ya utafiti yalibaini kuwa, lugha ya mawasiliano ni Kiswahili na Kiingereza. Licha ya kuwepo kwa kanuni hii, baadhi ya wanafunzi huwasiliana kwa lugha ya kiasili au Sheng. Aidha, shule hizi zina siku ya Kiswahili. Kuna shule ambazo mikakati imewekwa kuhakikisha kuwa wanafunzi wanawasiliana katika lugha sanifu, ilhali katika shule zingine, sheria hii imebaki tu katika maandishi. Matokeo ya utafiti pia yalionyesha kuwa, ingawa kuna mijadala katika lugha ya Kiswahili, walimu katika baadhi ya shule hawatili maanani mijadala hii. Mijadala hii inaendeshwa tu na wanafunzi au walimu wa zamu. Utafiti pia uligundua kuwa, shughuli za idara ya Kiswahili hutekelezwa sana katika shule za upili zenye uwezo wa kifedha wa kufadhili shughuli hizi. Katika shule za Kaunti au zisizo na uwezo wa kifedha, shughuli za idara zimebaki tu kwenye kumbukumbu za mikutano. Hii imechangia athari yake kwa somo la Kiswahili kuwa tofauti. Mahojiano yaliyofanywa katika shule teule na walimu wakuu pamoja na wakuu wa idara, yalionyesha kuwa, kanuni za lugha za shule huteuliwa ili kuimarisha somo la Kiswahili na Kiingereza. Hivyo, wadau katika sekta ya elimu wakishirikiana katika utekelezaji wa kanuni za lugha za shule, matokeo ya mtihani yatakuwa mazuri. Nyongesa na wenzake (2022) wanasema kuwa, matokeo mabaya katika somo la Kiswahili katika mtihani wa Kitaifa kwa kiasi fulani husababishwa na uzembe katika utekelezaji wa kanuni za

lugha za shule. Utafiti wa Wangeci (2011) pia unaafikiana kuwa, kutotekeleza kwa kanuni za lugha za shule katika mfumo wa elimu huchangia wanafunzi kufanya vibaya katika somo la Kiswahili. Ili kubaini athari ya kanuni za lugha za shule, utafiti huu ulifafanua jinsi kanuni za lugha za shule zinavyoathiri somo la Kiswahili.

#### **4.2.1 Athari ya lugha ya mawasiliano katika mazingira ya shule kwa somo la Kiswahili**

Lugha ni kipengele muhimu kinachotumika kukuza mawasiliano, kupanua fikra na katika kubadilishana mawazo, jumbe, hisia na mielekeo miongoni mwa waja (Aziz, 2003). Kiswahili kama lugha rasmi na lugha ya Kitaifa nchini Kenya, imekuwa muhimu sana. Licha ya somo la Kiswahili kuwa la lazima katika shule za upili nchini, inasikitisha kuwa, hata baada ya mabadiliko haya katika sera ya lugha ya Kiswahili, kuna baadhi ya kanuni za lugha ambazo zinazuia wanafunzi kuwasiliana kwa lugha hii kila siku. Kwa hivyo kwa kiasi fulani kuchangia matokeo mabaya katika somo la Kiswahili. Katika shule za upili kaunti ya Busia, ilibainika kuwa, lugha ya Kiingereza imepewa siku nyingi katika mawasiliano ikilinganishwa na lugha ya Kiswahili. Lugha ya Kiswahili haitumiki katika hadhi sawa na lugha ya Kiingereza. Shule za upili za Mundika na shule ya upili ya Kisoko, zina kanuni ya lugha ya shule kwamba wanafunzi hawapaswi kuzungumza lugha ya Kiswahili katika mazingira ya shule isipokuwa darasani wakati wa somo la Kiswahili. Wanafunzi hawa wanafaa kuzungumza lugha ya Kiingereza pekee. Hali hii huwalazimisha wanafunzi kuwa na mazoea ya kuongea lugha ya Kiingereza na kuona lugha ya Kiswahili kuwa haina umuhimu wowote. Hii imechangia wanafunzi kutowasiliana kwa lugha ya Kiswahili. Wanafunzi wasipowasiliana kwa lugha ya Kiswahili, athari yake kwa somo la Kiswahili huwa hasi.

Katika shule za utafiti, lugha ya mawasiliano katika mazingira ya shule ni Kiswahili na Kiingereza. Katika shule za upili za Mundika na Kisoko, Kiswahili huzungumzwa darasani wakati wa somo la Kiswahili. Lugha za kiasili haziruhusiwi katika mazingira haya. Mahojiano ya mtafiti na walimu wakuu wa shule pamoja na wakuu wa idara ya Kiswahili yalibaini kuwa, baadhi ya wanafunzi katika shule za upili badala ya kuzungumza lugha sanifu, wao huzungumza lugha za kiasili au sheng'. Hali hii huathiri somo la Kiswahili wakati wanafunzi wanapotumia maneno ya sheng au ya lugha za kiasili katika uandishi wao wa mitihani hivyo kusababisha matokeo mabaya katika somo la Kiswahili. Hali hii imechangia wakuu wa shule za upili kupiga marufuku mawasiliano katika lugha ya Kiswahili. Shule ya Upili ya Mundika na Kisoko wamepiga marufuku mawasiliano kwa lugha ya Kiswahili, za kiasili na sheng'. Mwalimu mkuu katika shule ya upili ya Kisoko alikuwa na haya ya kusema :

‘Katika shule hii, wanafunzi hawaruhusiwi kuzungumza lugha ya Kiswahili kwa sababu, badala ya kuzungumza lugha sanifu, wao huzungumza sheng huku wakidhani kuwa wanazungumza Kiswahili sanifu. Walimu wengine wa somo la Kiswahili hawahakikishi kuwa wanafunzi hawa wanawasiliana kwa lugha sanifu. Walimu wenye umri kati ya 25-40 huwa mstari wa kwanza kuwasiliana na wanafunzi kwa sheng'. Ili kuzuia wanafunzi hawa kuathiriwa na sheng katika uandishi na mawasiliano yao, nilionelea kupiga marufuku mawasiliano kwa lugha ya Kiswahili na badala yake nikatenga Siku ya Kiswahili mara moja kwa muhula ambapo shughuli muhimu zinazohusiana na somo la Kiswahili huandaliwa.’

Kauli ya mwalimu mkuu pamoja na walimu wengine inaafikiana na matokeo ya utafiti wa Makokha (2022) anayesema kuwa, Sheng imeenea sana katika matumizi yake miongoni mwa wanafunzi wa shule za upili na hivyo imekuwa na athari hasi miongoni mwa wanafunzi hawa. Wanafunzi katika shule za upili hutumia sheng na walimu wao wameshindwa kuthibiti matumizi ya sheng' shuleni. Wanafunzi hawa, hufanya makosa ya kimofolojia ambayo husababisha kufeli katika mitihani yao ya somo la Kiswahili hasa karatasi le kwanza na la pili yanayoshughulikia matumizi ya sarufi na lugha. Anasema kuwa, sheng ni suala ambalo limepelekea wanafunzi wengi kufeli katika mitihani yao ya kitaifa hasa ikikumbukwa kwamba Kiswahili ni somo ambalo ni la lazima katika shule za upili na hutahiniwa mwishoni mwa mwaka wa nne katika mitihani wa kitaifa katika shule za upili. Matokeo ya utafiti wake pia yalionyesha kuwa, wanafunzi wengine huiga walimu wao ambao hutumia lugha ya sheng katika mazingira ya shule. Matokeo ya Makokha (keshatajwa) yanawiana na ya Wanjiku (2014), anayesema kuwa, nusu ya walimu wa somo la Kiswahili huwasiliana kwa lugha ya Kiswahili ilihali wengine huchanganya lugha ya Kiswahili na lugha nyingine wanapowasiliana na wanafunzi. Kwa hivyo, wanafunzi huiga lugha ya walimu na baadaye huathiri uandishi wao wa Kiswahili. Athari ni kuwa, wanafunzi hawa huenda wakatumia lugha zingine na sheng katika uandishi wao. Hii huathiri somo la Kiswahili. Mkuu wa idara ya Kiswahili katika shule ya upili ya Mundika, alichangia kwa kusema kuwa ;

‘Kujumuishwa kwa somo la isimu jamii kwa silabasi ya Kiswahili ya somo la Kiswahili kumechangia uhuru wa wanafunzi kutumia lugha ya sheng katika mawasiliano yao huku wakidai kuwa ni sajili ya vijana. Hii inabainika katika mifano ya sajili ya vijana katika somo la Kiswahili la isimu jamii. Wanafunzi wengine hukopa misamiati kutoka sajili hii na kuihamisha misamiati hii katika uandishi wao wa insha wakidhani ni misamiati ya Kiswahili sanifu.’

Katika shule ya Upili ya Makunda, mkuu wa idara ya Kiswahili, alisema kuwa, ingawa wana siku ya kuwasiliana kwa lugha ya Kiswahili, imekuwa changamoto kutekeleza kanuni hii. Alisema kuwa, baadhi ya wanafunzi katika shule hii badala ya kuzungumza Kiswahili sanifu, wao huzungumza lugha za kiasili au sheng'. Hii huchangia matokeo mabaya katika mtihani wa somo la Kiswahili namna inavyobainika katika Jedwali 4.1, Mwalimu huyu alisema kuwa, kabla ya kuhamishwa hadi shule hii, alikuwa anafunza katika shule ya Kitaifa ambayo ni ya bweni na wanafunzi walifanya vizuri sana katika somo la Kiswahili. Katika shule za bweni, ni rahisi kuhakikisha kuwa wanafunzi wanawasiliana kwa lugha ya Kiswahili sanifu ikilinganishwa na wanafunzi wa shule ya kutwa wanaporudi nyumbani. Matokeo haya yanafikiana na ya Ogero (2012) ambaye alisema kuwa, katika shule za umma za kutwa, wanafunzi walipendelea kuwasiliana kwa lugha za kiasili au sheng'. Hii iliwafanya wanafunzi kutoka shule za kutwa kaunti ya Kisii kufanya vibaya katika mtihani wa somo la Kiswahili mwaka 2013. Aidha, utafiti wa Mutua (2015) ulibaini kuwa, katika shule za upili, kila shule ina kanuni za lugha za shule ingawa utekelezaji wake unatofautiana. Shule nyingi zinakubali matumizi ya lugha ya Kiswahili na Kiingereza lakini katika shule za kutwa, hali ni tofauti. Wanafunzi katika shule za kutwa huwasiliana kwa lugha za kiasili hivyo kusababisha matokeo mabaya kwa somo la Kiswahili. Utekelezaji wa kanuni hii imekuwa changamoto hasa katika shule za kutwa kwa sababu wanafunzi hawa hutumia muda mwingi nyumbani na lugha wanayoitumia kuwasiliana na wanakijiji ni ya kiasili.

Kulingana na Hymes (1966), mtu hujifunza lugha zaidi kwa kuitumia lugha hiyo. Aidha, katika nadharia ya Kijumuia na Kibinadamu ya Richards na Rodgers (1995), wanasema kuwa, wanafunzi wanaweza kujifunza lugha kwa njia mbalimbali ikiwemo mazungumzo ya jumla, kwa hivyo ili mwanafunzi aweze kuijua lugha, anafaa kupewa fursa ya kuwasiliana kwa lugha hiyo. Katika shule ya Upili ya Kitaifa ya Butula na Shule ya wasichana ya Lwanya, wakuu wa idara walikubaliana kuwa, wanafunzi wanapopewa fursa ya kuwasiliana kwa lugha ya Kiswahili sanifu, matokeo ya mtihani yatakuwa mazuri. Ili kuhakikisha kuwa wanafunzi wanawasiliana katika lugha ya Kiswahili, mkuu wa idara ya Kiswahili katika shule ya Upili ya Butula alisema kuwa, si rahisi walimu kuhakikisha kuwa wanafunzi wanawasiliana kwa lugha sanifu kutokana na idadi kubwa ya wanafunzi. Kwa hivyo, wanafunzi wa chama cha Kiswahili (CHAKIBU) wamepewa jukumu la kuhakikisha kuwa, wanafunzi wanawasiliana kwa lugha sanifu. Hii imewasadia sana kuimarisha matokeo ya mtihani katika somo la Kiswahili. Hali hii inawiana na utafiti wa Mutua (2015) anayesema kuwa, viranja na walimu wanafaa kuhakikisha kuwa utekelezaji wa kanuni za lugha za shule unazaa matunda. Mtafiti alipotafiti katika shule za kutwa, kaunti ndogo ya Moyale, alibaini kuwa matumizi ya lugha za kiasili katika mazingira ya shule ilikuwa kawaida licha ya siku mbili kutengwa za kuwasiliana kwa lugha ya Kiswahili. Anakubaliana na watafiti wengine kama Ogero (2012), ambaye matokeo yake yalibaini kuwa, sehemu fulani ya wanafunzi hasa katika shule za kutwa, walipendelea kuwasiliana katika lugha ya Sheng na za kiasili. Hii ilichangia matokeo mabaya katika somo la Kiswahili.

Uchunguzi wa utafiti huu pia ulibainisha kuwa, wanafunzi wanapowasiliana kwa lugha sanifu ya Kiswahili, huwawezesha wanafunzi hawa kuwa na umilisi wa juu wa lugha. Lugha hii sanifu hutumiwa katika uandishi wao wa mitihani kutokana na uzoefu. Matokeo haya yanawiana na ya Koko (2016) anayesema kuwa, sababu ya uimarikaji wa matokeo ya mtihani wa kitaifa katika shule za upili sehemu ya Nyanza ni kanuni za lugha za shule zinazowaruhusu wanafunzi kuwasiliana kwa lugha ya Kiswahili. Hii humwezesha mwanafunzi kufanya vyema katika somo la Kiswahili. Mwalimu mkuu katika shule ya Upili ya Amukura alisema kuwa;

‘Wanafunzi wamekuwa wakifanya vibaya katika mtihani wa somo la Kiswahili katika shule hii hata baada ya kuruhusiwa kuwasiliana kwa lugha ya Kiswahili. Nilipogundua kuwa wao huwasiliana kwa lugha ya Sheng na mara nyingine kwa lugha za kiasili, niliwapa viranja jukumu la kuwa mstari wa mbele kuhakikisha kuwa wanafunzi hawazungumzi lugha ya sheng au za kiasili ila Kiswahili sanifu. Kwa sababu hii, tunaweza kusema kuwa matokeo mema ya mwaka 2023 kwa kiasi fulani yalitokana na wanafunzi hawa kuwasiliana kwa lugha sanifu.’

Matokeo ya utafiti kuhusu athari ya lugha ya mawasiliano katika mazingira ya shule yalionyesha kuwa, matumizi ya lugha ya Kiswahili sanifu yana athari chanya katika somo la Kiswahili. Wanafunzi wanapowasiliana kwa lugha sanifu, ujuzi wao katika lugha ya Kiswahili huimarika. Aidha, matokeo ya utafiti yaliafikiana na ya watafiti wengine kuwa wanafunzi wanapowasiliana katika lugha za kiasili au sheng huathiri kile wanachoandika darasani na katika mitihani yao. Matokeo ya utafiti huu pia yalikubaliana na ya Rutto (2014) aliyebaini kuwa, kadri mwanafunzi anavyotangamana na lugha kupitia mazoezi ya kuizungumza, ndivyo anavyofanya vyema katika mtihani wake. Isitoshe, walimu kama kielelezo bora kwa wanafunzi,

wanafaa kuwasiliana kwa lugha sanifu wakiwa shuleni kwa sababu wanafunzi huiga wanachofanya walimu wao.

#### **4.2.2 Athari ya siku za Kiswahili katika somo la Kiswahili**

Siku za Kiswahili ni siku ambazo mawasiliano huwa katika lugha ya Kiswahili shuleni. Matokeo ya utafiti yalionyesha kuwa, katika shule za upili, Kaunti ya Busia, kuna siku za Kiswahili, ingawa idadi ya siku hutofautiana kutoka shule moja hadi nyingine. Kwa mfano, katika shule ya upili ya Butula, Lwanya, Chakol na Makunda, lugha ya Kiswahili huzungumzwa mara tatu kwa wiki, kwanzia Ijumaa hadi Jumapili. Hata hivyo katika shule za upili za Kisoko na Mundika, matumizi ya lugha ya Kiswahili hairuhusiwi, lakini kuna siku imetengewa shughuli za idara ya Kiswahili. Siku hii huitwa '*Siku ya Kiswahili*'. Katika shule ya upili ya Amukura, wanafunzi wana uhuru wa kuwasiliana kwa lugha ya Kiswahili au Kiingereza siku zote za wiki.

##### **4.2.2.1 Matumizi ya lugha ya Kiswahili mara tatu kwa wiki**

Kulingana na utafiti, lugha ya Kiswahili hutumika mara tatu kwa wiki katika shule ya upili ya Butula, Lwanya, Chakol na Makunda. Lugha ya Kiswahili huzungumzwa kuanzia siku ya Ijumaa hadi Jumapili. Kupitia mahojiano na walimu wakuu pamoja na wakuu wa idara ya Kiswahili, ilibainika kuwa, siku hizi hutengewa lugha ya Kiswahili ili kuimarisha ujuzi wa wanafunzi katika lugha hii. Wanafunzi wanapokuwa na ujuzi katika lugha ya Kiswahili, bila shaka, matokeo ya mitihani katika somo la Kiswahili huwa mazuri. Matokeo ya utafiti haya yanafanana na matokeo ya utafiti wa Nyongesa (2011), ambayo yalionyesha kuwa, katika shule za upili ambazo Kiswahili kilizungumzwa siku tatu kwa wiki, matokeo ya mtihani

yalikuwa mazuri ikilinganishwa na shule za mseto ambazo ziliwaruhusu wanafunzi kuwasiliana mara moja katika lugha ya Kiswahili. Licha ya wanafunzi katika shule ya Mseto kuruhusiwa kuwasiliana mara moja katika lugha ya Kiswahili, utafiti wake pia ulionyesha kuwa, wanafunzi wa jinsia ya kike walifanya vizuri katika somo la Kiswahili hata baada ya kuzuiliwa kuwasiliana kwa lugha ya Kiswahili ikilinganishwa na wavulana. Pasipokutilia maanani matokeo haya ya utafiti, Je, Lugha ya Kiswahili hutumiwa sawasawa katika mazingira ya shule ? Je, idadi ya siku ambayo lugha ya Kiswahili imepewa kuzungumzwa shuleni huathiri somo la Kiswahili ? Kupitia mahojiano na walimu wakuu, wakuu wa idara ya Kiswahili na matokeo ya mtihani katika shule saba za utafiti, mwandishi alibaini yafuatayo ;

Kwanza, matumizi ya lugha ya Kiswahili siku fulani kwa wiki au muhula huimarisha ujuzi wa wanafunzi katika uandishi na mawasiliano katika lugha hii. Shule zinapotenga siku fulani kwa sababu ya mawasiliano kwa lugha ya Kiswahili, huwapa wanafunzi motisha wa kuelewa lugha hii, hivyo kuweza kujibu maswali katika somo la Kiswahili. Hii huimarisha matokeo katika mitihani ya somo la Kiswahili.

Pili, utafiti ulibaini kuwa, kuwepo tu kwa siku za Kiswahili shuleni si muhimu, utekelezaji wa kanuni hii ndio muhimu sana. Shule ambazo zinawaruhusu wanafunzi kuwasiliana kwa lugha ya Kiswahili na kuweka mikakati ya kuhakikisha kuwa wanafunzi hawa wanazungumza Kiswahili sanifu, matokeo ya mitihani katika somo la Kiswahili ni mazuri na umilisi wao katika lugha hii pia ni wa juu. Katika shule ya upili ya Lwanya, ni jukumu la kila mshikadau katika shule hii kuhakikisha kuwa kanuni hii inazingatiwa. Mwalimu mkuu alikuwa na haya ya kusema,

Siku ya Kiswahili katika shule hii, ni siku muhimu sana. Wanafunzi, walimu na hata wafanyakazi wa shule huhimizwa kuwasiliana kwa lugha ya Kiswahili. Hii imewafanya wanafunzi kuwa na mielekeo chanya na kufanya vizuri zaidi katika somo la Kiswahili. Matokeo ya mtihani ni ishara kuwa, wanafunzi wanapopewa fursa ya kuwasiliana kwa lugha hii, ujuzi wao katika uandishi pia huimarika.

Vilevile, mtafiti pia alibaini kuwa, katika shule ya Upili ya Butula na Lwanya, walimu wanaozungumza kwenye gwaride siku ya Ijumaa ambayo ndiyo siku ya Kiswahili, huzungumza kwa lugha ya Kiswahili. Hii huchangia mielekeo chanya kwa wanafunzi. Wanafunzi huiga kile ambacho walimu wao wanafanya hivyo kuchangia mielekeo chanya. Isitoshe, wanafunzi nao hawajaachwa nyuma, matangazo na habari siku hii yanayowasilishwa kwenye gwaride huwasilishwa kwa lugha sanifu ya Kiswahili. Wanafunzi wengine hujifunza misamiati na matumizi ya lugha sanifu kutoka kwa wanafunzi hawa. Hii hufanya wanafunzi kuiga misamiati hii katika uandishi wao wa mitihani ya somo la Kiswahili. Wanapofanya hivyo, athari kwa somo la Kiswahili huwa chanya.

Ingawa, katika shule ya upili ya Makunda, matumizi ya lugha ya Kiswahili ni mara tatu kwa wiki, imekuwa changamoto kwa mkuu wa Idara ya Kiswahili pamoja na walimu wa somo la Kiswahili kuhakikisha kuwa wanafunzi hawa wanazungumza kwa lugha ya Kiswahili siku hizo tatu. Hii ni kwa sababu, kuanzia Jumamosi hadi Jumapili wanafunzi hawa huwa nyumbani kwa kuwa ni shule ya kutwa. Lugha ambayo wanafunzi hawa hutumia ni sheng au za kiasili. Mkuu wa idara ya Kiswahili alisema kuwa, wanafunzi wanapowasiliana kwa lugha za kiasili au sheng', huathiri matokeo ya somo la Kiswahili kwa njia hasi. Athari ya lugha ya kwanza ya wanafunzi hawa hubainika wanapojibu maswali katika mitihani ya somo la

Kiswahili hasa karatasi la insha na sarufi. Onyango (1997) katika utafiti wake eneo hili la Bunyala ambapo shule ya upili ya Makunda inapatikana alisema kuwa, makosa mengi ya wanafunzi hutokana na kuathiriwa kwa lugha ya kwanza, hata hivyo kuna makosa mengine ambayo hayahusiani na athari za lugha ya kwanza.

#### **4.2.2.2 Matumizi ya lugha ya Kiswahili mara moja kwa muhula**

Katika shule za upili za Kisoko na Mundika mawasiliano katika lugha ya Kiswahili yamepigwa marufuku ila kuna siku ya Kiswahili kila muhula. Siku hii hufidia upungufu wa wanafunzi kutowasiliana kwa lugha ya Kiswahili siku zote wanapokuwa katika mazingira ya shule. Ilibainika kuwa, wanafunzi wana mielekeo chanya kuhusu siku hii. Shughuli mbalimbali za idara ya somo la Kiswahili huandaliwa siku hii. Walimu wa somo la Kiswahili huhudhuria siku hii ili kuwaelekeza wanafunzi kuhusu maswala mbalimbali yanayohusu somo la Kiswahili. Walimu hawa huandaa shughuli mbalimbali zinazohusu uandishi na matumizi ya lugha sanifu. Mwanafunzi anayepatikana akizungumza sheng' au lugha za kiasili huadhibiwa. Mwalimu mkuu wa shule ya Mundika alikuwa na haya ya kusema kuhusu siku hii ;

‘Baada ya kupiga marufuku matumizi ya lugha ya Kiswahili katika mazingira ya shule, matokeo ya mtihani wa somo la Kiswahili yaliendelea kuwa mabaya mwaka wa 2020 na 2021. Walimu wa somo la Kiswahili walisema ni kwa sababu ya sheria hii. Badala ya kutenga siku ya Kiswahili kwa wiki walivyotaka walimu hawa, nilitenga siku ya Kiswahili kila muhula. Nilikuwa na uhakika kuwa, walimu wa somo la Kiswahili watahudhuria siku hii na athari yake itakuwa chanya kwa somo la Kiswahili ikilinganishwa na kuwaruhusu wanafunzi kuzungumza lugha ya Kiswahili siku fulani kwa wiki. Shughuli zinazoandaliwa siku hii zimewafaa sana wanafunzi katika

somo la Kiswahili. Tumeshuhudia kuimarika kwa somo la Kiswahili tangu mwaka 2022.’

Siku ya Kiswahili katika shule za upili za Kisoko na Mundika zimezaa matunda na kufidia upungufu wa kutowasiliana kwa lugha ya Kiswahili. Athari ya siku hii imekuwa chanya kwa somo la Kiswahili. Wanafunzi hupata fursa ya kuonyesha ujuzi wao kuhusu lugha hii. Aidha, walimu wa somo la Kiswahili huwaelekeza katika mambo ya kuzingatia wanapojitayarisha kufanya mtihani wa somo la Kiswahili. Mkuu wa idara katika shule ya upili ya Kisoka alisema kuwa, wao hualika wageni ambao ni watahini wa somo la Kiswahili kuzungumza na wanafunzi wao. Kwa kiasi fulani, siku hii imechangia matokeo bora katika mitihani ya Kitaifa kwa somo la Kiswahili.

#### **4.2.2.3 Matumizi ya lugha ya Kiswahili kila siku shuleni**

Katika shule ya upili ya Amukura, matumizi ya lugha ya Kiswahili ni kila siku, kuanzia Jumapili hadi Jumamosi. Matokeo ya mtihani katika shule ya upili ya Amukura kuanzia mwaka wa 2020 hadi 2022 yalikuwa ya kusikitisha licha ya kuwa na uhuru wa kuzungumza lugha ya Kiswahili siku zote za wiki. Utafiti ulibaini kuwa, ingawa wanafunzi wana uhuru wa kuzungumza lugha wanayoipenda, wanafunzi hawa huzungumza sheng au za kiasili hasa wanapokuwa pekee yao. Hali hii kwa kiasi fulani ilichangia matokeo mabaya katika mtihani wa somo la Kiswahili. Licha ya matokeo haya mabaya, mwalimu mkuu alisema kuwa, baada ya kuanza kuweka mikakati ya kuhakikisha kuwa wanafunzi hawa wanawasiliana kwa lugha sanifu, kumekuwa na mabadiliko katika mtihani mwaka 2023. Matokeo haya ya utafiti yamedhihirisha kuwa, kuwasiliana kwa lugha ya Kiswahili na wanafunzi itakuwa tu na athari chanya kwa somo la Kiswahili ikiwa walimu wa somo la Kiswahili wataweka mikakati ya kuhakikisha kuwa wanafunzi hawa wanawasiliana kwa lugha sanifu.

#### **4.2.2.4 Athari ya maoni ya walimu kuhusu Siku ya Kiswahili**

Kufaulu kwa kanuni ya lugha ya shule itategemea ushirikiano wa wadau wote katika mazingira ya shule. Utafiti ulibaini kuwa, kuna baadhi ya maoni kutoka kwa walimu wa masomo mengine ambayo imekuwa kikwazo katika utekelezaji wa mawasiliano katika somo la Kiswahili. Kwa mujibu wa Shiundu na wenzake (1992), alisema kuwa wanafunzi hutaka walimu ambao watawapa motisha ya kuwasiliana kwa lugha husika wakiwa darasani au nje ya darasa. Kwa hivyo maoni ya walimu huathiri mielekeo ya wanafunzi. Kwa mfano, mkuu wa idara katika shule ya upili ya Chakol alisema kuwa, utekelezaji wa kanuni ya lugha ya shule kuhusu mawasiliano katika lugha ya Kiswahili imekuwa changamoto hasa kutokana na maoni ya walimu wa masomo mengine. Maoni ya walimu hawa kuhusu kanuni ya lugha ya shule inayohusu siku ya Kiswahili ni ya kutamausha. Wanafunzi wanaposikia maoni hasi yanayotolewa na walimu hawa huchangia mielekeo hasi kwa wanafunzi inayowafanya wanafunzi hawa kuchukua somo la Kiswahili. Katika shule ya upili ya Chakol, mkuu wa idara alikuwa na haya ya kusema kuhusu kauli moja iliyotolewa na mwalimu wa somo la hesabu ;

‘Somo la Kiswahili si somo muhimu na ni rahisi sana kuelewa hata mwanafunzi asipowasiliana kwa lugha hii. Nilipokuwa mwanafunzi katika shule ya upili, hatukuruhusiwa kuwasiliana kwa lugha ya Kiswahili, lakini nilipita somo hili. Wanafunzi wengine ni werevu sana na wanaweza tu kupita mtihani wa somo la Kiswahili hata bila kuzungumza lugha hii. Somo kama la hesabu, halihitaji mwanafunzi kuwasiliana kwa lugha ya Kiswahili’.

Ingawa kauli hii ni ya kutamausha, mkuu wa idara kwa kiasi fulani alikubaliana na kauli ya mwalimu wa hesabu. Ameshuhudia wanafunzi werevu wakipita somo la Kiswahili hata baada ya kuwa na mieleko hasi kuhusu lugha ya Kiswahili. Matokeo

haya ya utafiti yawawiana na ya Babusa (2010) aliyebaini kuwa wanafunzi wenye mielekeo hasi kuhusu lugha ya Kiswahili walikuwa na viwango vya juu vya umilisi wa lugha ya Kiswahili. Licha ya mielekeo yao hasi ya lugha ya Kiswahili, walifanya vizuri katika mitihani yao.

Utafiti pia ulibaini kuwa, walimu wengine hawatilii maanani utekelezaji wa kanuni za lugha za shule kutokana na idadi ya siku ambayo lugha ya Kiswahili imepewa nafasi ya kuwasiliana katika shule nyingi nchini Kenya. Walimu hawa walisema kuwa, kuna kutowiana kati ya sera ya lugha ya nchi na kanuni za lugha za shule. Hali hii tatanishi pia imechangia tatizo katika ushirikiano wa walimu wengine katika utekelezaji wa kanuni ya lugha ya shule kuhusu siku ya Kiswahili. Mwalimu mmoja katika shule ya upili ya Kisoko ambaye pia ni mwalimu wa somo la Kiswahili ingawa anafundisha somo la Jiografia alikuwa na haya ya kusema ;

‘Tukitazama sera ya lugha ya nchi, lugha ya Kiswahili ni lugha rasmi na ya kitaifa. Lugha hii inafaa kutekeleza wajibu sawa na lugha ya Kiingereza katika shughuli rasmi za shule. Lakini hali si hivyo, lugha ya Kiingereza imekuzwa kihadhi na ndio lugha ambayo imeenziwa sana. Kwa mfano, wakati wa mikutano ya shule, kumbukumbu za mikutano huandikwa kwa lugha ya Kiingereza hata ikiwa shughuli ya kuandika kumbukumbu hizi imepewa mwalimu wa somo la Kiswahili. Hii inafanya utekelezaji wa kanuni hii na walimu wengine kuwa ngumu.’

Hali ya walimu wa somo la Kiswahili kuandika kumbukumbu za mikutano kwa lugha ya Kiingereza aidha ilibainika katika kumbukumbu za mikutano ya wanafunzi wanapokutana katika vyama vya Kiswahili. Kwa mfano, katika shule ya Upili ya Makunda, mtafiti alibaini kuwa, baadhi ya kumbukumbu za mikutano za chama cha

Uanahabari zimeandikwa kwa lugha ya Kiingereza. Matokeo haya yanawiana na ya Melly na Mohochi (2023), waliosema kuwa, sera ya lugha ya shule katika shule ya upili ya wasichana ya Itigo ilipendelea matumizi ya Kiingereza kama lugha ya mawasiliano. Kwa hivyo baadhi ya wanafunzi hutumia lugha ya Kiingereza kuandika kumbukumbu za mikutano ya lugha ya Kiswahili. Hali hii imekiathiri Kiswahili. Watu huiona kama lugha isiyokuwa na muhimu.

Vilevile, Omulando (2002) anaunga kauli ya mwalimu anaposema kuwa Kiingereza kina hadhi. Mtafiti huyu anasema kuwa, kuna muachano kati ya sera ya lugha ya Kitaifa na matumizi yake shuleni kupitia kanuni za lugha za shule. Kulingana na Omulando(keshatajwa), lugha ya Kiswahili ni muhimu na hufundishwa kama somo la lazima katika shule zote nchini Kenya. Vilevile ni somo la msingi wakati wanafunzi wanapochagua kazi za usoni kama Uanasheria, Uanahabari na Ualimu baada ya masomo yao katika shule za upili. Kwa hivyo, kanuni za lugha shuleni zinafaa kuinua hadhi ya lugha ya Kiswahili badala ya kupendelea Kiingereza.

Matokeo ya utafiti pia yalidhihirisha kuwa, katika baadhi ya shule, walimu huwaadhibu wanafunzi ambao huwasiliana kwa lugha ya Kiswahili siku iliyotengewa mawasiliano kwa lugha ya Kiingereza au wanafunzi wanaozungumza sheng' au za kiasili siku iliyotengewa mawasiliano kwa lugha ya Kiswahili. Hii imeathiri somo la Kiswahili pia.

#### **4.2.2.5 Athari ya adhabu katika somo la Kiswahili**

Adhabu ni mateso anayopewa mtu aliyevunja kanuni au sheria. Matokeo ya utafiti yalibaini kuwa, baadhi ya shule huwaadhibu wanafunzi wanaowasiliana kwa lugha ya Kiswahili siku iliyotengewa mawasiliano kwa lugha ya Kiingereza. Hii

imechangia mielekeo hasi dhidi ya lugha ya Kiswahili. Wanafunzi huogopa kuwasiliana kwa lugha ya Kiswahili wasije wakaadhibiwa. Matokeo haya yanafanana na uchunguzi wa Mukele (2008), aliyesema kuwa, baadhi ya shule zimeweka sheria zinazomzuia mwanafunzi kuwasiliana kwa lugha ya Kiswahili au mama. Mwanafunzi anayepatikana akitumia lugha ya Kiswahili au ya mama huadhibiwa vikali na hivyo anaweza kuamua kukichukia Kiswahili kwa kufikiria kuwa ni lugha ambayo haina manufaa yoyote nchini na kwa maisha yake ya hapo baadaye.

Fauka ya hayo, matokeo ya utafiti pia yalionyesha kuwa, kando na adhabu kuwa na athari hasi kwa somo la Kiswahili, kuna adhabu ambazo huwa na athari chanya. Katika shule ya upili ya Chakol, mwanafunzi anayezungumza sheng' au lugha za kiasili siku ya Kiswahili, huhitajika kuandika insha kumi au kusoma riwaya na kujibu maswali kutoka kwenye riwaya hiyo. Hii huchangia athari chanya kwa somo la Kiswahili. Matokeo haya yanaafikiana na matokeo ya watafiti kama Wanjiku (2014) ambaye alibaini kuwa, adhabu huwa na athari chanya au hasi kwa mwanafunzi. Ikiwa mwanafunzi ataadhibiwa kwa kuwa amewasiliana kwa lugha ya Kiswahili, wanafunzi hawa hawataitumia tena katika mawasiliano yao kwa kuwa wataogopa kuadhibiwa.

Matokeo ya utafiti pia yalibaini kuwa, kuna baadhi ya adhabu ambazo huwafadhaisha wanafunzi. Kwa mfano katika shule ya upili ya Lwanya, wanafunzi huvalia gunia ilioandikwa maandishi, 'I am a Language breaker'. Hii huzua wasiwasi miongoni mwa wanafunzi. Wanafunzi wanapokuwa na wasiwasi wanapozungumza lugha ya Kiswahili kwa kuogopa kuwa wataadhibiwa, huathiri ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili. Katika mhimili wa kwanza wa nadharia ya

Kijumuia na Kibinadamu ya Richards na Rodgers (1995) anasema kuwa, usalama wa mwanafunzi ulio na utu na ubinadamu ni muhimu sana. Wanafunzi wakiwa na wasiwasi na kutojisikia salama hawawezi kujifunza lugha vizuri. Kwa hivyo, walimu wanapotaka wanafunzi wajifunze lugha ya Kiswahili, wanafaa kuondoa adhabu za aibu na badala yake kubuni njia mbadala ya kushughulikia wanafunzi wanaokiuka kanuni hizi. Katika utafiti wa Nyariki (2023), alitambua kuwa, adhabu kali zinazokiuka haki za watoto hujitokeza katika mazingira ya shule. Adhabu kama hizi zinapaswa kuepukwa na badala yake njia mbadala za kushughulikia utovu wa nidhamu kutumiwa.

Tangazo la waziri wa Elimu Bwana Machogu kuhusu mfumo mpya wa kujumuisha gredi utakaotumiwa na baraza la mtihani la KNEC kwenye matokeo ya mitihani ya kitaifa pia umetambua somo la Kiswahili kuwa katika kiwango sawa na somo la Kiingereza (Muchunguh, 2023). Kwa sababu hii, mojawapo ya gredi za somo la Kiswahili au Kiingereza itatumika katika mfumo mpya wa kujumuisha gredi. Kwa hivyo, Mwanafunzi atakapohitajika kujiunga na chuo kikuu, atatumia gredi ya Kiingereza au Kiswahili. Hii imeendelea kuinua hadhi ya somo la Kiswahili katika shule za upili. Isitoshe, wadau katika sekta ya elimu wanapoteua siku za Kiswahili, wanafaa kujua kuwa lugha ya Kiswahili ina hadhi sawa na lugha ya Kiingereza. Licha ya haya, matokeo ya utafiti pia yalibaini kuwa, shule ambazo wanafunzi wanapewa fursa kuwasiliana kwa lugha ya Kiswahili hasa kwa kuelekezwa na walimu wao, matokeo ya mtihani ni mazuri na athari yake kwa somo la Kiswahili ni chanya.

Tunapohitimisha kipengele cha athari ya siku ya Kiswahili kwa somo la Kiswahili, mahojiano ya ana kwa ana kati ya mtafiti na wakuu wa shule pamoja na wakuu wa

idara ya Kiswahili, matokeo ya mitihani katika jedwali 4.1.1., ilibainika kuwa, kutenga siku za Kiswahili katika mazingira ya shule na kutekeleza kanuni hii ya lugha ina athari chanya kwa somo la Kiswahili. Siku hii huwapa wanafunzi fursa ya kunoa ujuzi wao wa uandishi na mawasiliano katika lugha hii hata ikiwa walimu wengine hasa wa masomo mengine wanapoona ugumu wa kutekeleza kanuni hii. Wanafunzi wanapopewa fursa ya kuwasiliana kwa lugha hii, lugha yao huwa sanifu na fasaha hivyo kuchangia uelewa wa maswali na kuyajibu ipasavyo. Hii huchangia matokeo mazuri katika mitihani na kufanya wanafunzi hawa kuwa na mielekeo chanya kwa somo la Kiswahili.

#### **4.2.3 Athari ya mabango na maandishi katika mazingira ya shule kwa somo la Kiswahili**

Kulingana na Koko (2016), mabango na maandishi tofauti katika mazingira ya shule hutumiwa kuwakumbusha wanafunzi na wapita njia kuhusu kanuni za lugha za shule na lugha inayokubaliwa katika mazingira haya au kuzungumza lugha sanifu wanapofika katika mazingira ya shule. Utafiti huu pia ulibaini kuwa, katika shule saba teule za utafiti, kuna mabango na maandishi tofauti. Kuna yale yanayohusu masomo mengine kama hesabu, kuna yale ya kuwapa nasaha kuhusu maisha kwa jumla wakiwa shuleni na pia kuna yale yanayohusu matumizi ya lugha sanifu. Katika shule za Upili za Lwanya, Mundika na Chakol, kuna mabango yanayohimiza matumizi ya lugha ya Kiingereza. Mabango ya aina hii yana athari hasi kwa somo la Kiswahili. Hayawapatii wanafunzi motisha wa kuwasiliana katika lugha ya Kiswahili. Aidha, katika shule ya upili ya Chakol, kuna bango linalohimiza wanafunzi na wapita njia katika mazingira haya kuepuka matumizi ya Sheng'.

Bango hili lina athari chanya kwa somo la Kiswahili. kwa hivyo, limewasaidia wanafunzi kutilia maanani maonyo na nasaha hizo.

Utafiti huu pia ulibaini kuwa, maandishi katika lugha ya Kiswahili au Kiingereza, huwekwa kwa ubao wa matangazo katika shule zote saba za utafiti. Lakini, mtafiti alipotazama ubao wa matangazo ulio katika mazingira ya shule hizi, taarifa nyingi ni katika lugha ya Kiingereza. Hali hii imechangia wanafunzi kuwa na mielekeo hasi kuhusu lugha ya Kiswahili. Mielekeo hasi nayo imechangia wanafunzi kutoona umuhimu wa somo la Kiswahili hivyo kuchangia matokeo mabaya. Kinya (2020) katika utafiti wake alipendekeza kuwa, kuna haja ya shule kuwa na maandishi ya matukio fulani kwa lugha ya Kiswahili na sio tu kwa lugha ya Kiingereza namna ilivyojitokeza katika utafiti wake. Hii itawafanya wanafunzi kuwa na motisha na polepole watabadilisha mtazamo wao kuhusu lugha ya Kiswahili na kufanya vizuri katika mitihani.

Katika shule ya upili ya Mundika na Chakol, ubao wa matangazo hutumiwa kuweka vielelezo vya insha bora ambazo zimeandikwa na wanafunzi. Insha hizi husomwa na wanafunzi wengine na kwa njia hii, wanafunzi hujifunza misamiati inayopatikana katika insha hizi. Fauka ya haya, wanafunzi hujifunza lugha na kufanya bidii zaidi ili insha zao ziwekwe katika ubao wa matangazo. Hali hii huchangia kuimarika kwa somo la Kiswahili hasa wanafunzi wanapotumia misamiati hii katika mitihani yao. Aidha wanafunzi hujikakamua kuandika insha bora ili pia insha zao ziwekwe kwenye ubao wa matangazo.

#### **4.2.4 Athari ya matumizi ya lugha ya Kiswahili katika mijadala kwa somo la Kiswahili**

Mijadala ni aina ya mazungumzo ambayo hufanywa kitaalamu juu ya mada fulani ambayo hujengwa kwa kutumia hoja. Katika nadharia ya Kijumuia na Kibinadamu ya Richards na Rodgers (1995), wanasema kuwa, kutomakinika kwa wanafunzi kupunguzwe hasa kwa kuwapa majukumu tofauti tofauti katika ufundishaji wa lugha ya pili. Kupitia mahojiano ya ana kwa ana kati ya mtafiti na wakuu wa idara ya Kiswahili alipowauliza, *Eleza umuhimu wa mijadala kwa lugha ya Kiswahili*. Mtafiti alibaini kuwa, mijadala huwapa wanafunzi ujasiri wa kujieleza mbele ya wanafunzi wenzao. Kwa njia hii, huimarisha ujuzi wao kwa lugha ya Kiswahili. Namna wanafunzi wanaendelea kujadili hoja mbalimbali mbele ya wanafunzi wenzao, ndivyo wanavyopata ujuzi wa kuwasilisha hoja hizo kwenye mitihani yao. Hii inachangia wanafunzi hawa kufanya vyema katika somo la Kiswahili. Katika shule ya upili ya Chakol, mkuu wa idara ya Kiswahili alikuwa na haya ya kusema kuhusu athari ya mijadala kwa somo la Kiswahili;

‘Mimi ni mtahini wa karatasi la kwanza. Swali la pili la insha huhusu kujadili maswala ibuka. Ni kutokana na sababu hii, mimi mwenyewe huchukua jukumu la kuhakikisha kuwa, kuna mijadala shuleni mwangu. Kila Alhamisi, huwa na mijadala kwa lugha ya Kiingereza au Kiswahili. Siku ya mijadala kwa lugha ya Kiswahili inapofika, huwa nimeandaa mada ya wiki na kuwapa wanafunzi kutafuta hoja ambazo hujadiliwa siku ya mijadala kwa lugha ya Kiswahili. Wanafunzi wanapopungukiwa na hoja, mimi huchangia kwa kuwapa hoja zaidi ambazo hunakiliwa kwenye vitabu vya insha.’

Ingawa mahojiano kati ya mtafiti na wakuu wa idara yalionyesha kuwa kuna siku za mijadala katika shule hizi, baadhi ya wanafunzi walisema kuwa, mijadala hii huendeshwa na wanafunzi wenyewe au hata hukosekana kabisa. Hivyo athari yake

kwa somo la Kiswahili huwa hasi kwa sababu, baadhi ya wanafunzi huleta mzaha kwa kuchanganya lugha ya Kiswahili na Kiingereza. Aidha, hoja zinazowasilishwa huhitaji uelekezi wa mwalimu wa somo la Kiswahili ili kubaini ikiwa ziko sawa au la. Mwalimu wa somo la Kiswahili asipohudhuria, mijadala hii hukosa maana. Kwa hivyo, ili mijadala kwa lugha ya Kiswahili iweze kuwa na athari chanya kwa somo la Kiswahili, utafiti ulipendekeza ihudhuriwe na walimu wa somo la Kiswahili. Kulingana na Nyakeoga (2018), matokeo ya utafiti wake yalionyesha kuwa, mijadala husababisha matokeo mema katika somo la Kiswahili, ingawa athari yake itakuwa tu chanya ikiwa itatekelezwa ipasavyo na walimu wa somo la Kiswahili. Isipotekelezwa, itabakia tu kuwa kwenye kumbukumbu za mikutano na sheria za shule.

Utafiti huu pia uligundua kuwa, kuna baadhi ya shule kama vile Amukura ambazo hazitekelezi sana baadhi ya kanuni za lugha za shule kama vile mijadala, ingawa matokeo ya mtihani wa somo la Kiswahili mwaka uliopita yalikuwa mazuri. Shule hizi hutilia sana stadi andishi (Kusoma na Kuandika) kwa sababu stadi hizi ndizo hutahiniwa katika mtihani wa KCSE. Kanuni za lugha za shule hujikita sana katika stadi zungumzi (Kuzungumza na Kusikiliza) ambazo kwao sio muhimu. Baada ya wanafunzi hawa kumaliza shule za upili, unapata hawawezi kuwasiliana kwa lugha sanifu hata baada ya kupita mtihani. Kwa mfano, mkuu wa idara ya Kiswahili katika shule ya upili ya Chakol, alisema kuwa, ameshuhudia wanafunzi ambao kuwasiliana kwa lugha ya Kiswahili ni changamoto lakini matokeo yao katika somo la Kiswahili yalikuwa mazuri. Maoni haya pia yaliungwa mkono na mkuu wa idara ya Kiswahili katika shule ya upili ya Mundika. Mwalimu huyu alisema kuwa, mwanafunzi bora katika somo la Kiswahili mwaka 2019, alikuwa na changamoto katika kuwasiliana

katika lugha ya Kiswahili, lakini alipita somo hilo. Matokeo haya yanafanana na ya Babusa (2010). Katika utafiti wa Babusa (2010), alibaini kuwa, walimu katika shule za upili huwafundisha wanafunzi jinsi ya kukabili mtihani wa KCSE na baada ya hapo, wanafunzi wanasahau Kiswahili. Ilibainika kuwa, wanafunzi hawa, hata baada ya kupata alama nzuri katika mtihani wa mwisho, hawawezi kuwasiliana kwa Kiswahili sanifu. Jambo hili linafaa kubadilishwa na wizara ya elimu. Litabadilika tu kama wizara ya elimu itaanzisha utahini wa stadi nyingine za lugha kama vile kuzungumza na kusikiliza fauka ya kuandika na kusoma.

#### **4.2.5 Athari ya shughuli za idara ya Kiswahili kwa somo la Kiswahili**

Idara ni sehemu inayoshughulikia jambo fulani katika wizara, shirika au kampuni. Kila shule iliyofanyiwa utafiti katika Kaunti ya Busia, ina Idara ya Kiswahili. Idara hizi husaidia shule katika kutekeleza mipango mbalimbali ya shule ili iweze kufanikisha shughuli zinazohusu somo la Kiswahili. Idara hizi husaidia shule kuweka imara sheria na utaratibu ili kuiweka shule hii katika kiwango cha juu cha usomaji. Mahojiano kati ya mtafiti na wakuu wa idara ya Kiswahili ulibaini majukumu yafuatayo hutekelezwa na idara ya Kiswahili; Kuwafunza wanafunzi somo la Kiswahili, kuwaandaa wanafunzi kwa mtihani wa kitaifa wa KCSE, kuwaandaa wanafunzi ili kushiriki katika mashindano na tamasha za muziki na maigizo, kuwashirikisha wanafunzi katika mijadala shuleni na kwingineko kama shule zingine, katika redio na runinga, kuwaelekeza wanafunzi katika utunzi wa kazi za Kiswahili kama mashairi, tamthilia na nyimbo, kuwahamasisha wanafunzi kuhusu matumizi ya lugha sanifu na kupambana na lugha ya sheng.

Ili idara ya Kiswahili iweze kutekeleza majukumu iliyopewa, shughuli zifuatazo za idara ya Kiswahili hutekelezwa na walimu wa somo la Kiswahili kupitia ratiba inayoandaliwa katika idara. Shughuli hizi hujumuisha vipindi vya ziada vya somo la Kiswahili, makongamano ya ndani na nje ya shule, vyama vya Kiswahili pamoja na usomaji wa vitabu na magazeti. Swali ambalo mtafiti aliuliza kupitia mahojiano, *Eleza namna shughuli za idara ya Kiswahili zinavyoathiri somo la Kiswahili.*

#### **4.2.5.1 Athari ya vipindi vya ziada kwa somo la Kiswahili**

Vipindi vya ziada katika shule za upili kaunti ya Busia, inatokana na silabasi pana ya somo la Kiswahili na vipindi vichache vya somo la Kiswahili kwenye ratiba ya shule. Katika mfumo wa elimu wa 8-4-4, somo la Kiswahili na Kiingereza ni masomo ya lazima na hutahiniwa, ingawa idadi ya vipindi vya masomo haya katika ratiba ya shule za upili inatofautiana. Mahojiano ya ana kwa ana kati ya mtafiti na mkuu wa idara yalibaini yafuatayo ;

Kwanza, katika shule za upili kaunti ya Busia, swala la vipindi vichache vya somo la Kiswahili limekuwa changamoto kwa somo la Kiswahili. Hali hii imechangia shule za upili katika eneo hili kubuni vipindi vya ziada ili wapate muda wa kukamilisha silabasi na kufanya marudio. Mkuu wa idara ya Kiswahili katika shule ya Upili ya Lwanya alisema kuwa ;

‘Somo la Kiswahili lina silabasi pana zaidi ikilinganishwa na somo la Kiingereza. Kuna sehemu ya insha, ufahamu na ufupisho, sarufi na matumizi ya lugha, isimu jamii, fasihi simulizi, fasihi andishi inayojuimuisha riwaya, hadithi fupi, tamthilia na mwisho ushairi. Ili kumwandaa mwanafunzi vilivyo, kama idara ilibidi tuzungumze na uongozi wa shule ili tupewe muda zaidi kupitia vipindi vya ziada. Hii imetusaidia kuwaandaa wanafunzi wetu

vilivyo. Matokeo mema ya mtihani katika somo la Kiswahili pia ni kutokana na vipindi vya ziada.’

Swala la vipindi vichache vya somo la Kiswahili limeshughulikiwa na watafiti mbalimbali na hata kutoa mapendekezo lakini halijawahi kushughulikiwa. Kwa mfano, Akaka (2017) anasema kuwa, sera ya elimu kuhusu ufundishaji wa somo la Kiswahili ni miongoni mwa matatizo mengine mengi yanayokabili ufundishaji wa somo la Kiswahili katika shule za upili. Licha ya kuwa, Kiswahili ni lugha rasmi na ya taifa nchini, kwa muda mrefu, lugha hii haitumiwi kama lugha ya kufundishia. Somo la Kiswahili pia, limepewa vipindi vichache sana katika ratiba ya masomo ikilinganishwa na muda uliotengewa ufundishaji somo la Kiingereza. Mtafiti alipotazama ratiba ya masomo katika idara ya Kiswahili, ilibainika kuwa vidato vya kwanza na pili hupewa vipindi tano kwa wiki yaani kimoja kila siku. Vidato vya tatu na nne hupewa vipindi sita kwa wiki yaani kimoja kila siku isipokuwa siku moja ambapo vipindi viwili hufundishwa katika shule ya Upili ya Butula, Lwanya, Kisoko, Chakol, Amukura na Mundika. Katika somo la Kiingereza, vidato vya kwanza na pili kuna vipindi saba ilihali vya tatu na nne kuna vipindi vinane kwa wiki. Isitoshe, mwalimu wa somo la Kiswahili hutarajiwa kupitia vipengele hivi vyote na wanafunzi darasani kwa muda mfupi kuliko ule anaopewa mwalimu wa somo la Kiingereza. Ni kutokana na sababu hii, idara ya Kiswahili katika shule hizi sita ikabuni vipindi vya ziada ili wakamilishe silabasi kabla ya wanafunzi kufanya mtihani wa kitaifa.

Katika shule ya upili ya Makunda, vipindi vya ziada vimejumuishwa katika ratiba ya kawaida ya shule (Tazama kielelezo 1.4) Badala ya vipindi sita vya Kiswahili katika kidato cha tatu vinavyokubaliwa na wizara ya elimu, somo la Kiswahili

limetengewa vipindi nane ili waweze kukamalisha silabasi. Hii inawezekana tu kwa shule za upili ambazo hazina masomo ya ziada kama ya uchoraji, sayansi ya nyumbani, ujenzi au lugha za kigeni kama Kifaransa na Kijerumani.

Vilevile, utafiti ulibaini kuwa, vipindi vya ziada wakati mwingine hutumiwa na walimu katika majadiliano ya vikundi. Hii huwa na athari chanya kwa somo la Kiswahili kwa kuwa huimarisha stadi ya kuzungumza. Kwa mfano, katika shule ya Upili ya Chakol, mkuu wa idara ya Kiswahili alisema kuwa, vipindi vya ziada hutumiwa kuwaweka wanafunzi katika makundi ya mjadala. Wanafunzi hawa huelekezwa na walimu wa somo la Kiswahili. Matokeo ya utafiti yalidhihirisha kuwa, wanafunzi wanapoelekezwa na walimu wa somo la Kiswahili, huwa na athari chanya kwa somo la Kiswahili kwa sababu wanafunzi hupata motisha wa kusoma na kuuliza maswali kwa vipengele wasivyoelewa. Matokeo haya yaliwiana na ya Yuvinalis (2017) ambaye alisema kuwa, walimu wanapokuwa katika vikundi vya majadiliano, wanafunzi hupata motisha na huwa na mwelekeo chanya. Walimu hawa wanaposhiriki katika shughuli za vikundini, huchangia kuepusha changamoto zinazoweza kuibuka wanafunzi wakiwa pekee yao. Mkuu wa idara ya Kiswahili katika shule ya Chakol alisema pia, kutokana na vipindi vichache vya somo la Kiswahili katika ratiba ya shule, kama sio vipindi vya ziada, ingekuwa vigumu sana kupata muda wa kufanya majadiliano na wanafunzi.

Matokeo ya utafiti pia yalidhihirisha kuwa, ili mwanafunzi afanye vizuri na kujiamini katika somo la Kiswahili, anafaa kuandaliwa vyema kwa kumaliza silabasi na kufanya mazoezi ya kutosha. Hii inawezekana tu ikiwa shule itakuwa na vipindi vya ziada. Matokeo haya yanalingana na matokeo ya Okeyo, Kimemia, na Ndethiu (2023) wanaosema kuwa, wanafunzi wanapofanyiwa maandalizi mwafaka,

maandalizi haya huwapa imani kuu wanafunzi katika kufuzu. Wanafunzi hawa huishia kujiamini. Aidha, madai haya yanafanana na ya Simiyu (2013), anayesema kuwa, walimu wanapokamilisha silabasi mapema, huwasaidia wanafunzi kukuza dhana ya kujiamini na kuwaondolea wanafunzi hawa hofu ambayo huchangia na kuathiri kwa njia hasi matokeo yao. Utafiti wa Simiyu pia ulibaini kuwa, walimu katika shule za upili wanapitia changamoto wanapofundisha mada za lugha. Kwa hivyo, ili mada hizi ziweze kutekelezwa, muda zaidi unahitajika.

Utafiti pia ulibaini kuwa, licha ya somo la Kiswahili kuwa na vipindi vichache pia kuna changamoto katika kukamilisha silabasi. Walimu wa somo la Kiswahili wametwikwa jukumu la kufundisha somo lingine kando na somo la Kiswahili hata baada ya mapendekezo kutolewa. Mkuu wa idara ya Kiswahili katika shule ya Upili ya Amukura alisema kuwa, kutokana na uhaba wa walimu, ni vigumu kupata mwalimu wa somo la Kiswahili akifundisha somo la Kiswahili pekee. Huwabidi kufundisha somo lingine. Hali hii imechangia walimu hawa kutotekeleza kazi yao ipasavyo. Mwalimu mkuu katika shule ya upili ya Butula alisema kuwa ;

‘Ili kuwe na utendakazi mzuri kutoka kwa walimu wake, amewaajiri walimu wengine ili kupunguza mzigo. Kwa hivyo, hakuna mwalimu katika shule yake ambaye hufundisha masomo mawili. Hii imepunguza kazi kwa walimu wake na kuchangia matokeo mema, si kwa Kiswahili tu bali masomo mengine’.

Ingawa walimu wa somo la Kiswahili wana masomo mawili ya kufundisha, utafiti wa maktabani ulibaini kuwa, baadhi ya mapendekezo yaliyokuwa yakitolewa na tume mbalimbali za Kiswahili kuhusu mkabala wa elimu nchini hayajatekelezwa. Mapendekezo yaliofanywa na Tume ya Koech (1999) alipendekeza kuwa, masomo

ya lugha ya Kiswahili na fasihi ya Kiswahili, yafundishwe kama masomo mawili tofauti. Maoni sawia na haya pia yalitolewa na Akaka (2017) katika utafiti wake. Anasema kuwa, uamuzi wa kuunganisha vipengele vya lugha ya Kiswahili na fasihi umekuwa changamoto kwa walimu. Ilibainika katika utafiti wake kuwa, walimu hawa hujikuta wakiegemea zaidi upande wa fasihi kuliko lugha. Utafiti wake unaonyesha kuwa, fasihi huchangia matokeo mazuri ya mtihani wa kitaifa wa somo la Kiswahili. Hii ni kwa sababu, makosa ya sarufi hayazingatiwi sana wakati wa usahihishaji wa mitihani ya fasihi kama ilivyo katika mitihani ya lugha. Licha ya haya, utafiti wake pia ulibaini kuwa, mwalimu mmoja hawezi kumudu nyanja zote za somo la Kiswahili. Kwa hivyo, baadhi ya walimu huepuka kufunza sehemu ya lugha ili wasije wakaulizwa maswali wasiyoyaelewa wanapofundisha darasani.

Mahojiano ya ana kwa ana na wakuu wa idara ya Kiswahili pia yalidhihirisha kuwa, kando na sera ya lugha inayokipa somo la Kiswahili vipindi vichache kwenye ratiba, Tume ya kuwaajiri walimu nchini pia imechangia kuathirika kwa somo la Kiswahili kupitia sera ya kuajiri walimu nchini. Sera hii inapendelea somo la Kiingereza. Walimu wa somo la Kiswahili hupaswa kufundisha somo la Kiswahili pamoja na mojawapo ya masomo ya sayansi ya kijamii kama vile Jiografia, Dini, Historia na Hisabati. Kwa hivyo, mwalimu anayefundisha somo la Kiswahili hukabiliwa na kazi marudufu. Isitoshe, katika hali kama hii, mwalimu anayefunza somo la Kiswahili hukosa muda wa kutosha wa kuandaa na kuzama katika ufundishaji. Hii huwa na athari hasi kwa somo la Kiswahili. Maelezo haya yanalingana na ya Babusa (2010), aliyesema kuwa, walimu wa somo la Kiswahili hulazimishwa kufanya somo jingine la pili walilosomea. Alipendekeza kuwa, somo hili wagawe sehemu mbili kama vile somo la Kiingereza ambalo lina fasihi na lugha kama masomo mawili tofauti. Hivyo

mwalimu wa somo la Kiswahili afundishe tu somo la fasihi na lugha kama masomo mawili tofauti bila kuongeza somo la ziada. Hili litawafanya walimu wa somo la Kiswahili wabobee katika somo la Kiswahili na kuwa na mielekeo chanya kuhusu lugha ya Kiswahili. Matokeo ya utafiti yalibaini kuwa, shule ya upili ya Butula imedumisha matokeo mema katika mitihani ya kitaifa kwa sababu, walimu katika shule hii ni wengi na hufundisha tu somo moja.

#### **4.2.5.2 Athari ya makongamano ya ndani na nje kwa somo la Kiswahili**

Lengo la makongamano ya ndani au nje ya shule, ni kuwapa wanafunzi na walimu fursa ya kutangamana na wenzao nje ya darasa ili kupata maarifa mapya kando na yale ambayo wanajua. Katika nadharia ya Richards na Rodgers (1995) ya Kijumuia na Kibinadamu, wanasema kuwa, ujifunzaji ni jukumu la jumuiya ya wanafunzi pamoja na walimu. Katika shughuli za makongamano, wanafunzi pamoja na walimu wa somo la Kiswahili, hujifunza maarifa mapya kwa kushiriki na kutangamana na wenzao. Makongamano haya huwapa wanafunzi fursa ya kutumia njia mbalimbali za usomaji. Wanafunzi hunufaika hasa wanapokutana na wanafunzi wengine. Katika shule za utafiti Kaunti ya Busia, makongamano hutokea katika viwango tofauti tofauti, makongamano ya ndani mwa shule yanayojumuisha viwango vya madarasa kwa madarasa, kati ya mikondo tofauti na hata bweni tofauti. Makongamano ya nje ya shule hutokea baina ya shule moja na nyingine au walimu wa somo la Kiswahili wanapoalikwa kuhudhuria kongamano au warsha ili kunoa ujuzi wake katika somo la Kiswahili. Maelezo haya ni sawia na utafiti wa Koko (2016) kwamba, makongamano hutokea katika viwango tofauti, makongamano ya ndani na yale ya nje ya shule. Utafiti ulibaini kuwa, katika shule ya upili ya Butula, Lwanya, Kisoko,

Chakol na Mundika, matokeo mazuri ya mitihani yanatokana na makongamano ya ndani na nje ya shule kama ilivyojadiliwa ;

#### **4.2.5.2.1. Athari ya Makongamano ya ndani ya shule kwa somo la Kiswahili**

Makongamano ya ndani ya shule ni kati ya shughuli za idara ya Kiswahili ambazo huandaliwa ili wanafunzi wawe na mielekeo chanya na kuweza kufanya vizuri katika somo la Kiswahili. Katika shule za upili Kaunti ya Busia, utafiti ulidhirisha kuwa, shule ya upili ya Mundika na shule ya upili ya Kisoko huandaa makongamano ya ndani ya shule ‘ Siku ya Kiswahili’ kama njia ya kutekeleza kanuni za lugha za shule. Mwalimu mkuu katika shule ya upili ya Mundika alisema kuwa, wanafunzi wanapopewa fursa ya kushiriki katika makongamano ya ndani ya shule, huwasaidia katika kutoa ujuzi wao waliofunzwa darasani na nje ya darasa. Pia, hukuza vipaji vyao wanapoiingiliana na wengine katika uwanja wa mawasiliano. Mkuu wa idara ya Kiswahili katika shule ya Kitaifa ya Butula pia alikuwa na haya ya kusema ;

‘Idara ya Kiswahili pamoja na chama cha Kiswahili cha wanafunzi CHAKIBU, kimepewa jukumu la kuandaa makongamano ya ndani ya shule. Ratiba ya shughuli ya siku huandaliwa. Siku hii huwaleta wanafunzi pamoja kwa shughuli mbalimbali. Huwa na mashindano kati ya kidato cha kwanza na pili, kidato cha tatu na nne. Nyimbo na mashairi ambayo hutungwa na wanafunzi huwasilishwa siku hii. Kama njia ya kuwapa motisha, washindi hutunukiwa zawadi. Ni sheria kwa kila mwanafunzi kuzungumza lugha sanifu. Walimu pia huwa pale kuwaelekeza wanafunzi.’

Katika shule ya Butula, mkuu wa idara ya Kiswahili alisema kuwa, tangu kuanzishwa kwa makongamano ya ndani ya shule, wameshuhudia matokeo mema katika somo la Kiswahili. Na sio matokeo mema tu, wanafunzi huwasiliana pia kwa lugha sanifu. Aidha maoni haya pia yalitolewa na mkuu wa shule ya upili ya Lwanya

ambaye alisema kuwa, tangu aanze kufadhili makongamano ya ndani ya shule, matokeo ya somo la Kiswahili yamekuwa yakiimarika kila mwaka. Matokeo haya ya utafiti yanawiana na ya Nyakeoga (2018) aliyesema kuwa, wanafunzi wanapopewa fursa ya kushiriki katika mashindano ya shule, kujadiliana na kuwasiliana kwa lugha sanifu, matokeo yao katika somo la Kiswahili huimarika pia.

Matokeo ya utafiti pia yalidhihirisha kuwa, sio shule zote katika Kaunti ya Busia huandaa makongamano ya ndani ya shule. Kati ya shule saba za utafiti, Shule mbili hazina shughuli ya aina hii. Mkuu wa idara ya Kiswahili katika shule ya upili ya Makunda alisema kuwa ;

‘Wametamani kwa muda mrefu kuwa na makongamano ya aina hii, lakini changamoto ni ufadhili kutoka uongozi wa shule. Shughuli kama kuzawadi washindi wa siku, motisha kwa watahini walioalikwa kuzungumza na wanafunzi huhitaji ufadhili kutoka uongozi wa shule. Ukosefu wa shughuli za aina hii inaweza kuwa sababu ya matokeo duni katika somo la Kiswahili shuleni mwetu.’

Wanafunzi katika shule ambazo shughuli ya aina hii haitekelezwi, huwa hawana motisha ya kuwafanya kupenda kanuni za lugha hivyo kuwa na athari hasi kwa somo la Kiswahili. Maelezo haya ni sawa na maoni ya Nyongesa na wenzake (2022), wanaosema kuwa, ili kanuni za lugha ziweze kutekelezwa, motisha ni muhimu sana kwa walimu na wanafunzi. Matokeo ya utafiti wao yalionyesha kuwa, wanafunzi wanapopewa motisha, wao hutekeleza kanuni za lugha za shule, na matokeo ya mtihani katika somo la Kiswahili huwa mazuri. Wanjiku (2014), naye alisema kuwa, utafiti wake ulibaini kuwa, shule nyingi hazikushiriki katika makongamano ya ndani ya shule, kwa hivyo hali hii iliathiri ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili kwa sababu mwanafunzi hukosa kufanya mazoezi zaidi ya yale ambayo amefunzwa na

mwalimu. Kando na makongamano ya ndani mwa shule, pia kuna yale ya nje ya shule.

#### **4.2.5.2.2. Athari ya Makongamano ya nje ya shule kwa somo la Kiswahili.**

Makongamano ya nje ya shule pia hutokea katika viwango tofauti tofauti. Kuna yale ambayo wanafunzi kutoka shule moja hualikwa na shule nyingine hasa inayofanya vyema katika somo la Kiswahili. Kuna pia makongamano ya wanafunzi ambayo huandaliwa kati ya mataifa ingawa utafiti ulionyesha hakuna shule katika Kaunti ya Busia ambayo imewahi kushiriki katika makongamano ya aina hii. Aidha, kuna makongamano ya walimu wa somo la Kiswahili kualikwa katika warsha. Haya yote hufanywa ili kupata maarifa mapya katika somo la Kiswahili. Matokeo ya utafiti kupitia mbinu ya mahojiano ya ana kwa ana na wakuu wa idara ya Kiswahili yalibaini kuwa, kabla ya wanafunzi kushiriki na wanafunzi wengine katika makongamano ya nje ya shule, maswali kuhusu mada ya masuala ibuka hutolewa kwa wanafunzi ili kwenda kufanyia utafiti. Maswali haya hujadiliwa na kuwasilishwa siku hiyo. Washindi hutunikiwa kwa kupigiwa makofi au kupewa zawadi.

Kutokana na utafiti, imebainishwa kwamba, makongamano ya nje yanapendwa sana na wanafunzi wote ingawa si shule zote hufadhili shughuli ya aina hii. Makongamano haya huwa kama motisha kwa wanafunzi na huwapa wanafunzi ari ya kufanya vizuri katika somo la Kiswahili ili wachaguliwe kati ya wanafunzi wanaoenda nje ya shule. Katika shule ya upili ya Butula, mkuu wa idara alisema kuwa, wanafunzi wengi wamejisajili kwa chama cha Kiswahili ili waweze kuhudhuria makongamano ya nje ya shule. Makongamano haya huwa kama motisha ya kuhakikisha kuwa wanafunzi wanajiunga na chama hiki na pia kutekeleza kanuni

za lugha za shule. Maoni sawia na haya yalitolewa na Nyongesa na wenzake (2022) waliobaini kuwa, motisha huchangia matumizi mazuri ya lugha ya Kiswahili katika shule za upili. Ukosefu wa motisha huwa na athari hasi katika utekelezaji wa kanuni ya lugha ya shule. Njia moja ya kuwapa wanafunzi hawa motisha ni kuwapeleka katika shule jirani kwa makongamano ya nje ili waendeleo kutii sheria hizi.

Utafiti pia ulibaini kuwa, Makongamano humpa mwanafunzi nafasi ya kutangamana na wanafunzi kutoka shule nyingine na kupata maarifa ambayo hawajafunzwa shuleni mwao. Aidha makongamano haya hukuza kipawa cha ujasiri. Ili mwanafunzi aweze kujadili mada fulani mbele ya wengine, ni lazima awe na ujasiri. Ujasiri huu humsaidia hata baada ya kumaliza masomo ya sekondari. Kulingana na Ongaro (2019), katika *Gazeti la Taifa Leo*, Bi. Rose Ndichu ambaye ndiye Mkurugenzi mkuu wa Kenya National Debates Council (KNDC) alisema kuwa, mashindano katika makongamano ni muhimu sana. Mashindano haya huwapa wanafunzi msukumo wa kujieleza wazi katika umati bila kuwa na wasiwasi wowote. Aliendelea kwa kusema kuwa, mashindano haya huwa kama mwongozo mzuri kwa wanafunzi kwa sababu huwafanya wanafunzi hawa kuwa watu wa kutegemea siku za usoni. Mwanafunzi akiwa mkakamavu wakati anapojieleza, bila shaka hata maisha yake ya baadaye yataimarika. Bi. Ndichu alisema kuwa, mashindano haya huwasaidia wanafunzi wa shule za upili hasa wanapofika katika vyuo vya juu. Mashindano haya huwafanya kupevuka kimawazo na huwasaidia kujieleza bila wasiwasi.

Kando na makongamano ya wanafunzi, walimu pia huandaliwa warsha ili kujifunza ujuzi mpya. Makongamano haya huandaliwa na wizara ya elimu ama shule fulani kwa kuwaalika walimu (Tazama kielelezo 1.5). Kulingana na Peters (1980), utafiti

wake ulionyesha kuwa, maarifa huendelea kubadilika kulingana na wakati au huibuka kutokana na mambo mapya. Maandalizi ya nyanjani ni muhimu katika kutekeleza ufundishaji wa mambo mapya na kuvuta kumbukumbu ya yale yaliyosahaulika. Kwa hivyo, utafiti wake ulipendekeza kuwa, walimu wote wapewe fursa ya kuhudhuria warsha, semina ili kupiga msasa ili waweze kupata maarifa. Katika shule za upili Kaunti ya Busia, ilibainika kwamba, ingawa kuna warsha ambazo huandaliwa kwa walimu wa somo la Kiswahili, warsha hizi huhitaji ufadhili kutoka uongozi wa shule. Hii huwa changamoto kwa shule ambazo hazina uwezo wa kifedha. Kiongozi wa idara ya Kiswahili katika shule ya upili ya Makunda ambaye hajawahi kupata fursa ya kuhudhuria warsha hii, alisema kuwa ingekuwa bora zaidi ikiwa wizara ya elimu ingechukua jukumu la kuandaa warsha za aina hii na kuwaalika walimu wote wa somo la Kiswahili katika Kaunti hii.

Wakuu wa idara ya Kiswahili katika shule ya upili ya Amukura na Makunda walisema kuwa, matokeo duni ya wanafunzi katika mtihani wa kitaifa katika shule zao huenda yalisababishwa na walimu wa somo la Kiswahili kukosa kuhudhuria warsha za aina hii. Kuna mbinu mpya za utahini na namna ya kusahihisha kazi ya wanafunzi hufundishwa katika warsha hizi. Ogero (2012) katika uchunguzi wake, anahimiza umuhimu wa walimu kuhudhuria mafunzo. Anasema kuwa, mafunzo haya huwasaidia walimu kujikumbusha mara kwa mara ili kuimarisha stadi zao za kufundisha lugha. Suter (2013) anakubaliana naye kwa kusema kuwa, ni sharti walimu wawe sambamba na maendeleo ya kisasa ya ufundishaji lugha. Aidha walimu hawa wanafaa kujifunza mbinu za kisasa za kufundishia kupitia kwa mafunzo- kazini. Kupitia kwa semina, warsha, makongamano na mikutano ya majopo ya walimu wa lugha, walimu hawa wanaweza kupata maarifa mapya.

Walimu wa somo la Kiswahili pia walilalamikia ubaguzi unaosababishwa na wizara ya elimu. Hivi karibuni wameshuhudia wizara hii ikiandaa warsha kwa walimu wa Kiingereza, Hesabu na Sayansi huku wakiwasahau walimu wa somo la Kiswahili. Matokeo haya ya utafiti yanawiana na ya Akaka (2017) aliyesema kuwa, matokeo duni katika somo la Kiswahili yamesababishwa na kukosekana kwa warsha za kuwapiga msasa walimu wa Kiswahili. Uchunguzi wake ulibaini kuwa, warsha hizi huandaliwa mara moja kila mwaka kwa walimu wote wa masomo ya Sayansi na Hisabati kote nchini.

#### **4.2.5.3 Athari ya vyama vya Kiswahili kwa somo la Kiswahili**

Katika shule za upili, kuna vyama mbalimbali ambavyo hutekeleza wajibu wa kuimarisha lugha ya Kiswahili na Kiingereza. Kuna vyama vya Kiswahili na kile cha Wanahabari. Matokeo ya utafiti pia yalibaini kuwa, chama cha wanahabari hushughulikia habari zinazojitokeza shuleni katika lugha ya Kiswahili au Kiingereza. Katika shule za upili za Lwanya, Chakol, Makunda na Butula, kila Ijumaa, habari huwasilishwa kwa gwaride kwa lugha sanifu ya Kiswahili. Hii imekuwa na athari chanya kwa somo la Kiswahili.

Katika shule ya upili ya Butula, wana chama cha Kiswahili, CHAKIBU. Chama hiki huwasajili wanafunzi wa kidato cha kwanza wanapoingia shuleni. Majukumu yanayotekelezwa na chama hiki ni kama, kuandaa mijadala kila wiki, kuhakikisha kuwa wanafunzi wanazungumza lugha sanifu, kushirikiana na idara ya Kiswahili katika kuandaa makongamano ya ndani mwa shule, na wanachama wake pia hushiriki kwa kukusanya habari zinazoibuka na kuwasilisha kwenye gwaride siku ya Ijumaa. Majukumu haya yote huimarisha lugha ya Kiswahili kwa sababu wanafunzi hutafuta misamiati watakayoitumia wanapowasilisha habari hizi.

Matokeo haya ya utafiti yanafanana na ya Koko (2016), aliyesema kuwa, vyama vya Kiswahili hutokeleza majukumu ya kuhakikisha kuwa lugha sanifu inatumiwa shuleni. Pia hupiga marufuku uzungumzi wa sheng, kuandaa mijadala na makongamano ya ndani na nje ya shule. Kwa mujibu wa Adungo (2019), alipokuwa akirejelea, CHAMAKINJE (Chama cha Kiswahili cha Njega), alisema kuwa, chama hiki kina malengo ya kuendeleza lugha ya Kiswahili kwa dhati ndani na nje ya shule. Chama hiki kinatarajia kuwapa wanafunzi jukwaa la kuhudhuria makongamano na kuzuru shule mbalimbali za upili na msingi. Hali hii itawahamasisha wanafunzi kuhusu umuhimu wa Kiswahili kama somo la utahini na pia kitega uchumi. Katika shule ya upili ya Butula, mtafiti alibaini kuwa Chama cha Kiswahili kimekuwa cha manufaa sana kwa somo la Kiswahili. Mwanafunzi mmoja alisema kuwa;

‘Ndoto yangu ni kuwa mwanahabari siku moja. Tangu niujiunge na Chama cha Kiswahili katika shule hii, naona ndoto yangu ya kuwa mwanahabari ikitimia. Kupitia chama hiki, ujuzi wangu katika lugha ya Kiswahili umenolewa vilivyo. Matokeo yangu katika mitihani ya somo la Kiswahili pia ni mazuri.’

Matokeo ya utafiti yalitambua mchango wa vyama vya Kiswahili katika shule ya Upili ya Butula ni muhimu katika somo la Kiswahili. Ilibainika kuwa, majukumu ya chama cha Kiswahili katika shule hii ni kuchapisha jarida la chama. Jarida hili litazingatia mijadala muhimu katika taaluma za Kiswahili ili kuwapa wanafunzi nafasi ya kujieleza na kukuza vipaji vyao katika nyanja mbalimbali. Aidha katika shule ya upili ya Lwanya, ingawa hawana chama cha Kiswahili, jukumu la kuchapisha jarida la shule limepewa Chama cha Uanahabari. Chama hiki kimepewa jukumu la kuchapisha jarida katika lugha ya Kiingereza na Kiswahili. Matokeo haya yanawiana na maoni katika gazeti la Taifa Leo, Adungo (2019), alisema kuwa Chama cha Kiswahili katika Shule ya upili ya Njega, Kirinyaga, kimewawezesha

wanafunzi wa shule hii kupiga hatua na kutia fora si kuendeleza Kiswahili tu kama lugha bali pia kuimarisha matokeo ya mitihani ya kitaifa ya KCSE. Kama shule ya upili ya Butula ambayo chama cha Kiswahili kimekuza somo la Kiswahili, shule ya upili ya Njega pia imekuwa kati ya shule zinazojivunia matokeo bora zaidi katika Kaunti ya Kirinyaga.

#### **4.2.5.4 Athari ya usomaji wa vitabu na magazeti kwa somo la Kiswahili**

Kwa mujibu wa Ngoge (2014), magazeti ni machapisho yanayochapisha nakala nyingi kila wiki au siku. Uchunguzi wake ulibaini kuwa, Gazeti la Taifa Leo ndilo gazeti la kipekee linalotambuliwa na pia linaloandikwa kwa lugha ya Kiswahili. Kwa hivyo, utafiti ulibaini kuwa, gazeti la Taifa Leo ndilo hununuliwa katika shule za upili katika Kaunti ya Busia.

Matokeo ya utafiti yalibaini kuwa, baadhi ya shule za upili hupendelea kununua gazeti la Kiingereza. Kwa mfano katika shule ya upili ya Mundika, utafiti ulibaini kuwa ni gazeti la Kiingereza tu ambalo hununuliwa na uongozi wa shule. Hali hii imeathiri vibaya somo la Kiswahili kwa sababu wanafunzi katika shule hii huibuka kuwa na mielekeo chanya kuhusu lugha ya Kiingereza na hasi kwa lugha ya Kiswahili. Owala (2014), alipendekeza kuwa, mwalimu anayefunza lugha ya pili anafaa kufanya mipangilio ili wanafunzi waweze kununuliwa magazeti yanayohusu lugha hiyo. Mkuu wa idara katika shule ya upili ya Mundika, alisema kuwa, juhudi zake za kukumbusha uongozi wa shule kununua Gazeti la Taifa leo zimembulia patupu. Kwa hivyo imekuwa vigumu sana kwa wanafunzi hawa kusoma gazeti la Kiswahili wakiwa shuleni.

Katika shule za upili za Butula na Shule ya upili ya Chakol, wakuu wa idara ya Kiswahili walisema kuwa, idara imeandaa siku maalumu ya kusoma vitabu vya hadithi au magazeti kwa lugha ya Kiswahili. Mwalimu wa somo la Kiswahili huwa pale ili kuhakikisha kuwa wanafunzi hawa wanasoma vitabu vile. Usomaji wa vitabu vya hadithi umewawezesha wanafunzi kuwa na umilisi wa juu wa lugha ya Kiswahili. Matokeo yao ya mtihani yamekuwa mazuri hasa kwa fasihi andishi. Aidha misamiati ya lugha ambayo wao hujifunza kutoka kwenye vitabu hutumika katika uandishi wao wa lugha. Matokeo haya ya utafiti yanaoana na ya utafiti wa Okeyo na wenzake (2023), ambayo yalidhihirisha kuwa, huenda matumizi ya vitabu vya hadithi iliawezesha wanafunzi kufanya vyema katika shule za Kakamega mijini kuliko wenzao wanaopatikana sehemu ya Kisumu na kule mashambani.

Katika shule za Upili za Amukura na shule ya upili ya Makunda, wakuu wa idara ya Kiswahili walikubaliana kuwa, changamoto wanazopitia kama walimu wa somo la Kiswahili ni kuhakikisha kuwa wanafunzi wanasoma vitabu vya hadithi hasa wanafunzi wavulana. Hii imesababisha athari hasi kwa somo la Kiswahili. Maoni haya pia yaliungwa na mkuu wa idara ya Kiswahili ya Mundika aliyesema kuwa, wanafunzi wa siku hizi hasa wavulana hawapendi kusoma vitabu vya hadithi. Hali hii pia imechangia matokeo duni hasa katika fasihi andishi. Matokeo haya ya utafiti yanaoana na maoni ya Chacha (2016) aliyegundua kuwa, wanafunzi ambao hawasomi vitabu vya hadithi vya kutosha hawawezi kuimudu lugha kwa ufasaha. Ili kuwapa wanafunzi maandalizi mema zaidi na kuimarisha ujuzi wao, walimu waliwapa maswali na mitihani mingi kutoka katika vitabu teule vya hadithi.

#### **4.4 Hitimisho**

Sura hii ililenga kufafanua athari ya kanuni za lugha za shule kwa somo la Kiswahili. Utafiti huu ulibaini udhaifu katika utekelezaji wa kanuni za lugha za shule hasa katika shule zenye matokeo duni katika mtihani wa somo la Kiswahili. Mtafiti alibaini kuwa, licha ya kila shule ya upili kuwa na kanuni za lugha za shule, kuna changamoto katika utekelezaji wake kutoka kwa wizara ya elimu, uongozi wa shule, walimu wa somo la Kiswahili, walimu wa masomo mengine na hata wanafunzi. Ilibainika katika utafiti huu kuwa, wanafunzi wanapowasiliana kwa lugha sanifu, kunakuwa na athari chanya kwa somo la Kiswahili lakini wanapowasiliana kwa lugha za asili au sheng', athari yake inakuwa hasi. Mabango na maandishi yanayopatikana kwa mazingira ya shule yanakitukuza Kiingereza na masomo mengine hivyo kuwa na athari hasi kwa somo la Kiswahili. Uchunguzi huu pia ulibaini kuwa, walimu wa somo la Kiswahili wanaposhirikiana na wanafunzi katika mijadala ya shule kwa lugha ya Kiswahili, makongamano ya ndani na nje ya shule, usomaji wa vitabu vya hadithi na magazeti na uundaji wa vyama vya Kiswahili, kutakuwa na athari chanya kwa somo la Kiswahili. Sura ambayo inafuata ndiyo itakayotamatisha uchunguzi huu.

## **SURA YA TANO**

### **HITIMISHO, MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UTAFITI**

#### **5.0. Utangulizi**

Sura hii ndiyo iliyokamilisha utafiti huu. Sura hii ilishughulikia muhtasari wa utafiti, matokeo ya utafiti, mchango wa utafiti, changamoto zilizoibuka wakati wa kufanya utafiti na mapendekezo ya utafiti.

#### **5.1 Muhtasari wa utafiti**

Utafiti huu ulichunguza namna mielekeo ya wanafunzi na walimu wa sekondari kuhusu kanuni za lugha za shuleni zinavyoathiri somo la Kiswahili. Shule saba za upili katika Kaunti ya Busia zilichunguzwa ili kutambua kanuni za lugha za shule na mielekeo ya walimu na wanafunzi kuhusu kanuni hizi. Utafiti huu pia ulichunguza ikiwa kuna athari ya kanuni za lugha za shule kwa somo la Kiswahili.

Katika sura ya kwanza ya tasnifu, ilieleza usuli wa mada ambapo mitazamo tofauti ya watafiti kuhusu suala la sera ya lugha ya taifa kwa jumla na kanuni za lugha za shule ilidhihirika. Vipengele vilivyoshughulikiwa ni pamoja na, Suala la utafiti, maswali na malengo ya utafiti, sababu za kuchagua mada ya utafiti, upeo na mipaka ya utafiti, yaliyoandikwa kuhusu mada, misingi ya nadharia na mbinu za utafiti.

Sura ya pili ilichunguza kanuni za lugha za shule zinazojitokeza katika shule za upili kaunti ya Busia. Katika nadharia ya Kijumuia na Kibinadamu ya Richards na Rodgers (1995) wanapendekeza namna ya ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya pili. Katika kujifunza lugha ya pili, mwalimu ana jukumu la mshauri na msaidizi wa mwanafunzi na inasisitiza ufunzaji ulio na utu na ubinadamu. Katika utekelezaji wa

kanuni za lugha za shule, usalama wa mwanafunzi ni muhimu sana. Wanafunzi hawawezi kujifunza lugha vizuri wakiwa na wasiwasi ya adhabu au kutojisikia salama. Mihimili ya nadharia hii ilitumika kubainisha kanuni za lugha za shule. Utafiti ulibaini kuwa katika utekelezaji wa kanuni hizi, wakati mwingine usalama wa mwanafunzi kupitia adhabu za shule huwa hauzingatiwi hivyo kuathiri ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili. Hojaji kwa wanafunzi na wakuu wa idara ya Kiswahili pamoja na mahojiano kwa walimu wakuu pia yalitambua kanuni za lugha shuleni. Kanuni za lugha shuleni zilizobainishwa ni; Lugha ya mawasiliano katika mazingira ya shule, siku za Kiswahili, mabango na maandishi katika mazingira ya shule, matumizi ya lugha ya Kiswahili katika mijadala na shughuli za idara ya Kiswahili.

Sura ya tatu ilichunguza mielekeo ya wanafunzi na walimu wa somo la Kiswahili kuhusu kanuni za lugha shuleni. Mihimili miwili ya nadharia ya Vitendo vilivyofikiriwa ya Ajzen na Fishbein (1980) ilitumika kubainisha mielekeo ya wanafunzi na walimu kuhusu kanuni za lugha za shule. Watangulizi wa nadharia hii wanaeleza kuwa, binadamu hufanya jambo ambalo litamnufaisha. Hii huchangia basi mtazamo kubalifu kuhusu jambo hilo. Isitoshe, ikiwa jambo hilo halitakuwa na manufaa kwake, binadamu atakuwa na msimamo usiokubalifu. Matokeo ya utafiti yalionyesha kuwa, wanafunzi na walimu wa somo la Kiswahili walikuwa na mielekeo chanya kwa kanuni za lugha za shule ambazo ziliwanufaisha na kuwa na mielekeo hasi kwa zile kanuni za lugha za shule ambazo hazikuwanufaisha kwa somo la Kiswahili. Vilevile, mtafiti alitumia hojaji likati kwa wanafunzi na wakuu wa idara ya Kiswahili, majadiliano elekezi ya vikundi kwa wanafunzi na mahojiano ya ana kwa ana kwa wakuu wa idara ya Kiswahili. Matokeo ya utafiti yalionyesha kuwa, walimu na wanafunzi wa shule za upili wanapenda kanuni za lugha za shule

ingawa mielekeo yao chanya huathiriwa na nafasi inayopewa lugha ya Kiswahili katika mazingira ya shule licha ya kuwa lugha rasmi na ya taifa. Mielekeo hasi ya wanafunzi hutokana na mielekeo hasi ya walimu na adhabu wanayopata wakati wanapoenda kinyume na kanuni za lugha za shule. Adhabu hizi huwapa aibu.

Sura ya nne ilichunguza athari ya kanuni za lugha za shule kwa somo la Kiswahili. Matokeo ya mtihani kutoka shule saba za utafiti, mahojiano ya ana kwa ana kwa wakuu wa idara ya Kiswahili pamoja na mihimili ya nadharia ya Kijumuia na Kibinadamu ya Richards na Rodgers (1995) ilitumika kubainisha athari ya kanuni za lugha kwa somo la Kiswahili. Mhimili wa pili wa nadharia hii ni ule unaosema kuwa, kutomakinika kwa wanafunzi kupunguzwe hasa kwa kuwapa majukumu tofauti tofauti shuleni. Kanuni za lugha za shule kama matumizi ya lugha ya Kiswahili katika mijadala, makongamano ya ndani na nje ya shule pamoja na vyama vya Kiswahili, huwasaidia wanafunzi kumakinika katika mawasiliano kwa kuonyesha ujuzi waliojifunza katika somo la Kiswahili. Hii huasabisha athari chanya kwa somo la Kiswahili. Mhimili wa mwisho unaosema kuwa, ujifunzaji ni jukumu la jumuiya ya wanafunzi pamoja na walimu ulitumikizwa kubaini umuhimu wa ushirikiano kati ya walimu na wanafunzi katika kufanikisha utekelezaji wa shughuli za idara ya Kiswahili katika kuimarisha somo la Kiswahili. Ilibainika kuwa, njia sawa ya kuhakikisha kuwa kanuni za lugha zimekuwa na athari nzuri kwa somo la Kiswahili ni ushirikiano wa walimu na wanafunzi katika utekelezaji wake.

## 5.2 Matokeo ya utafiti

Utafiti ulichanganua namna mielekeo ya wanafunzi na walimu wa sekondari kuhusu kanuni za lugha shuleni zinavyoathiri somo la Kiswahili katika Kaunti ya Busia. Mihimili ya nadharia ya Kijumuia na Kibinadamu na ile ya Vitendo vilivyofikiriwa ndiyo iliongoza utafiti huu. Mbinu za mahojiano, hojaji likati, hojaji likati, mjadala elekezi wa makundi, uchunzaji na matokeo ya mitihani ya somo la Kiswahili zilitumika kupata matokeo ya utafiti huu. Data ilipochanganuliwa, matokeo ya utafiti yalithibitisha tafiti zilizofanywa na watafiti wengine awali. Tafiti hizi zilithibisha kuwa, shule za upili tofauti zina kanuni za lugha za shule tofauti. Kanuni za lugha za shule zina athari kwa somo la Kiswahili na matokeo ya mitihani ya Kitaifa. Baadhi ya mambo yaliyojitokeza na ambayo yana uhusiano na kanuni za lugha za shule yalijadiliwa katika sura ya pili.

Sura ya pili ilichanganua kanuni za lugha shuleni. Ilibainika kuwa, kanuni za lugha za shule ni kama, lugha ya mawasiliano katika mazingira ya shule, siku za Kiswahili, mabango na maandishi katika mazingira ya shule, matumizi ya lugha ya Kiswahili katika mijadala na shughuli za idara ya Kiswahili. Shughuli hizi ni kama; vipindi vya ziada, makongamano ya ndani na nje ya shule, vyama vya Kiswahili na usomaji wa vitabu na magazeti. Kanuni hizi zilibainika kupitia hojaji kwa wanafunzi na walimu wa somo la Kiswahili ambao ni wakuu wa idara ya Kiswahili. Mahojiano ya ana kwa ana na walimu wakuu wa shule za upili pia yalidhihirisha sababu ya uteuzi wa kanuni hizi.

Sura ya tatu, ilichunguza mielekeo ya wanafunzi na walimu wa somo la Kiswahili kuhusu kanuni za lugha za shule. Matokeo ya utafiti yalibaini kuwa, wanafunzi wana mielekeo chanya kuhusu kanuni za lugha za shule hasa ambazo zina manufaa katika somo la Kiswahili. Kanuni hizi ni kama mawasiliano kwa lugha sanifu, matumizi ya mijadala kwa lugha ya Kiswahili, makongamano ya ndani na nje ya shule, vyama vya Kiswahili na usomaji wa vitabu na magazeti katika lugha ya Kiswahili. Wanafunzi walioonyesha mielekeo hasi kwa kanuni za lugha zinazoshusha hadhi yake. Kwa mfano, unapoingia katika mazingira ya shule za upili, utakutana na mabango na maandishi katika lugha ya Kiingereza. Idadi ya siku inayopewa lugha ya Kiswahili katika mawasiliano pia ni chache ikilinganishwa na lugha ya Kiingereza. Hii hufanya wanafunzi kudunisha lugha ya Kiswahili hivyo kuchangia mielekeo hasi. Wizara ya elimu pia imetenga vipindi vichache vya lugha ya Kiswahili katika ratiba ya shule. Hii hufanya shule kubuni vipindi vya ziada ambavyo havipendwi na baadhi ya walimu na wanafunzi. Ilibuuka kuwa, baadhi ya walimu shuleni wana mielekeo hasi kuhusu kanuni za lugha za shule. Hii huchangia mielekeo hasi pia kwa wanafunzi ambao huiga wanachofanya walimu wao. Adhabu zinazotolewa na walimu kwa wanafunzi wanaoenda kinyume na kanuni za lugha za shule pia husababisha mielekeo hasi kwa kanuni hizi. Ilibainika kuwa, wanafunzi wanapowasiliana kwa lugha ya Kiswahili siku ya Kiingereza, wanafunzi hawa hupewa adhabu za aibu kama kuvaa mavazi ya aibu yalioandikwa '*I am a language breaker*'. Hii ni tofauti na mwanafunzi anapowasiliana kwa lugha ya Kiingereza siku ya Kiswahili.

Fauka ya haya, utafiti ulibaini katika sura ya tatu kuwa, mielekeo hasi kuhusu kanuni za lugha shuleni pia ilitokana na changamoto zinazokabili shule za viwango vya Kaunti ama zile ambazo hazina uwezo wa kufadhili shughuli za idara ya Kiswahili. Utafiti ulibaini kuwa, motisha ni kipengele muhimu katika kubadilisha mielekeo ya walimu na wanafunzi kuhusu kanuni za lugha shuleni kuwa chanya. Kutokana na ukosefu wa ufadhili kutoka kwa uongozi wa shule, baadhi ya shughuli za idara ya Kiswahili hazijaweza kutekelezwa. Hii imechangia mielekeo hasi dhidi ya kanuni hizi. Shughuli kama makongamano ya nje kwa wanafunzi na walimu wa somo la Kiswahili husababisha mielekeo chanya. Na ni shughuli za aina hii ambazo huhitaji ufadhili.

Sura ya nne ilifafanua athari ya kanuni za lugha za shule katika somo la Kiswahili. Mtafiti alibaini kuwa, wanafunzi wanapowasiliana kwa lugha sanifu bila kuchanganya sheng' au lugha za asili, huwa na athari chanya kwa somo la Kiswahili. Walimu katika shule za kutwa, wana changamoto katika utekelezaji wa kanuni za lugha za shule zinazohitaji wanafunzi kuwasiliana katika lugha sanifu. Tatizo lilipo ni kuwa, wanafunzi hawa wanaporudi nyumbani, lugha wanayotumia katika mawasiliano na wanakijiji ni sheng' au za kienyeji. Kwa hivyo ili kusuluhisha tatizo hili, shughuli za idara ya Kiswahili zinazowapa wanafunzi fursa ya kuwasiliana kwa lugha sanifu, zinafaa kutekelezwa. Isitoshe, muda unaotengewa mawasiliano kwa lugha ya Kiswahili ni mchache, hivyo kusababisha matokeo duni katika mitihani ya Kitaifa na somo la Kiswahili. Kanuni za lugha za shule kama mijadala, mawasiliano kwa lugha sanifu, makongamano ya ndani na nje ya shule, vyama vya Kiswahili, vipindi vya somo la Kiswahili na usomaji wa vitabu na magazeti zinahitaji ushirikiano. Changamoto iliyopo ni hakuna ushirikiano katika utekelezaji wa kanuni

za lugha za shule kutoka kwa wizara ya elimu, uongozi wa shule, walimu na wanafunzi. Kwa hivyo, ili kanuni hizi ziweze kuwa na athari chanya kwa somo la Kiswahili na kuwe na matokeo mazuri katika mitihani ya Kiswahili, ushirikiano wa wadau hawa unahitajika sana.

### **5.3 Changamoto za utafiti**

